# Maisha ya Kiroho ya

# PADRE JORDAN

**Fr. Jozef Lammers    SDS**

Tafsiri ya Kiswahili na:

**Fr. Lazarus Msimbe, SDS**

**Maisha ya kiroho ya Padre Jordan**

na Fr.Jozef Lammers,SDS

Tafsiri ya Kiswahili na:
Fr. Lazarus Msimbe, SDS



Maisha ya kiroho ya Kisalvatoriani & Karama No. 09

*Kimetolewa na :*

Shirika la Mungu Mwokozi
Wasalvatoriani, Carmelaram
P.O Bangalore – 560 035
Karnataka , India

© copyright 2006 na
Shirika la Mungu Mwokozi

*Kimepigwa chapa na:*

Matha Prints, Bangalore, India
Tel. +91 80 41310081, 25536026
mathaprints@gmail.com www.mathagroup.org

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| | **Maelezo ya asili.** | **5** |
| | **Dibaji.** | **7** |
| | **Utangulizi** | **11** |
| | **Utangulizi** | **13** |
| | **Historia fupi ya maisha yake** | **15** |
| | **Kalenda yake.** | **17** |
| **I.** | **Ndoto na maono.** | **19** |
| **II.** | **Wito wake.** | **25** |
| | 1. Wito wake kama Mwanzilishi. | 25 |
| | 2. Juhudi katika wito wake | 27 |
| | 3. Mtazamo wake katika utume | 33 |
| | 4. Fikra juu ya tukio la Lebanon | 38 |
| | 5. Kuzingirwa na nguvu za giza | 40 |
| **III.** | **Maisha yake ya sala.** | **47** |
| | 1. Fumbo la sala | 47 |
| | 2. Mitindo muhimu ya sala | 48 |
| | 3. Fr. Jordan, mtu wa sala | 50 |
| | 4. Fr. Jordan na Ekaristi | 51 |
| | 5. Kuwa mtu wa sala | 53 |
| | 6. Sala inaunda nafsi | 55 |
| **IV.** | **Kukua katika maisha ya sala** | **61** |
| | 1. Mtu ana kuwa kadiri ya sala zake | 61 |

2. Kipindi cha utakaso 67
3. Sala ya Muungano kamili 72

**V. Maria katika maisha ya Mwanzilishi 77**
1. Uchaji ulio kama wa mtoto kwa Maria. 77
2. Tabia za ibada zake kwa Maria 80
a. Ugumu 80
b. Ukunjufu 81
c. Unyofu 82
3. Picha ya Maria. 83
a. Mama wa Mwokozi 83
b. Mkingiwa dhambi ya asili 84
c. Malkia wa mitume 85

**VI. Kumezwa na Matashi yasiyowezekana. 87**

**VII. Matunda ya kumtafakri Mungu zaidi katika maisha yake. 95**
1. Unyenyekevu kama msingi. 95
2. Kumtumainia Mungu kama Mwamba 99
3. Juhudi ya pekee kwa Roho. 104
4. Upendo wake kwa Msalaba. 109
5. Maisha yake yaliyojaa mateso 113
6. Alipenda Maandiko Matakatifu 120
7. Mkataba na Mungu 122
8. Nia ya Shirika 128
9. Sheria za kitume. 130
10. Wosia wake wa kiroho. 135

**VIII. Je Padre Jordan alimtafakari Mungu zaidi na habari zake? 139**

**IX. Mwanzilishi na wafuasi wake. 147**

# Maelezo ya Asili

**ANNALES SDS Salvatorianer -Chronik** – baadaye Annales SDS:

Inamaanisha Gazeti rasmi la Shirika, lililotolewa na Padre Pancratius Pfeiffer (1916- 1938) Mkuu wa Shirika wa pili.

**DSS** Inamaanisha mfululizo wa " Documenta et studia Salvatoriana" hutolewa na tume ya kimataifa ya Historia huko Roma. Mfululizo huu una maelezo mbalimbali. Nimekuwa natumia sana Matokeo ya Historia fupi ya Padre Timotheus Edwein, na matokeo yenye Kalenda, barua na mafundisho kutoka mikutano ya Padre Jordan.

**D** Inamaanisha kalenda ya kiroho (spirtual diary) kama ilivyotolewa katika sehemu ya XXII ya mfululizo wa DSS. Pia nimekuwa natumia kwa shukrani kubwa tafsiri ya kalenda ya Kidachi iliyofanywa na Padre Piet Cuijpers.

Kalenda imeundwa na vitabu vidogo vidogo vine vya 8 x12cm. Sehemu ya kwanza ina vipande viwili; ya kwanza ina kurasa 220, ya pili ina kurasa 122. Mnamo mwaka 1894, Padre Jordan aliunganisha sehemu hizi mbili pamoja, ili iwe rahisi kuchukua kwenye safari. Sehemu ya tatu ina kurasa 35 na ya mwisho 42. Angalia DSS XXI, ukurasa wa X.

**AS I** "Aussagensammlung I" Ina maana ya ushuhuda wa waliokuwepo wakati wa Mwanzilishi, uliokusanywa na padre Camillus Mohr huko Gurtweil katika miaka ya 1924-1925 kwa amri ya Padre Pancratius Pfeiffer, vitabu vya asili vinatunzwa katika ofisi kuu ya kutunza hati za

mwanzilishi na harakati za kumtangaza mwenye heri huko Roma ( APS, G – 18. 1+2)

**AS II** "Aussagensammlung II" inamaanisha ushuhuda ulioandikwa Octoba 1935, Padre Pancratius Pfeiffer alipeleka maswali ya msaada kwa mapadre mabruda na masista waliomjua mwanzilishi vizuri sana ili kuweza kuanzisha harakati za kumtanzangaza mwenyeheri. Alipokea majibu hamsini na tatu katika APS, N. 3. 1.3. Tunanukuu haya maneno ya wazi yaliyochapwa na kutunzwa katika ofisi ya kutunza hati ya Heverlee.

**SUMMARIUM** Ni muhtasari wa shuhuda zilizokusanywa katika majimbo mbalimbali wenye hatua kwa utangulizi wa kumtangaza mwenye heri katika rejea, kwanza tutaona jina halafu namba mwisho ukurasa.



**AGS:** (General Archive of the Society in Rome ) Ofisi kuu ya kutunza kumbukumbu iliyopo Roma

**APS** (Archive of the Postulation) Kutunza hati zinazohusu kumtangaza Padre Jordan kuwa mwenye heri huko Roma.

**DAS GEBETSLEBEN P. JORDANS** Ni kitabu changu nilichoandika ili kupata digrii huko Gregoriana Roma, kilitolewa 1957 ikiwa ni msingi wa kitabu hiki.

**TOLD TO THE AUTHOR** Maneno ya wazi ya ndugu walioishi pamoja na mwanzilishi na ambayo yamesikika na kukusanywa na mwanzilishi.

# Dibaji

Katika ofisi ya kutoa kitabu cha "P. Jordan und seine Grundunge" 1931 Padre Pancratius Pfeiffer alisema: "Sasa tuna kitabu cha kweli za kihistoria za Padre Jordan, lakini hii haitoshi. Mpaka hapa ni muhimu kitabu kitolewe ambacho kinatuambia nini kilichomhamasisha mwanzilishi kuendesha maisha kama haya na wapi amepata nguvu ya kusimama katikati ya majaribu".[1] Kwa uhakika tunahitaji kuwapa historia ya Mwanzilishi wetu na kazi zake, lakini hatuwezi kuishi kutoka jukwaa hilo. Tunaishi hasa kutokana na mwanga uliomwongoza yeye na ambao ametuachia sisi, kama mwanzilishi. Mwangaza huu pia unazuiwa na nyakati, lakini unaweza kupitishwa sababu una wakilisha wazi ubunifu mpya ambao una weza kupewa mtindo ya nyakati hizi.



Hakuna mwana historia atakayefanikiwa kufunua siri ya utu wake au kutoa tamko linaloeleweka la kazi yake kamwe kama hatumpi nafasi ya kutosha kwa uhusiano wake na Mungu. Mwanzilishi wetu amepata uzoefu Fulani na Mungu.Watakatifu hawajitangazi wenyewe.

Wanaeneza mwanga wa Mungu katika yeye ambaye utakatifu wowote unapata mizizi yake . Kama ilivyo katika hali ya maisha ya Mt. Yeyote, maisha ya Mwanzilishi ni upendo wa ujasiri kati ya Mungu na yeye. Mungu anayempenda mtu na mtu ndiye anayejibu upendo huu Mungu mwenyewe anatunga tuni ya maisha. Yeye mwenyewe ni asili ya utakatifu wote.Tukishindwa kusiliza tuni hii, kamwe hatutasikia sauti ya wimbo. Lazima tutafute undugu na Mwanzilishi wetu kwa kujaribu kufikiri kama

[1] Padre Donatus Blonde kwa mwandishi.

alivyofanya. Kama ukitaka kumjua yeye, lazima tumpende,; tumruhusu aseme nasi. Hatuwezi kusema kama alivyosema, lakini tunaweza kujaribu kuishi kulingana na uvuvio wake. Tunatumaini kuifanya tuni hii au mvuto huu wa Mwanzilishi utambulike. Karama ya Mwanzilishi wetu inafurika, ni kazi ya kutafuta asili yake katika nguvu inayosukuma ya upendo wa Mungu.

Kitabu hiki kina lengo la kuwa ufupisho wa maisha ya kiroho. Kina husika na mabadiliko ya kiroho yaliyotokea katika maisha ya mwanzilishi wetu.

Kweli za kihistoria hazitafsiriwi nje ya somo la historia katika sehemu ya kwanza, lakini nje ya mtazamo wa kiroho katika hali ya mvutano kati ya mwaliko wa Mungu na jibu la mtu. Kwa sehemu kubwa, yaliyo katika kitabu hiki yanatoka kwenye maandiko yangu kule Gregoriana Roma 1954: "Das Gebetsleben Pater Jordans." Muda umebadilika Teologia pia. Hii ndiyo sababu iliyonifanya nifikiri kuwa inafaa kuandika kitabu kipya.



Natumaini kuwa toleo hili litachangia kutunza ndani yetu moto uliomuhamasisha Padre Jordan. Kama mwanzilishi alisema: "*Sala ni pale ambapo ungepata moto na kuueneza duniani.* [2.]

Katika kitabu hiki, tunanukulu mawazo mengi ya Mwanzilishi sababu yana angaza sura yake kiroho. Maandishi yake lazima yatafsiriwe katika mtazamo wa wakati wake.

Elimu roho ni wazi ina uhusiano na mtizamo wa kihistoria na fikra za kipindi maalumu. Tamaa na kazi zake zimepata

[2] Chapter 05.01.1900, DSS XXIII,366 (katika Toleo la kiingereza la 2003)

sura katika hali halisi ya mila na desturi hiyo. Sasa ni juu yetu kutafsiri kwa wakati wetu mtazamo wa kiroho wa maisha yake.

Nafikiri ilikuwa furaha kubwa kukutana, katika miaka ya 1946-1954, mapadre na mabruda wengi wa mwanzo na kupata kuona ushahidi wao. Kati yao walikuwa mapadre Paulus Pabst, Fullgentius Moonen, Dorotheus Brugger, Marcellus Hilger na mabruda Giuseppe Capparella na Gabriele Manni.

**Fr Jozef Lammers SDS**



*Picha ya kwanza iliyopatikana ya Jordan  1861?*

# Utangulizi

"Mahali fulani katika nafasi kwenye madawati ya wanachama wengi wa familia ya Kisalvatoriani, kuna hazina zilizofichika za uzoefu wa kimaisha kama wasalvatoriani". Tamko hilo kutoka kwenye utangulizi wa kitabu cha kwanza cha maisha ya kiroho ya kisalvatorian na mfululizo wa karama zilizokuwa wazi. Kama kitabu hiki humfikiria kila mmoja wetu.

Elimu roho ya maisha ya Kisalvatoriani imeingizwa katika msukumo mkubwa wa kumfuata Mwokozi wetu na kumfanya ajulikane katika upekee na namna ya kisalvatoriani.

Elimu ya kiroho ya mpendwa mwanzilishi wetu ni moja ya zawadi nono ya Roho Mtakatifu kwa shirika na imekuwa njia ya wanaume na wanawake wengi kwa miaka mingi kufikia hatua kubwa ya utakatifu.



Moyo wa maisha ya kiroho ya Mwanzilishi ni pamoja na sehemu zake muhimu za kumtamfuta Mungu kwa undani, katika kujifungamanisha na Mwokozi na kupata maelezo ndani ya maisha ya kindugu na juhudi za kitume zilizotolewa katika kitabu hiki na Fr. Jozef Lammers, SDS

Jumuiya ya Wasalvatoriani wa Provinsi Ndogo Misioni ya Tanzania kwa kweli ina shukuru na kufurahia ushirikiano uliotolewa na mwandishi pamoja na halmashauri kuu na ruhusa iliyotolewa kwa kuchapa toleo hili la Kiswahili la kitabu hiki huko India.

**Fr. Lazarus Msimbe, SDS,**
Masasi, August 2006.



Francis Jordan akifanya huduma ya Kijeshi 1868

# Utangulizi

Mkutano Mkuu wa XVII wa Shirika letu la kitawa uliweka mwongozo kwa Wanachama wetu wote wa kuamsha uwepo wetu kama Wasalvatoriani. Tunaweza kufanya hivyo tukikua katika maisha yetu ya kiroho na kuishi kiaminifu zaidi kadiri ya karama ya Mwanzilishi wetu, Mtumishi wa Mungu, Padre Francis Maria wa Msalaba Jordan.

Nilipokuwa mlezi wa wanovisi kwa miaka minne huko Namiungo hatukuwa na kitabu chochote cha Kiswahili juu ya swala hilo muhimu. Tangu miaka walau 20 vimeandikwa vitabu vingi vinavyotufunulia uroho wetu wa kisalvatoriani. Lakini bado tunayo mahitaji makubwa ya kufanya utafsiri kwa lugha ya kiswali wa vitabu vingi juu ya historia yetu, karama, na uroho wetu. Kwa furaha tunakaribisha utafsiri wa kitabu cha Padre Jozef Lammers, SDS kinachoitwa "Maisha ya Kiroho ya Padre Jordan".



Kama ninavyojua ni kitabu cha kwanza katika kiswahili juu ya swala hilo. Mheshimiwa Padre Lazarus Msimbe, Mkuu wa Provinsi Ndogo Misioni ya Tanzania alifanya kazi hiyo ya utafsiri wakati alipokaa katika Makao Makuu yetu hapa Roma kwa matibabu. Ingawa alifanya hapa operesheni na alikuwa na maumivu mengi alijitoa kwa kufanya hivyo. Kwa hiyo tunamshukuru kwa moyo wote kwa kazi hiyo. Kweli anastahili shukrani zetu za pekee.

Ninatumaini ya kuwa kitabu hiki kitakuwa msaada mkubwa kwa Wasalvatoriani wote wanaojua kiswahili, watawa na walei, kwa kujua kinaganaga zaidi uroho wa Mwanzilishi wetu ambao ni pia uroho wetu. Tukiwa na uroho huo tutakuwa Wasalvatoriani wa kweli, tutaishi maisha yetu ya kisalvatoriani kiaminifu zaidi, tutatimiza utume wetu kwa juhudu kubwa na kuvutwa zaidi kwa

utakatifu. Kwa hiyo, Msomaji Mpendwa, ninakuomba sana upokee kitabu hiki kwa moyo, ukakisome mara kwa mara na ukiweke kwa fikra zako. Kiwe rafiki yako na kiongozi katika juhudi zako za kukua vizuri zaidi katika maisha yako ya kiroho ya kisalvatoriani.

Wako katika Mwokozi,

**Padre Andrea Urbanski, SDS**
Mkuu wa Shirika la Mungu Mwokozi.

Roma, Agosti 22, 2006

# Historia fupi ya maisha yake.

Yohane Baptist Jordan alizaliwa Gurtuweil (Baden) Juni 16, 1848.[3] Wazazi wake walikuwa maskini sana katika kijiji na hawakuwa na tamaa ya mali. Kiasi kwamba hatuwezi kusema juu ya maisha ya ndani ya kidini.

Baptist alikuwa na kaka wawili ambao waliachana naye kwa hasara yao. Alipokuwa na umri wa miaka 14, baba yake alifariki kutokana na ugonjwa alioumwa kwa muda mrefu, ulikuwa matokeo ya ajali. Hivyo Baptist alikuwa daima kama mbwa mkali kati ya wenzake. Baada ya kifo cha baba yake na Komunyo ya kwanza, amekuwa makini zaidi na kupenda kuwa faraghani. Kwa sababu ya kutawaliwa katika ujana wake na mwelekeo wa kusoma kupita kiasi, aliumwa ugonjwa wa mishipa ya fahamu unaotokana na kazi nyingi za maisha yake yote.



Baada ya wiki sita za huduma ya kijeshi alipelekwa nyumbani kwa sababu ya kutokuwa na uwezo, ingawa vita ilikuwa inaendelea. Ingawa daima alitamani kuwa padre, hakuweza kusoma kwa sababu ya umaskini wa familia. Hivyo akawa mpiga rangi na mpambaji. Hata hivyo katika umri wa miaka 21, aliamua kuwa padre. Shukrani kwa masomo ya binafsi aliweza kuruka baadhi ya madarasa shuleni. Halafu alienda chuo kikuu cha Friburg kwa miaka mitatu na alipewa upadrisho 1878 baada ya mwaka wa mwisho kwenye seminari ya Freiburg.

Alikuwa mvulana wa umri wa kati, jasiri na aliyejengeka kishupavu. Tathmini ya tabia yake iliyofanywa na mhusika wa seminari ilikuwa fupi lakini wazi: "Hakuwa na umaridadi, alikuwa mpole sana, kidogo mzito na mweye

[3] Kwa habari zote kuhusu ujana wake angalia ASI na DSS XIII- XV

kusita sita, lakini mchaji, mkunjufu pamoja na mwelekeo wa kufikiri mno. Alifanya kazi kwa juhudi sana.[4]

Alikuwa mtu mchangamfu, lakini namna yake ya kutenda mambo ni ya pekee wakati mwingine. Kama mjumbe wa baraza la wanafunzi alikuwa akikaa na glasi ya bia mbele yake lakini hakumaliza.[5]

Wakati wa mapumziko kati ya vipindi, wanafunzi wa chuo kikuu cha Freiburg walitembea kwenye bustani au kwenye veranda, lakini yeye alibaki darasani akiandika lugha ya kale sana ya kihindi au lugha za mashariki ubaoni. Alichukua muda mfupi sana kwa mapumziko. Katika mazoezi ya viungo hakuwa na upinzani.

Askofu wake alimpeleka Roma, ili akajifunze lugha za mashariki, kwani alikuwa na kipaji cha lugha. Kule amekutana na watu wenye utume mkubwa na amejifunza na kujua matatizo mengi ya kidini ya wakati ule. Sababu ya hitaji la kiroho na watu wengi kutojua dini alijawa na tamaa kubwa ya kuanzisha Shirika Funzishi, ambalo lingemtangaza Yesu mahali pote, kwa njia zozote zinazowezekana, kama Mwokozi wa ulimwengu.



Hivyo Desemba 8, 1881 Shirika la kitume lilianza Roma pamoja na mapadre wengine wawili. Desemba 8, 1888 waliweza kuanzisha tawi la wanawake la Shirika pamoja na Mama Maria wa Mitume. Wakati wote wa maisha yake alibakia Roma. Mwaka 1915 alikimbilia Uswisi sababu ya vita.Alifariki Septemba 8, 1918 huko Tafers Uswisi.

4. DSS XII, 157
5. Dean Josef Blattman, barua ya 20.05.1928 kwa Fr. Bonaventura Schweizer

# Kalenda yake

Mwanzilishi wetu aliandika mawazo yake binafsi tangu Julai 1, 1875 mpaka april 14, 1918 miezi michache kabla hajafa.Mawazo hayo yanaitwa "Kalenda yake ya Kiroho" lakini siyo kalenda katika maana halisi ya kalenda.Siyo hadithi ya maisha ya kila siku ya Mwanzilishi.Kuna miezi hata miaka bila mawazo yeyote.

Hakuna vitabu vilivyoandikwa vizuri, hakuna kumbukumbu, bali vipande vya maandishi yasiyo katika utaratibu.

Asilimia 20% tu ni mawazo yake mwenyewe, 30% ni nukuu kutoka maandiko matakatifu na 50% ni nukuu kutoka waandishi wa kiroho. Tunaendelea kuiita "Diary" Kalenda ya kiroho.Katika kalenda yake Mwanzilishi hakujiangalia mwenyewe, bali anayotumia kusimulia historia yake ya kiroho na masumbuko ya kuanzisha Shirika yanakuja kutokana na ugumu wa kina. Mara nyingi anatafuta kumjua Mungu kwa kina, na namna ya kumshukuru Yeye, jinsi anavyoyaongoza maisha yake, na kwa namna ambayo angejibu sauti ya Mungu kwa uaminifu zaidi. Lazima tutunze kwa unyeyekevu sana akilini kwamaba hitoria ya maisha ya mwanzilishi wetu inajulikana kwa yule tu Ambaye amekuwa akimtumikia mpaka mwisho, yaani Mungu.



Mwisho wa maisha yake akatoa kalenda yake kwa Padre Victorinus Plieger aliyekuwa anamtunza. Alimhimiza ahakikishe kuwa kitabu hicho hakiendi kwenye mikono ya mtu mwingine, sababu alisema," kina mambo kati ya Bwana Mungu na mimi tu"[6] Kama tukitambua hili, itaeleweka wazi

[6] Salvatorianer- Chronik,vol 3 (1919) No. 2, 182

kwamba ufafanuzi mzuri wa kitabu hiki cha kiroho huthamini kuwa msomaji pia ana uhusiano wa kiroho na Mwanzilishi. Hisia hii ni sharti kwa kuelewa vizuri kalenda yake. Lazima tujaribu kujiangalia wenyewe katika wakati wake, katika teleojia yake, katika mtazamo wake wa maisha ili kuweza kugundua njia aliyotumia Mungu katika maisha yake.

Kweli ni muhinu kujifunza kusoma kurasa zisizo na kitu katika kalenda yake na kuruhusu alama za kushangaa zijisemee zenyewe. Vifupisho, nukuu, na marudio kurasa zilizo wazi au kuachwa,vyote vina kitu cha kutuambia. Kalenda inatuonyesha namna ya mwongozo wa Mungu (unavyopanda) polepole unavyopata mkono wa juu,kwa kweli, mwandishi hayatoi hayo kutoka kwake, Mungu anamvuta Mwanzilishi Kwake. Hii ni alama ya fumbo la Kalenda ya kiroho ya Mwanzilishi. *"Ina mambo kati ya Bwana Mungu na mimi tu."*

# I

# Ndoto na Maono

Kama tukitaka kusema juu ya maisha ya mwanzishi wetu binafsi, tunatakiwa kuwa na kiasi. Kwa uaminifu lazima tutambue kwamba kamwe hatutaweza kujua kwa kifupi namna neema za Mungu zinavyofanya kazi ndani ya mtu. Mungu daima anaheshimu uhuru wa mtu.Hataweza kuingilia mara nyingi katika maisha ya mtu yeyote. Kwa upande Mwigine tunajua kwamba Mungu anashughulika na Wokovu wa ulimwengu bila kuchoka. "Katika Yeye tunaishi, tunatembea na tupo".[7]

Uzoefu wa mwanzo wa Padre Jordan kwa Mungu ulitokea wakati wa komunio yake ya kwanza April 7, 1861. Alikuwa na miaka 13 wakati huo. Wakati wakomunio alihangaika, na hali ya kutotulia ilijitokeza. Baadaye Paroko alipouliza juu ya hali hiyo, alisema "Singeweza kusaidia, kulikuwa na njiwa mweupe ambaye alikuwa akiruka taratibu juu ya kichwa changu na baadaye akaruka juu mbinguni."[8]

---

[7] Mdo 17, 28

[8] Eduard,AS II, no.20, DSS XIII, 85 – 90

Swali linalotupasa kuuliza sio: kweli alimwona njiwa? Hilo ni tukio tu. Swali ni: nini kilitokea katika moyo wa Baptist wakati ule? Kwa uhakika alibadilika tangu siku ile,na wenzake,na wanakijiji walishuhudia badiliko hilo.Aliachana na wenzake,alijenga banda katika msitu ili apate nafasi ya kusali kwa uhuru.Tangu siku ile, alipokea Komunio Takatifu kila Jumapili, kitu ambacho ilikuwa si kawaida kwa wakati ule.Vilevile alikwenda kuungama kwa uaminifu kila baada ya wiki tatu.Paroko na wenzake walishangaa kwa badiliko hili la kiroho.Hadithi ilienea sana kijijini kiasi kwamba,baadaye alipotaka kuwa Padre,wengine walimuuliza kwa uchokozi:”Kuna njiwa anayekugusa kichwani mwako tena?”[9]

Mwanzishi wetu mwenyewe alitilia maanani hali hii ya kiroho kuwa kama sehemu ya kubadilisha maisha yake. Baadaye, alimwambia aliyemfuata kwamba alibadilika kabisa baada ya Komunio ya kwanza na baada ya kifo cha baba yake.[10] Tangu wakati huo Paroko wake alikuwa makini sana kwake. Mara moja alimwangalisha: “Baptist, nisikilize. Utakua na kuwa au mtu mwema sana na mwenye uwezo, au kinyume chake.”[11]



Katika ujana wake, mwanzishi alikuwa na ndoto mbalimbali. Anaandika katika kalenda yake:Mara nikiwa katika ndoto,nikifuatwa na namba kubwa ya watu, na nilikuwa nakimbia,Maria pamoja na mtoto Yesu katika mikono yake,alitokea kwangu katika mwanga wa utukufu.Aliniangalia kwa upendo kiasi kwamba nikazama kwenye magoti yangu tayari kuruhusu mateso yale yaniangukie.[12]

9 DSS XIII,85-90
10 Fr. P. Pfeiffer, Mitteilungen, APS I, 85
11 JohanMuller (schoolmate), AS I, no.129
12 D I / 121

Wakati mwingine, nililazimika kuvuka ng'ambo ya shimo kubwa, na ni njia pekee,kama ninavyoamini kuvuka ng'ambo ilikuwa kupita juu ya ubao.Halafu nilichukuliwa ng'ambo ya shimo na kitu cha kiroho kisichoonekana,ambacho sikukiona lakini nilihisi na kwa furaha kufika upande wa pili wa shimo,kile kitu kikaniacha.Tukio la kwanza lilitukia mwanzoni mwa masomo yangu baadaye tukio la pili…[13]

"Mwanzoni mwa masomo yangu"hakuna muda wazi uliooneshwa. Ilikuwa pengine kati ya mwaka 1870, alipokwenda chuoni Konstanz,au 1874 alipoanza masomo yake ya chuo kikuu cha Freiburg. Aliziwekea alama ndoto hizi katika kalenda yake wakati wa Pasaka 1878, baada ya kuwa nazo kwa muda mfupi. Hii inaonesha kuwa alizipa kipaumbele kama alama ya neema. Kwa uhakika aliziandika ili ziweze kuwa chanzo cha nguvu na matumaini.

Mwaka 1874,baada ya mitihani yake ya Taifa,Padre Jordan alisafiri kwenda Roma. Miaka minne baadaye, akikumbuka safari hii, anaandika kwenye kalenda yake: Kamwe usisahau muda ule na jakamoyo uliohisi katika makatakombi ya Roma.[14]



Anaeleza uzoefu huu wa kiroho katika kalenda yake kama ifuatavyo: Enyi watu, nani anaweza kujua nini ulichopata katika mahali hapa patakatifu.Ah, utakatifu gani, uzuri gani wakati mabikira watakatifu,walipovaa nguo nyeupe na mishumaa mikononi mwao,walipita pale,wakisali na kuimba,,wakati katika kipimo cha chini mmoja aliwaona wakitembea mbele. Ah, usafi na imani ya kweli ya wakristo wa kwanza. Hakuna anayeweza kufikiri hivyo! Mtakatifu sana na Baba wa milele,tujalie ili tuweze kujiunga kwa haraka na hawa wafiadini watakatifu! O wakati wa furaha! O wakati mtakatifu! O wakati usiosahaulika![15]

[13] D I / 121
[14] D I / 107
[15] D I / 117

Huu ulikuwa wakati wa imani kubwa kwake,"wakati usiosahaulika" kama alivyoandika miaka saba baadaye. Wengine wanasema kuwa ilikuwa maandamano ya masista watawa,lakini wakati ule hakukuwa na maandamano katika makatakombi.Anazungumza juu ya imani ya Wakristo wa kwanza.

Bado alikuwa na ndoto nyingine alipokuwa mashariki ya kati. Mwezi Mei,1, 1880, alifika Ain Warka, km 28 kaskazini mwa Beirut,huko Lebanon.Anaandika kwenye kalenda yake: Ewe sehemu yenye miti na chemchemi uliyebarikiwa kati ya jangwa.[16]

Tarehe 2 Mei, siku moja baadaye, hakuandika kwa utaratibu juu ya nafsi ya tatu: Alipolala, kando yake alisimama Mt.Aloys aliyeshikwa homa karibu na kifo,na alimgusa kwa unyenyekevu wakati Mt.alipoamka na kumbusu yeye aliyemgusa.[17]



Nukuu hii haiko wazi na ina mtindo wa pekee. Inaweza kuwa ni nukuu nje ya kitabu, lakini kwa vile iliandikwa kwa kilatini lugha ambayo Mwanzilishi aliijua vizuri sana kwa urahisi tunaweza kupenda nukuu yake binafsi. Nani atakayetuambia alikuwa na maana gani katika sentensi hii? Anataarifu juu ya ndoto ya mwisho: Tarehe 12,Octoba, 1885, wakati sikukuu ya Mt.Francis ilipoadhimishwa kwetu, usiku ule katika usingizi nilimwona Mt.Francis wa Assisi, aliyevaa kanzu fupi. Nilikuwa nasali ili abariki Shirika na alinibariki mimi na Shirika, halafu niliamka.[18]

Tunaweza kuiweka ndoto hii katika mtindo uliotolewa.Wakati Padre Jordan anaishi Ujerumani, muungamishi wa Shirika la masista, aliloanzisha, alilalamika kwa makamu wa Mkuu wa Shirika Roma juu ya baadhi ya

[16] D I / 156
[17] D I / 156
[18] D I / 184

fujo dhidi ya masista. Muungamishi alimlaumu mwanzishi,na matokeo yake ni kwamba wakubwa walimkataza kuchanganyika na masista.

Padre Jordan alikuwa na uhakika wa mambo na aliona kwamba ni lazima ajitetee na aliandika kwenye kalenda yake: Nilikuwa na nia njema nilipoamua kuanzisha na kuhamasisha Shirika la masista tarehe 10.10.1885. Rota pia alitamani na kutaka nifanye hivyo.[19]

Hii ni hali ambayo Padre Jordan alijikuta anapambana nayo. Hivyo ilieleweka sana kwamba Mt.Francis alimtokea katika sikukuu yake. Alichagua jina la Francis kama jina lake la kitawa na mkuu wa masista aliitwa Francisco.Hata hivyo, Octoba 13, ilikuja amri ya kutengana kwa kudumu. Aliandika katika barua kwa Kardinali Paroch, Kardinali msaidizi wa Roma: Mungu anajua namna nilivyoteseka katika miaka mitatu iliyopita, zaidi kiasi cha kupata karaha katika maisha.[20]



Mwanzishi wetu aliishi ndoto na maono haya kama katika hali ya neema. Walimsaidia kuyashinda magumu yasiyotajika.Mt.Bernard lazima atakuwa ameishi maisha yanayofanana na haya,kama alivyoandika:"Ukitembelea moyo wetu, ukweli unaanza kuangaza, ubahili wa dunia unaanza kupotea na moto unavamia moyo wetu."[21]

Yatupasa tuwe waangalifu sana tunapoandika juu ya ndoto na maono. Tunaweza kujiuliza sisi wenyewe: Je, ufafanuzi huu haupo katika misingi ya uzoefu au hisia tofauti, ambayo haiwezi kuzuiliwa? Tayari angalia kwenye historia ya maisha ya kiroho tunaambiwa wazi kwamba ndoto katika maisha ya watakatifu ni kitu cha lazima. Zinatokea karibu kwa waanzishi wote: Benedict, Francis, Don Bosco,... Ndoto na maono, ingawa hii haina uhakika wa moja kwa moja, sio kitu kilichotungwa

[19] D I / 183

[20] DSS X, no.200 ( bila tarehe )

[21] Wimbo: "Jesu, Rex admirabilis", sehemu ya pili

kwenye mawazo tu,bali ni matukio yanayoweza kutokea kwa watu. Zaidi ya hayo, Maandiko Matakatifu yamerudia kutaja ndoto: Yakobo kule jangwani, ndoto za Yosef, na maono makubwa ya Manabii. Malaika anaongea na Yosef, anamtokea Yesu, Petro na Paulo. Katika Maandiko Matakatifu, Mungu anaongea na watu kwa njia ya ndoto. Kusikiliza ndoto sio uchawi, bali ni kukutana na Mungu.Wakati mwingine ndoto na maono hutokea kwenye matukio, na matokeo yake yanaweza kwenda mbali katika historia.

Kwa njia ya ndoto, Mungu anaweza kutuonesha nini anataka tufanye na njia ambayo tungeichagua. Lugha ya Mungu ni amani,furaha,usalama na ahadi ya msaada. Pia, Mungu anaweza kuongea nasi kwenye moyo wetu wakati wa usiku. " Namsifu bwana aliye mlinzi wangu, hata wakati wa usiku moyo wangu wanituma kufanya hivyo."[22] Kufafanua tukio lenye fumbo hutegemea mtu mwenyewe alivyo. Katika ndoto zetu, ukweli wa kiroho unaweza kutengeneza njia katika maisha yetu. Haikuelezwa kabla kwamba ndoto ziwe na ukweli kidogo kuliko vile tunavyoona kwa ufahamu. Katika ndoto zetu tunaweza kuona alama jinsi maisha ya Padre Jordan yalivyofungamanishwa na Mungu, kwa ndani zaidi kiasi kwamba muungano huu haukuvurugwa na usingizi. Ndoto ni ufafanuzi wa binadamu wa hali ya kimungu ambayo Mt.Tomas anasema: "Hakuna ulimi unaoweza kuiweka katika maneno,hakuna barua inayoweza kuelezea, ni wale tu ambao wamepata uzoefu wanaweza kuamini nini maana ya kupendwa na Mungu ."[23] Ndoto kama hiyo inaweza kung,arisha maisha ya mtu.



Baadaye, Mwanzilishi hafanyi marejeo zaidi kwa ndoto na maono. Labda hakutaka zaidi, sababu alikuwa mwaminifu sana kwa uzuri wa uwepo wa Mungu.

[22] Ps. 16,7

[23] Wimbo: "Jesu, dulcis memoria", sehemu ya nne

# II

# Wito wake

## 1. Wito wake kama Mwanzilishi

Inaeleweka kwamba Padre Jordan tayari alifikiri kuanzisha Shirika jipya muda mrefu kabla hajapata upadrisho.Kwake, hii ilikuwa ni kazi ya maisha.

Tayari tangu nilipokuwa na miaka 18, alimwambia Padre Pancratius, nilikuwa na mvuto wa kusikia sauti ndani yangu iliyoniambia kuwa Bwana wetu mwema alitaka kitu cha pekee toka kwangu.[24]

Baadaye, alimwambia mmoja wa mapadre:Nilipokuwa nasafiri kama mpiga rangi msaidizi katika miji mikubwa ya Ujerumani na kuona mahitaji makubwa ya watu wengi, hasa katika bandari ya Bremen,niliamua kwanza kusoma ili niweze kuwasaidia watu wanaoteseka kama Padre.[25]

---

[24] Vitini toka Fr.Pancratius Pfeiffer, APS I, 85
[25] Fr. CallixtusWaizenhofer, AS II, no. 6

Rejea ya kwanza inayohusu uanzishaji wa Shirika inarudi nyuma kwenye mwaka 1878 na tayari ni wito wa sala: Kila siku kwa wakati mwafaka chukua muda wa kushauriana na Mungu.Umwombe akuangaze ili utimize mapenzi yake matakatifu na kwamba Ajulikane na kupendwa na wote.[26]

Kadiri upendo wa Kristo ulivyokua ndani yake, ndivyo hamu ya kuwaruhusu watu washiriki upendo wake ilivyokua: Yesu Kristo, unipokee kama chombo chako,na unitumie kama upendavyo, nitazame kwa msaada wa neema zako, niko tayari kufa kwa ajili yako.[27]

Sababu mbili zimejitokeza mara nyingi: Kuyafanya mapenzi ya Mungu na kujishughulisha ili kwamba Yesu afahamike na kupendwa na kila mmoja. Toka hapo analeta wazo lake alipendalo alilolipa kipaumbele, wazo ambalo baadaye lingekuwa msemo mfupi wa maana sana kwa Shirika, chini ya utawala wa Padre Pancratius Pfeiffer: "Huu ni uzima wa milele, kwamba wakujue wewe, Mungu mmoja wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma."[28]



Angependa kuwaleta watu wote kwenye asili ya wokovu, kupeleka wokovu kwa ulimwengu mzima: Angalia mataifa yote, nchi, na lugha za dunia nakuona kuna kazi gani ya kufanya kwa heshima ya Mungu na kwa wokovu wa watu.[29]

Anatambua wazi kwamba hana nguvu ya kushughulika na hili hitaji kubwa la roho peke yake:Ee Bwana, katika wakati mgumu kama huu njia za ziada ni lazima ili,kwa msaada wa neema zako, kutuliza hali ya dhambi.[30]

---

[26] D I / 59
[27] D I / 12
[28] D I / 83 Yn.17.3
[29] D I / 63
[30] D I / 61

Miaka miwili baadaye, kama mwanafunzi Roma, aliandika: Uovu umekithili kiasi kwamba Padre Matatias aliweza kushangaa: “Ole wangu! Kwanini nimezaliwa ili kuona uovu wa watu wangu na uovu wa mji mtakatifu,na kuishi pale wakati unaanguka katika mikono ya adui”[31] Polepole anaanza kugundua kwa namna gani angeweza kuwasaidia watu kwa njia bora zaidi. Anaandika katika kalenda yake wazo la Paroko wa Ars: “ Mara nyingi nafikiri kwamba watu wengi waliopotea, wamepotea sababu ya kukosa mafundisho.”[32] Ukurasa mmoja zaidi anaandika.: Mafundisho,mafundisho,fanya ulichonacho akilini, kifanye, kama ni mapenzi ya Mungu![33]

## 2. Juhudi katika wito wake

Ingawa Padre Jordan aligundua polepole kwamba aliaminiwa kwa utumishi wa Mungu alibaki katika hali ya Mashaka.Aliogopa juu ya utume mkubwa. Wakati mwingine, angependa kutoroka, kama Musa na Yona Mbali kutoka uwepo wa Mungu.



Hata hivyo,Padre Jordan anajisikia kubanwa na mwaliko wa Mungu: Jiandae kwa migongano ya kila aina, kwa vyovyote mateso ya kimwili au ya kiroho yakikuangukia katika kutekeleza kazi yako, daima, mtumaini Mungu, kwa Yeye na kwa njia yake peke yake ungeweza na unaweza kuikamilisha. Kamwe usiwe na woga kuhusu hilo, lakini uwe na furaha kama unaweza kuteseka zaidi kwa ajili ya Mwokozi wako.[34]

[31] Skizze, Archief II, 1,Das Gebetsleben P.Jordans, 36

[32] D I / 78

[33] D I / 79

[34] D I / 84

Padre Jordan na watakatifu wanakwenda njia ya uwepo wao si kwa kuchaguliwa katika Mwanga wa neema, ila katika kusita na Mashaka. Kuna muda, wanaendeshwa kwa ndani na juhudi takatifu, na wakati mwingine, wanajua upweke katika giza la usiku wa Mashaka. Kwa hiyo mara nyingi anakamatwa katika ugumu wa ajabu kati ya ukuu wa neema na udhaifu wake binafsi.

Juhudi hizo zinaonekana wazi katika maandishi yake: Usidharau kushughulika na mpango uliandaliwa, kwa sababu uliamuliwa na kuwekwa sawa, kumbuka,juu ya matukio ya mara kwa mara. Kwa mwenyewe huwezi kufanya kitu lakini naweza kufanya yote katika Yeye anayenipa nguvu.[35]

Na sehemu nyingine: Pima vizuri kabla hujaacha kazi hiyo. Fikiri juu ya muda ambao ulijisikia hasa kwa kazi hiyo.[36] Chukua kazi hiyo iliyopangwa kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa roho.[37] Je, Mungu mpendwa hakukupa alama wazi amekuita kwa sababu gani, anapokupa katika mazoezi ya nguvu kwa ajili ya roho furaha Kubwa ya kiroho, faraja na amani ya moyo?[38] Fikiria tena ni furaha gani wazo la ufahamu ule ulioletwa tayari kwako. Katika wakati ambao kwa kweli sikuwa na hamu kuhusu jambo hilo,vishawishi vilinisumbua.[39] Usife moyo katika harakati zako,hata kukiwa na vizuizi na mateso,kudhaniwa vibaya, dhihaka, dharau,na mateso yote yanayoweza kukujia, ishi tu katika muungano wa upendo na Mungu na utafakari mara nyingi juu ya mifano ya watakatifu,mtumaini



[35] D I / 127
[36] D I / 129
[37] D I / 130
[38] D I / 134
[39] D I / 152

Mungu na umpe utukufu wake Yeye tu, umeshapata baraka na bado mateso mengi zaidi.[40]

Kipindi hiki cha kutafuta na Mashaka kinaisha kwa miaka miwili na nusu. Septemba 19,1878,anaandika: " Anzisha Shirika la kitume."[41] Tayari baada ya miaka mitatu baadaye, Desemba 8, 1881 alianzisha Shirika Funzishi la kitume.

Swali linakuja: Namna gani Padre Jordan amekuja kuamini kwamba, kwa namna hii, alikuwa anatimiza mapenzi ya Mungu? Imetokea kwake kama ilivyo kwa Waanzilishi wa Mashirika wengi: Mungu ameamsha ndani yao tamaa na kwamba anawapa amani zaidi,furaha na uhakika, kwamba hawawezi kuhofu tena.

Padre Jordan lazima alikuwa ameelewa hili,sababu ananukuu katika kalenda yake: Ni Mungu pekee anayefariji roho bila sababu yoyote inayotangulia, kwani ni kazi sahihi ya Muumbaji kuingia katika kiumbe chake na kukibadilisha kabisa katika upendo wake. (Mt. Ignasius wa Loyola )[42]



"Bila sababu inayotangulia" maana yake ni kwamba faraja ya ndani kabisa haiwezi kusababishwa na nguvu za kiakili, au kwa nguvu ya utashi, lakini hutokea "mara moja" "kwa haraka" na bila kutegemewa.

Katika siku hizo, Padre Jordan anaandika mara kwa mara juu ya nyakati hizo za faraja: Ee Mungu wangu na yangu yote, nakuwa na utulivu mkubwa ninaposikia sauti yako! ~ Ee Bwana unikumbushe kama, kwa bahati mbaya, ningesahau; kamwe isingetokea![43]

---

40 D I / 151
41 D I / 145
42 D I / 37
43 D I / 139

Novemba 10,1878, baada ya Ekaristi Takatifu: Kamilisha kazi hiyo kwa heshima ya Mungu na wokovu wa roho. Ee Yesu, ewe harufu nzuri ndani yangu, mdhambi! Ewe unayenipenda!44 Na: Ni mapenzi ya Mungu kwamba ufanye kazi hiyo. Desemba 27,1879 baada ya Misa Takatifu: na fikiri ulivyofanya wakati ule baada ya Komunio.[45] : Baada ya misa Takatifu nilihisi faraja kubwa juu ya kazi iliyokwishapangwa.[46]

Akiwa Lebanon, kwenye Konventi ya Mwokozi, anaandika: Kwa kurudia baada ya Misa Takatifu kuwa na wajibu maalum na furaha.[47]

Ni mapokeo ya zamani sana na yanayodumu katika Kanisa kufikiri Ekaristi kama kisima cha hali ya fumbo toka chini kabisa mpaka juu kabisa. Vilevile,Mungu Ameongea wazi kwa Padre Jordan , ili asihofu tena bila kujinyima mwenyewe. Ah, usidharau kutekeleza nia yako ambayo Mungu mpendwa ameionyesha kwako kwa kukupa majitoleo mengi na upendo kwa mambo yasiyo ya ulimwengu huu na kadhalika. Usichelewe, kadiri utii usivyokurudisha nyuma, wahi.[48] Wazo la uanzishaji kwake, kama anavyoandika mwenyewe: Kama mionzi ya mwanga wa mbinguni inavyofanya upya na kutakatifuza.[49] Jiandae na kazi hiyo mara moja, sababu ni ustawi wako, unaokufanya unawiri katka mwili na roho.[50]



Maneno haya yamelenga kwenye hisia za ndani za utawa zinazotoka ndani kabisa ya roho ambapo, Ruusbroec

[44] D I / 149
[45] D I / 151
[46] D I / 154
[47] D I / 156
[48] D I / 163
[49] D I / 156
[50] D I / 134~135

anasema,kiini cha binadamu kinakaa ndani yake “super being”.

Catharina wa Siena anaita mahali hapo “nyumba ya ndani ya moyo” na Theresa wa Avila anasema juu ya “ngome ndani ya mji” ni madhabahu ya ndani ambapo wokovu unatolewa. Kwa kweli, Mungu si matokeo ya uzoefu wetu wenyewe,ni kinyume chake kabisa. Sio uzoefu wetu unaotuongoza kwa Mungu, lakini Mungu anajifunua mwenyewe katika hisia au uzoefu wetu.

Katika mwanga wa ufafanuzi huu tungependa kusimama kidogo kufikiri juu ya “ uzoefu wa Lebanon” wa Mwanzilishi wetu.

Katika muda fulani, kulikuwa na hamu kubwa katika huu “Uzoefu wa Lebanon” Fr. Beda Alfred Schneble anasema “Huu uzoefu wa Lebanon ni msemo wa kisasa wa mwanzo wa hadithi, iliyoanza baada ya kifo cha Mwanzilishi na ambapo kitabu cha Fr. Jozef Lammers kimechangia kwa vikubwa.”[51] Swali ni kama kweli uundaji wa hadithi hiyo haukustahili.

Kiini haswa cha uzoefu wa Lebanon umefupishwa vizuri katika kitabu cha jubilei ya 1931: “Wiki ambazo Mwanzilishi alikaa Lebanon zilikuwa pia ni wiki za sala ili kuweza kujua wazi kama ufahamu wa ndani wa kuanzisha Shirika ulikuwa ni mapenzi ya Mungu.”[52]

Wakati huohuo ni wazi kabisa kuwa uzoefu wa Lebanon hauwezi kufungwa na mahali au wakati mmoja. Ni tukio la neema, lililoenea wakati wote alipokaa huko Mashariki ya kati. Sehemu ya kuanzia fikra zaidi inalala katika maneno ya Padre Pancratius Pfeiffer kwenye Salvatorianer Chronik



[51] Study of Fr.A. Schneble in Historica SDS, no. 78 | 790, 27.02.1978

[52] Fr.Theophilus Muth, Die Salvatorianer, Vienna 1931,5~6

ya 1919: "Mheshimiwa Padre aliniambia mara moja kuwa,alipokuwa kwenye kilele cha Lebanon na kuangalia nchi Takatifu na kuruhusu mahitaji yenye sura tofauti yapite katika akili yake,alisikia katika akili yake vizuri zaidi kuliko wakati wowote,maneno ya Mwokozi: "Huu ni uzima wa milele,kwamba wakujue wewe,Mungu mmoja wa kweli, na Yesu Kristo, uliyemtuma." Na alijisemea mwenyewe "Ndio, Shirika ambalo lingeanzishwa lazima likutangaze, Ee Mungu, na Mwana wako wa pekee."[53]

Uzoefu huu na nukuu lazima ziwe na mtazamo mzuri kwake.Katika katiba yake ya kwanza ya 1882, tunapata nukuu ya Injili ya Yohane kenye utangulizi,pia ni neno muhimu katika sheria ya utume ya 1884.Katika kile kilichoitwa "Smyrna~text" ya julai 31,1880, pia ni jina, pamoja na Dan. 12:3.



April 28,1941 Padre Pancratius Pfeiffer alichapa hati fupi aliyofanya mwanzoni mwa maisha yake ya upadre juu ya kile alichomwabia Padre Jordan.Anaandika: "Huko Lebanon alipata uhakika kuwa Shirika lake alilopanga lingeanzishwa, hata kama yeye asingerudi Ulaya salama."[54]

Bado tuna asili ya zamani sana toka 1895, ambapo mlezi wa Wanovisi, Padre Crysologus Raich aliwaambia wanovisi wake:"Wakati mheshimiwa Padre alipokuwa akisali kwenye Kaburi Takatifu~aliniambia hivyo~alikuwa na ufunuo kwamba Shirika ambalo alikuwa anapanga, lingeanzishwa kwa uhakika, hata kama yeye asingekuwa mwanzishi."[55] Mwanzishi hakujisikia kuwa yeye ni kiungo cha lazima; kwa kweli, kila kitu kingekuja kutoka kwa Mungu, Akitaka wokovu wa watu wote.

[53] Salvatorianer~ Chronik, vol. 3 (1919), no. 2, 2~12

[54] APS I, 85

# 3. Katika Mwanga Wa Utume Wake

Padre Jordan anamalizia ripoti ya safari yake na: Nun ging's ans werk, "na sasa kazi inaanza."[56] Tukio la Lebanon ni chanzo cha uzoefu ulioleta badiliko. Pale Mwanzilishi hakuwa na hali ya kuona mbele, hakuwa mtazamaji, bali alikuwa msikilizaji. Kwa kweli, hakuona chochote, alikuwa akisikiliza, na alichosikia alikifafanua katika maisha yake yote. Ingawa hakuwa na picha kamili ya nini angefanya katika miaka ijayo, safari hii imekuwa kitovu cha maisha yake ya utume ya baadaye. Tangu sasa nakuendelea, angejisumbua juu ya wokovu wa watu tu.Anawatafuta wasaidizi wanaopenda kuanza jumuiya ya kitume. Katika mtazamo huu wa kinabii, aliona hitaji la kidini ulimwenguni ambalo halijasikika na maneno ya Mt.Yohane juu ya uzima wa milele yaliyomfanya awe makini kwamba kila mtu ana tamaa ya ndani kabisa ya kumjua Mungu. Mpango maalum wa kwanza wa Shirika funzishi la kitume aliupeleka kwa maaskofu wote wa Italia mwanzoni mwa 1881,ukianza na maneno yafuatayo: "Ni wajibu wa Shirika kujibu madai ya Bwana wetu Yesu Kristo aliyoyaeleza kwa Baba yake wa milele kabla ya mateso yake: 'Kwamba watu wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.'"[57] Katika Katiba ya 1884, kama utangulizi wa sheria za jumla padre Jordan anaandika ungamo la imani la binafsi kabisa: Huruma na hekima ya muumbaji aliyetaka kulileta Shirika hili katika uhai atalitunza pia na kulifanya likue.[58] Wakati wapinzani wake wakidhani Shirika litaanguka na wengi wa watoto wake walikuwa wakiacha,yeye alinyamaza kimya. Aliwaambia watoto wake waliokata tamaa: Shirika letu



55 APS G 14, no. 19

56 Reise nach Africa und Asien im Jahre 1880, p.35; APS RB-G.5.2

57 DSS XI,651

58 DSS I, 35

limeitwa kwa mambo makubwa na Mungu.Litakua na kuenea duniani kote. Kama nisingejua hilo nisingalisema.[59]

Msaada wa Mungu katika ukweli huu wa kinabii daima umeshutumiwa. Mgeni, wa kwanza Fr.Raimondo Bianchi O.P aliandika kwamba Shirika la kidini la Roma ambalo Baba Jordan alimhakikishia kulianzisha, lingekuwa katika misingi ya uvuvio wa Roho Mtakatifu.[60]

Wakati wa kampeni ya nguvu dhidi ya Padre Jordan katika uchapishaji 1906, walimsuta: "Anafikiri kuwa atapata msaada wa Mungu Roho Mtakatifu bila kupingwa katika jitihada zake."[61]

Akijua kabisa juu ya utume wake, angeweza kuweka wajibu wa kimaadili kwa wafuasi wake ili waukubali mtazamo wake: *Muwe na uhakika kwamba kama msiposhikamana na roho ya Mwanzilishi mtazama chini.* [62] Kwa herufi kubwa zisizo za kawaida, anaandika katika kalenda yake: *Maongozi ya Mungu yameniumba.*[63]



Mnamo 1885, mwaka wa majaribu na mateso kwa Shirika, wakati utengano na masista ulipokaribia, aliandika: *Mimi ni baba wa familia, ninayewatunza watoto wote na ninaweza kuwapa kila kitu. Inatia uchungu kuona kuwa watoto, hata hivyo, wanaomba msaada toka sehemu nyingine.Nimewapa nchi yenye rutuba.Kwa nini mnakwenda kuwauliza wengine namna ambavyo mngelilima na bila kuja kwangu,Bwana? "Nitalionesha Kanisa kuwa kazi ni yangu"anasema Mwenyezi.*[64] Na zaidi, anaandika:

---

59 Letter of Fr. Konrad Hansknecht, 14.05.1936- APS. N, 3.12.37

60 DSS XXI, 269, Letter of 10.03.1882, Fr.Pancratius Pfeiffer, P. Jordan…,114

61 Fr. Pancratius Pfeiffer, P.Jordan…,336

62 Chap. 02.12.1898, DSS XXIII,247

63 D I / 185

64 D I / 166

*Tenda,ongea na kujiongoza mwenyewe kama ungekuwa malaika aliyeletwa na Mungu, anayeongea na watu si kingine zaidi ya wajibu wake aliopewa na Mungu. Kuna maana gani kitu chochote cha kidunia, mimi ni malaika wa mungu aliye juu kabisa,aliyenipeleka mimi kuhubiri kwenu maneno yote ya uzima wa milele. Yeye ambaye ndiye, aliyekuwa na atakayekuja amenituma kwenu kuwatangazia mapenzi Yake.Mfalme wa mbingu na dunia amenituma. Mimi ni mtumishi wa Aliye juu kabisa wa Mungu anayeishi milele!*[65]

Asubuhi hii inatukumbusha maneno ya maana sana ya Dag Hammarskjord aliyosema wazi 1961: “Sijui nani- au nini- swali liliulizwa. Sijui lini liliulizwa. Sikumbuki kama limejibiwa. Lakini, mara moja nimesema *ndiyo* kwa mmojawapo,au kwa kitu Fulani.Tangu hapo, najua kwa uhakika kuwa maisha yana maana na kwamba maisha yangu,kwa kujitoa yana lengo.”[66] Padre Jordan kamwe hakuweza kusoma mapenzi ya Mungu kama kitabu kilichowazi. Walipomkaripia baadaye kuwa hakueleweka hapo mwanzoni, alijibu kwa mshangao na kwa urahisi: *Sijapokea mikononi mwangu utaratibu kamili ulioandikwa wa Shirika kutoka kwa Bwana, Mwema.*[67]

Uhakika wa utume na mashaka katika utekelezaji havinyamazishani. Msaada wa Mungu daima upo,lakini mara nyingi ni vigumu kuutambua kama mtu hawezi kwenda mwenyewe. Kwa Padre Jordan, ilikuwa ni vigumu sana kuamua aanzishe Shirika wapi. Alipokuwa anaadhimisha Misa kwenye kaburi la Mt. Petro Kanisius wakati wa sikukuu ya Kanisius Februari, ghafla aliona kila kitu wazi kabisa. Roma, katikati ya Ukristo na sehemu



[65] D I / 181

[66] Merkstenen, Bruges – Utrecht, 1968, 200

[67] Fr.Pancratius Pfeiffer, Salvatorianer- Chronik, vol. 2 (1920), no. 3, 62

iliyopendelewa ya utaalamu wa Kikristo itakuwa ni kitovu cha Shirika.[68]

Haipo wazi sana kwamba uvuvio unaweza kusemwa kuwa una asili ya Kimungu. Chaguo la Roma limekubaliana na mawazo yake kumbakumba, lakini kiutendaji, halikuwa chaguo zuri.Usumbufu uliokuwa unaendelea na Curia ya Roma ungeweza kuepukwa. Kuna mashirika makubwa mengi ya kitawa yaliyoanzishwa Roma! Nini zaidi,Roma, na mabwawa yake,hapakuwa pazuri kwa afya. Kati ya 1893 na 1902, vijana wa kiume 14 na masista 17 walifariki katika mashirika mawili ya Baba Jordan.

Walilipa bili kubwa kupatunza Roma kama moyo na kiini cha Shirika.Kwa jambo hilo mwanzishi anasema yafuatayo: *Kwa kweli baadhi ya mambo Roma yalikuwa ni hasara au si mazuri mf.hali ya hewa, n.k.Kama tukiangalia hilo tungeweza kuuliza:Kwa nini wote wenye hekima,wenye utaalamu na kuangaziwa walichagua Roma kama kiini cha Kanisa Takatifu ambapo kila mmoja anakuja?Kwanini Mungu hakuchagua sehemu nzuri zaidi? Tunaona kwamba Papa mkuu Leo XIII, licha ya Roma kutokuwa na hali nzuri, analeta hapa vyuo vyote vya Teolojia toka sehemu nyingine za dunia. Unaweza kuona kwamba sadaka kubwa nzuri zinaunganishwa na uamuzi huu. Lakini Leo wa XIII anaangalia kwa mbali. Hapa wazo la msingi ni kutunza kiini cha Shirika kuwa Roma. Mara tu tukiacha wazo hilo, Shirika litaanza kuharibika polepole. Limeanzishwa kwa ulimwengu wote, na mara tutakapolitoa kutoka Roma lingeharibiwa na tabia za utaifa. Lingesimama au kuanguka na fanaka za taifa moja.*[69]



Mwanzishi aliamini kuwa ameanzisha Shirika ndani ya utume wa Ki-mungu.Katika Sheria ya 1884, ameandika kama utangulizi wa Sheria za jumla, Huku kukiri imani

[68] Fr. Otto Hopfenmuller, Die kath. Lehrgesellschaft, 1888, 18 na katika DSS VI, 140

[69] Chap. 02.12.1898 DSS XXIII, 248-249

binafsi:*Huruma na hekima ya Muumbaji aliyetaka kulileta Shirika hili katika uhai pia atalitunza na kulifanya likue.*[70] Namna hali hiyo ilivyompa furaha yabidi kusoma katika barua aliyomwandikia Padre Bonaventura Luthen 1884:*Upendeleo usio wa kawaida wa Mungu kwa Shirika ni mkubwa mno,kiasi kwamba karibu nitokwe na machozi.Ningependa kuanguka chini na kumkumbatia Mwokozi kwasababu ya upendo wake mkuu aliouonesha na anaoendelea kuonesha kwangu, nisiyestahili.*[71]

Mwanzishi wetu kwakweli alikuwa ni mtu aliyejazwa na Mungu.Kwake yeye, Mungu ni kama hewa aliyopumua, ‘Mwingine’aliyeongea na kumhitaji,kwake yeye daima aliyejaribu kumjibu:kwa upole, kuabudu, kutumikia. Alijisikia salama katika kukumbatiwa na Mungu kwa ulinzi.

Kwa njia ya hali hii ya uaminifu wa maisha, Padre Jordan alikuwa wazi kwa utume wa Mungu uliokuwa wazi kwa njia ya mahitaji ya watu. Karibu watakatifu wote na hasa waanzishi wa mashirika ya kitawa walikuwa wana ufunuo na mitazamo ya Ki-Mungu. Hakuna mashaka kuwa Mungu anaongea kwa siri na rafiki Zake na kwamba anawaongoza aliowachagua kwa wajibu huu.



Katika historia ya Kanisa, imekuwa hivyo daima kwamba mageuzi ya kweli ya kidini hayakuanza katika chuo au vikundi. Kwenye asili, kuna mtu mpole mwenye busara ambaye, kwa njia ya uvuvio wake aminifu, ameweza kutafuta suluhisho kwa mahitaji ya kidini ya Kanisa.Tufikiri juu ya Charles de Foucauld,au Mama Teresa. Njia yao ya kiinjili ya maisha imefungua njia mpya za uponyaji na mageuzi. Na kwa mshangao, hawakutafuta mahitaji ya Kanisa, haya yamekuja kwao. Kuishi kwa upole kiinjili, wamewapa mwanga wengine na kuwalazimisha kufanya ndoto zao kuwa kweli.

[70] DSS I,35

[71] DSS X, no. 180, 15.08.1884, 130

# 4. Fikra juu ya tukio la Lebanon

Mwanzilishi daima anazungumzia juu ya ukweli wa ndani alioupata. Inaonekana kwamba, katika nafasi fulani, alitambua juu ya kukutana uso kwa uso na Mungu, wazo hilo lingemaanisha chochote kwake. Ukweli huu ulidumu katika maisha yake na umemuongoza katika matendo yake yote. Kiini cha ukweli wa furaha hiyo ni vigumu kuelezea.Katika maisha yake ya kiroho, alijiachia kuongozwa na kile alichojihisi au kukifikiria kuwa amejisikia zaidi kuliko mawazo yaliyoletwa na wengine. Vilevile anazungumzia mara nyingi juu ya kutoweza kuelezea au kufafanua uzoefu wake: ”Siwezi kuuweka wazi”, “Sijui namna ya kuusema.” Ni wazi, uzoefu huu wa kiroho unahusika zaidi na hisia kuliko na akili. Uzoefu wa vionjo ni vigumu kuueleza. Ghafla, muda ulipoonekana kuwa ni tayari, anaona baadhi ya vitu katika mwanga mpya, anapata ufahamu mpya wa mambo ambayo hayaunganishwi na fikira au hoja. Aina hii ya “Mwangaza”imemtia nguvu ya kujitoa, umempa uwezo mkubwa katika utu wake. Hivyo lazima tutambue ya kwamba uzoefu wa Lebanon uliomsukuma kwa nguvu kujitoa hauwezi kuwa “bure”, kinyume chake, umemaanisha kipindi cha mabadiliko kwake. Tangu wakati huo…ameanza kufanya kazi”[72]



Uzoefu wa fumbo hilo, au vyovyote utakavyopenda kuuita, haukuwa uzoefu wa starehe; analazimika kujaribu kuuweka katika matendo ukweli aliouona. Bila shaka uzoefu wa kimafumbo unaweza kutanguliwa na hatua fulani za matayarisho. Kwa uhakika hakuna mgongano kati ya maelezo ya tukio kiroho na kisayansi. Kamwe hatutakuwa na haki ya kutaka kwamba hata wasio wanachama wakubali tamko hilo.

72 Fr.Jordan,Reise nach Africa und Asien im Jahre 1880, 35

Uzoefu wa fumbo ni wa “ghafla” na wa muda mfupi, ni wakati wa kupata mwanga vizuri. Lakini tabia ya mpito ya uzoefu kama huo haubadili ukweli wa ufahamu wa kina au nguvu ya matokeo kuleta badiliko halisi katika njia yake ya maisha.

Uzoefu wa mwisho wa Mwanzilishi ulikuwa: huu kweli ni mwanzo wa uzima wa milele, na kwamba uzima wa milele umeshaanza katika ulimwengu huu, wakati huu. Mungu anajifanya mwenyewe ajulikane. Tumeshtushwa na ukweli kwamba Mwanzilishi,ijapokuwa uchaguzi wake kwa kujua wa “societas apostolica” umemfanya mwenyewe aangaziwe ghafla na sheria ya kutafakari kwa kina mashirika alipokuwa akiandika sheria na katiba. Angalipenda maisha katika nyumba za wanafunzi yawe tafakari ya maisha ya kutanabahi katika konventi. Ndiyo maana alianzisha kitubio na sala katika mtindo wa kwaya hata kama sehemu nyingi ilikuwa ni vigumu kutekeleza kwenye jumuiya kutokana na kazi nyingi mno za kitume. Kwa namna fulani, alitaka maisha ya jumuiya katika konventi, zaidi kadiri ya uwezekano,yawe tafakari ya maisha ya konventi ya kutanabahi. Alifurahi kwamba mkaguzi wa kitume alikuwa Mkarmeli.

Bila shaka,kama mwanzishi wetu angesimama Lebanoni sasa,pengine angekuwa na uzoefu mwingine.Pengine angeona ulimwengu ambao Kristo anasulubiwa upya katika watu wengi wasio na hatia.Badala ya neno “ukombozi” angesikia neno “kuwa huru”, kuwa huru toka uchumi,mila na desturi, na ukandamizaji wa kiroho. Hali yetu ya kiroho ingekuwa moja na macho yaliyofunguka,makini kwa alama za wakati wetu. Lakini pia angesema na maneno ya uzima wa milele na elimu ya ukombozi, kwamba Kristo bado anatenda kazi katika ulimwengu huu.

# 5. Kuzingirwa na nguvu za giza

Karibu Waanzilishi wote na Watakatifu walikuwa na ufunuo na maono ya ki-Mungu.Bila shaka Mungu anazungumza kwa siri na Rafiki zake na anawaongoza hao aliowachagua kwa utume huo. Lakini pia walipitia mateso makali dhidi ya shetani na nguvu za uovu.Mwanzishi wetu pia aliwashirikisha waamini wa wakati wake uzoefu wake na fumbo la uovu na maoni yake juu ya motoni na shetani.

Mwaka 1887,Padre Bonaventura Luthen aliandika kwenye “Der Missionar” juu ya kutoa pepo katika nyumba Mama.[73] Matoleo haya yamekuja kama ganda la bomu. Magazeti mengi yamefuata na kutoa kama vipeperushi.

Padre Bonaventura Luthen anaandika katika utangulizi kwamba alitaka kutoa ukweli kwa utukufu wa juu kabisa wa Mungu: “Ilikuwa ukubwa wa shetani Shirika lililazimika kupigania,hivyo ilikuwa ni mapenzi ya Mungu.” Anajisikia kulazimika kwa ndani kufunua kweli hizi kwa watu ili kuonyesha kushindwa kwa shetani.anaandika wazi kwamba haelezi maoni yake kuhusu kweli hizi; anaacha uamuzi kwa uongozi wa Kanisa.Kwake, matunda tu yanaonesha. Kutoa pepo, anasema, kumetokana na msimamo wa kiroho wa jumuiya yote na Bruda alipata ruhusa na wakubwa ya kuwa Padre. Ni hakika kuwa padre Pancratius Pfeiffer hakuongelea juu ya kweli hizi, wala katika historia fupi ya mwanzo ya mwanzishi wala katika ushuhuda wake kwa harakati za kumtangaza mwenyeheri.



[73] Fr.Bonaventura Luthen, “Eine Teufelsbeschworung” in Der Missionar,1887: Jan.30,Feb.13,March 13 na 17,Apri 10 na 24. Na 1892, kila kitu kiliandikwa mara moja zaidi kama kipeperushi. Angalia pia Fr.A.Schneble katika Historica SDS, no.437,440-445, kutoka Sept.25 hadi Oct.22,1982.

Sijui kama nalazimika kufunua kweli hizi hapa au kuziacha kimya. Maisha ya kiroho na mapambano dhidi ya maovu huenda pamoja. Tunaweza kuona kwamba nguvu za uovu zinafanya kazi kila mahali.Kuamini ni kuwa na tumaini haswa kwa Fulani.Tunavunja nguvu za uovu kwa kutoziamini.Baadaye,Mwanzilishi aliandika kwa Bruda huyu: Utii unavunja shingo yake[74], usimtumainishe kwa lolote.[75]

Ni wazi kabisa kwamba pambano hili la moja kwa moja na nguvu za giza, au vyovyote unavyoweza kuziita, zilikuwa zina mtazamo usiofutika kwa Mwanzilishi kama kushindwa kwa shetani na kwamba umemfanya hata zaidi kuwa na matumaini katika msalaba wa Bwana.Padre Jordan anaandika kwa hiari bila kutumia nguvu katika sura moja,kuhusu namna anavyomwona shetani: *Mshindani wetu,adui mwovu anachukua vitu vizuri sana.Inaonekana kwangu,kadiri kitu kinavyokuwa kitakatifu ndivyo anavyozidi kupigana dhidi yake.Yeye ni mpinzani wa Mungu na anachukia ndani yetu sisi binadamu kila kitu anachogundua kuwa kimetoka kwa Mungu. Akijua kuwa mmoja amejitoa kwa Mungu, anamtia woga wa ajabu na chuki kubwa, na anampinga mtu huyo kadiri anavyoweza akimtia hali ya hasira na kisasi. Kadiri anavyokufuru kitu kitakatifu zaidi, ndivyo furaha yake inavyozidi.*[76] *Mwanzishi aliamini kwamba hasa motoni-nini kisichotumia dhidi ya Shirika ambalo limetangaza vita ya wazi dhidi yake,na ambalo linapanga kukamata roho ambazo limeziona kuwa zimeshinda.Kwa hiyo,moto utakasirika na kufanya kila uwezacho kuwaharibu wanachama na Shirika lote.Shetani anapigana hasa na sehemu mpya zinazoanzishwa.Ndio maana ni muhimu kwenu kusali daima.Sala ndiyo silaha yenye nguvu zaidi.*[77]



74 DSS X, no.277, 17.04.1895
75 DSS,X, no.284, 07.09.1895
76 Chap.18.12.1896,DSS XXIII, 93
77 Chap.15.02.1901,DSS XXIII, 400

Kwa kweli, Kanisa hukaa pembeni wakati shetani anapozungumziwa na kukaa mbali kutoka hali ya kushikwa na kutoa pepo. Hata hivyo tunafikiri kwamba, kama tukitaka kuzungumza juu ya maisha ya kiroho ya Mwanzilishi wetu, hatuwezi kuacha kusema juu ya pambano lake dhidi ya mwovu.Baba Jordan alianzisha Shirika akijua kabisa kama kikundi cha watu wenye akili wajiingize katika mapambano dhidi ya shetani.Kwa nguvu zao zote,watatetea imani takatifu dhidi ya maadui wa Mama yetu Kanisa na dhidi ya nguvu za kishetani.[78] Ndio maana analiweka Shirika chini ya ulinzi wa Mama yetu mkingiwa dhambi ya asili,aliyemponda nyoka,na ndio maana ameomba Mt.Michael awe msimamizi.Miaka ya mwanzo wakati wa kuanzisha,Padre Jordan alivutiwa sana na Mt.Ignasius na mbinu zake za kupigana na uovu kama jitihada. Maneno"Askari wa Kristo", "Pambano dhidi ya nyoka"daima yalikuwa mdomoni mwake: Tusali leo (Desemba 8) kwa upendeleo mkubwa wa Maria, aliyemkanyaka nyoka ili atusaidie kumshinda mwovu ambaye anatawala kwa vikubwa roho siku hizi. Chini ya mwanga wa Mwokozi wa ulimwengu ni lazima tupigane na baba wa upinzani na adui wa malaika.[79]



Tungependa kutaja hapa tukio linalohusiana na mapambano dhidi ya shetani.

Januari 5, 1887, Bruda Felix Bucher akifanya kazi jikoni katika nyumba mama Roma, alionyesha alama wazi za kupagawa. Maoni ya dactari yalikuwa kwamba hakuna kifafa wala ugonjwa mwingine wa kawaida. Bruda hakuweza kutawala miguu yake zaidi. Alivutwa juu hewani na kutupwa chini kwenye ardhi. Alikunja miguu yake au mikono yake kwa haraka hewani huwezi kuamini. Alitukana na kutoa sauti ya mnyama kama punda, au kama

[78] Sheria ya1882,DSS I, 22
[79] DSS X, no. 295, 08.12.1895

jogoo.Dalili hizi zilikuwa sababu ya kutosha ya kuomba kutoa pepo Januari 16. Ilimalizika saa moja na nusu.Wiki nne baadaye, kupagawa kulianza tena, kwa nguvu zaidi kuliko mwanzo.Utoaji wa pepo uliofuata umechukua siku tatu,pamoja na mapumziko.Wakati wa kupunga pepo,fujo zaidi ilikwenda kwa mpunga pepo, Padre Jordan, ambaye,pamoja na Padre Bonaventura Luthen na Padre Thomas Weigang walijaribu kumtoa pepo kwa jina la Kanisa. Mara nyingi, Bruda alitupa kitabu cha sala toka mikono ya Mwanzilishi. Tena na tena, alitupa miwani chini na kujaribu kuwafanya waliopo wacheke kwa kukunjakunja uso. Alimpa Padre Jordan jina la “Baba wa wachawi.” “Unaweza kusali na kufanya viinimacho, unavyoweza,” alisema kwa dharau, hakuna yeyote aliyefanya vizuri kama unavyofanya. Jehanam kote kumejaa uovu. Unawaloga watoto wako wote.” Hakujua ukweli kwamba jumuiya ilikusanyika mezani wakati huduma ile ilifanyika kwenye kikanisa kidogo. Alimwambia Mwanzilishi: “Nenda kawaambie watoto wako wanyamaze.”Mara moja alifungua mlango wa mezani, akisema kwa nguvu:”mimi ni Luciferi!” Njiani kutoka mezani kwenda kanisani, kulikuwa na sanamu ya Mama yetu mkingiwa dhambi ya asili. Mwanzilishi alimwomba Bruda apige magoti mbele ya sanamu, alifanya hivyo bila kupinga,na aliposimama tena,alisema kwa dharau: “Kama nikifukuzwa leo,itakuwa ni kosa lake,pale.”Hakuelewa maji ya Lourdes. Alipoyanywa kiasi bila kuelewa yalisababisha hasira kubwa kwake. Wakati Lucifer, kama alivyojiita mwenyewe,alipofika chumbani kwake na kuona ubao wenye jina la Padre Jordan,aliugeuza ili asione jina tena. Baadaye, alisafisha vidole vyake kana kwamba alichafuka kwa kuugusa ule ubao.

Baada ya Februari 2, hakukuwa na mashambulizi tena. Baada ya kupona Bruda aliomba kuwa Padre.Mnamo Sept. 19,1891, alipata upadrisho.Alikuwa akifanya kazi kwa miaka 40 kama mmisionari kati ya “Redskins”eneo la Wahindi huko Oregon (Marekani Kaskazini)

Alifanya kazi katika Makanisa mawili umbali wa kilometa 70 toka moja hadi lingine.Aliishi pale,maskini kati ya maskini waliomheshimu kama mtakatifu.Alifariki St.Nazianz (USA) April 13,1938. Mkubwa wake wa Provinsi alishuhudia kuwa alikuwa akiishi kama mtakatifu.Ingawa, alipagawa kipindi cha nyuma katika maisha yake.Mwanzilishi alikuwa akiwasiliana naye daima,tunajua juu ya barua kumi na tano.[80] Alimshauri:*Akae karibu na kuwasiliana na Padre wake wa kiroho, sababu roho ya kishetani ingefanya chochote ili ikukamate katika nyavu zake.Usimwamini; anaweza kuja katika mtindo wa mwanga.Utii utavunja shingo yake.Kuvumilia njiani inapinga.Hivyo, umuombe Maria Mama yetu wa Mbiguni.*[81]

Miezi michache baadaye, Mwanzilishi aliandika:*Uzoefu wangu ni kwamba, adui mbaya anapotaka kumshika mmoja,anamweka katika ugomvi na mkubwa wake na anajaribu kuamsha tabia ya kutomwamini.Unijibu haraka unafanyaje.*[82] Baadaye Mwanzilishi anaandika tena:*Usikate tamaa kwa mshawishi, bali simama kwa mapambano,kama ulivyofanya moramoja…vumilia;tunza kile ulichonacho kwani hujui hali ya mshawishi. Uyashike maneno ya mpendwa baba yako wa kiroho.*[83]



Vishawishi na mashambulizi yaliyorudiarudia ya mwovu yalikuwa daima ya kweli kwa Padre Jordani. Katika Kalenda yake, anaongelea juu ya hili: *Shetani anafanya kazi kwa kutumia mambo madogomadogo kusababisha tupoteze wito wetu.*[84]

Kwake yeye, jibu la kwanza ni daima kutumainia maongozi ya Mungu.*Umdharau shetani.Uweke matumaini*

[80] DSS X, Idadi ya waliopokea Barua XXX

[81] DSS X, no.277

[82] DSS X, no.284

[83] DSS X, no. 327

[84] D II / 37


*kamili kwa Mungu.Usife Moyo!*[85] *Shetani anatuogopa, kama tusipomuogopa.*[86] Katika barua yake wakati wa Jubilei ya miaka 25 ya Shirika, anaandika: *Mnajua namna adui alivyona hasira kali.*[87]

Padre Jordan aliishi kwa mtazamo wa Teologia tofauti kabisa na sura ya shetani tofauti kabisa na tujuavyo sasa. Lakini jibu alilotoa kuhusu siri ya uovu bado lina thamani: *Uwe mbali nami kwa utukufu isipokuwa katika msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo.Ulimwengu umesulibiwa kwangu na mimi kwa ulimwengu.*[88]

Mwanzishi aliita uovu wa dunia kwa jina lake na alipambana nao kwa nguvu ya msalaba wa Bwana. (Waef.6:11-16.)[89]



85 D IV / 2
86 D IV / 28
87 DSS X, no. 854
88 Gal.6:14 D I / 71, D I / 179, D IV / 18
89 Eph, 6:11-16



*Wanachama wa kwanza 1882: (toka kushoto kwenda kulia)*
*Friedrich von Leonhardi,*
*Padre Jordan, Bernhard Luthen, Mgr. von Essen.*

# III

# Maisha yake ya sala

## 1. Fumbo la sala

Wakati wa mkutano, Padre Jordan alisema: *Hatuwezi kuishi miito yetu bila sala zaidi. Ikiwa mmoja ataniambia namna anavyosali na mara ngapi, naweza kusema yeye ni nani.*[90] Kipimo hicho kinaweza kutumiwa na Mwanzilishi wetu. Hakuna njia bora zaidi ya kumjua zaidi ya kutafuta namna gani na mara ngapi alisali.

Ni katika sala hasa, mtu yule ni yeye kweli. Ni peke yake kabisa na dhaminri yake pamoja na Mungu.Tunaweza kunyanyua kipande kidogo tu cha mfuniko wa mkutano huu, kwa sababu tunazungumzia juu ya ulimwengu ambao kwa kweli si wetu tena,bali wa Mungu.Tunashuhudia,kwa kuona jinsi binadamu alivyo mnyonge na nguvu za Mungu zinavyokutana katika uhusiano.

90 Chap.29.11.1895, DSS XXIII, 47

## 2. Mitindo muhimu ya sala

Kama tukitaka kusema wazi juu ya maisha ya sala ya Padre Jordan, inafaa kuonyesha muhtasari juu ya mitindo ya sala.Kwa ufupi sala inaweza kugawanyika katika njia ya utakaso,wakati toba na kujitesa huchukua nafasi muhimu,njia ya wongofu ina tabia ya kuziishi fadhila na mwisho njia ya muungano ambapo Mungu anachukua nafasi kubwa kwa nguvu ya roho.

Katika kupanda kwetu kwa Mungu, tunazungumzia juu ya kujinyima vitu na mambo ya kufurahisha hata yakiwa halali ili kuwa mwema na kuepuka mabaya, na kumshiriki Mungu na kutafakari sana habari za Mungu. Kwetu, hali hiyo ina maana ya kujitahidi kwa ukamilifu kwa mkazo wa pekee juu ya matendo ya binadamu, hasa pambano dhidi ya maovu na kufuata njia ya utakatifu kwa kujua. Inaonekana kwamba sisi wenyewe tunafanya mazoezi ya uchaji. Alama ya tabia ya kumshiriki Mungu na kutafakari zaidi habari zake ni uzoefu wa moja kwa moja wa uwepo wa Mungu, ndani ya nafsi zetu, ambapo picha zote na akili ya kufikiri huishia.



Tabia ya kwanza ya uzoefu wa kumshiriki Mungu ni hali inayokuja bila kujilazimisha. Mungu mwenyewe hujionyesha moja kwa moja, bila kuwa na kiunganishi. Mtu anayemshiriki Mungu anamhisi Mungu, anajisikia kuchukuliwa naye moja kwa moja. Kwa kawaida,mmoja wa waamini anakuja kwenye uhusiano na Mungu wakati wa sala,kusoma neno la Mungu kwa njia ya mwamini mwenzake. Kwa namna nyingine,wakati wa hali ya kumshiriki Mungu hakuna kiunganishi kinachohitajika na hali hiyo inaweza kumpata mtu wakati asipotegemea. Ndio maana tabia ya pili ya uzoefu wa kumshiriki Mungu ni utulivu. Mungu mwenyewe anapanga mwanzo na mwisho wa uzoefu huo. Hauwezi kuitwa, kwenye utaratibu, mmoja

hawezi kuupangia muda, na mara nyingi inamchukua mtu akiwa amezidiwa na shughuli fulani. Hivyo mawasiliano haya hayawezi kuelezwa, hayaelezeki na kwa urahisi hakuna maneno ya kuelezea.

Matunda ya kwanza ya kujisikia kuwa karibu na Mungu kwa karibu ni: amani, furaha na kujiamini anakojisikia bila kutumia nguvu nyingi.

Inajulikana kwamba mtu anayemshiriki Mungu haimbi sifa zake mwenyewe juu ya uzoefu wake wa kiroho na Mungu.Kama akiruhusu chochote kijulikane, ni kwa ujumla katika kalenda yake au katika mazungumzo na rafiki wa karibu kabisa.

Hali ya uzoefu wa kumshiriki Mungu kamwe hakuna uhuru wa kujitoa.Hupewa wale wenye nia ya kukubali kwa ajili ya maendelea ya jumuiya.



Tusitilie mkazo mno tofauti kati ya hali ya kujinyima anasa na hali ya kumshiriki Mungu.Maisha ya Kikristo ni muungano mzuri wa kazi na tafakari au kutanabahi. Zawadi ya kumshiriki Mungu ni za lazima. Nadhani ni watu wachache sana ambao hawajapata uzoefu wa kumshiriki Mungu katika maisha yao.”Watu wema wote wanao uzefu huo.” Anasema Ruusbroec,”lakini wanawezaje kubaki wamejificha maisha yao yote.”[91]

Lakini uzoefu huo haumfanyi mtu awe wa kimafumbo. Zawadi za kimafumbo za kumshiriki Mungu si za upendeleo ambazo hutolewa kwa watu waliochaguliwa,zinaweza kushinda akili iliyowazi, na hutokea mara nyingi zaidi kwa watu wa kawaida kuliko tunavyoweza kudhani.Inaweza kuwa ni faraja kwa baadhi ya watu kwamba hatulazimiki

[91] Die gheestelike brulocht, Book I,Part I,p.43

kuwa mfano wa ukamilifu wa kisaikologia au tabia ya muungano ya kuwa mshiriki wa Mungu kwa vikubwa. Tunaweza kusema kwa urahisi kwamba maisha ya kumshiriki Mungu yanatangulia zaidi kuliko maisha ya fadhila; lakini ni kweli pia kwamba Mungu anaweza kutoa vipaji vyake kwa yeyote na wakati anaotaka.

## 3. Padre Jordan, mtu wa sala

Padre Jordan aliandika karibu na chombo cha maji ya baraka kwenye mlango wa chumba chake: *Sala ni nguvu kubwa sana katika ulimwengu.*[92]

Maisha yote ya Padre Jordan yamejengwa kwenye ukweli wa maneno hayo. Maisha yake ya sala ni ufunguo unaotupa sisi nafasi kwa maisha yake ya binafsi na kutupatia pia tamko la mwisho la jinsi alivyoshinda mateso yake yote, kukatishwa tamaa na majaribu mbalimbali.



Katika historia fupi ya Mwanzilishi, Padre Pancratius Pfeiffer anaweka kama ifuatavyo: Kama Padre Jordan hakushindwa chini ya mzigo mkubwa alioubeba na kama kazi aliyoitiwa katika maisha haikufikia mwisho mbaya, hatuwezi kutoa maelezo mazuri zaidi kuliko kusema kwamba sala zake zilimsaidia katika kazi zake. Ndiyo maana mara nyingi alitumia maneno ya Maandiko Matakatifu: "*Ni huruma ya Bwana tu iliyotuokoa kutoka uharibifu.*"[93] Alikuwa mtu wa sala. Kwa kweli, alikuwa akisali daima. Alitumia kila muda kusali. Sala zilimsindikiza katika kila kazi yake, mwenendo wake wote, maneno na matendo yake yalielekea kwenye roho yake ya sala. Alikuwa na woga kuwaruhusu wengine washuhudie mawasiliano yake ya ndani na Mungu.Hata hivyo,hii ilijitokeza ukimwangalia,katika uso

[92] Fr. Cyrillus Braschke,AS II, no. 30
[93] Fr. Pancratius Pfeiffer, P.Jordan, 388

wake na jinsi alivyopumua ilionesha wazi.Alipokuwa peke yake bustanini,alipenda kusali rosali ambayo alikuwa akiificha ndani ya kanzu au kwenye mikono ya kanzu yake.Alipokuwa Roma alikuwa anachukua mapumziko mafupi kila siku.Alikwenda karibu na Kanisa la Mt.Petro.Kwanza alikwenda kwenye kikanisa cha Sakramenti Takatifu,halafu kwenye Altare ya Mama yetu wa Colonna na mwisho kwenye kaburi la Mt.Petro.Alisali kwa utulivu sana na kwa uangalifu kiasi kwamba wala mazingira wala jirani yake asingemtambua.Walioshuhudia sala hizo wasingesahau kamwe.Siku moja, kiranja wa Seminari ndogo Roma alimwona Padre Jordan kwenye kaburi la Mt.Petro,akiwa amemezwa katika sala.Aliwaita waliomfuata,akawaonyesha Padre aliyekuwa akisali na kusema: “Angalia namna mtakatifu anavyosali.”Si ajabu watu waliomwona pale kila siku walimwita: “Il santo.”

Padre Mbenedictini alisema baadaye kwamba mmoja kati ya wenzake alionyesha kwa Padre Jordan aliyekuwa akisali akisema: “Angalia jinsi anavyosali.”[94]



## 4. Fr. Jordan na Ekaristi

Padre Jordan alitumia muda mwingi kwenye kikanisa kidogo.Ekaristi Takatifu ndio ilikuwa ya muhimu sana katika maisha yake ya kila siku.Waliomwona Padre Jordan akiingia kanisani walielewa kuwa kwa siri alivutwa kwenye Tabernakulo,aliguswa sana. Namna alivyopiga magoti ni hotuba kwa yenyewe. Kwa sababu ya uchaji wake,alitaka masharti yote yaheshimiwe. Alipokuwa mzee, maadhimisho ya Ekaristi na sala za Breviari zilikuwa ni mzigo mzito sababu ya tabia yake. Vyote viwili vimekuwa chanzo cha hofu, mahangaiko na maumivu yaliyosababisha wenzake

[94] Kwa habari hii,angalia Fr. Jozef Lammers, Das Gebetsleben P. Jordans, 49-66

wamwonee huruma.Hiyo ndiyo sababu baada ya miaka hamsini ya kuzaliwa aliadhimisha Misa ya Jumuiya mara chache. Pia alipenda kusali mkesha peke yake chumbani,au pamoja na mwenzake mmoja.

Tunaweza kuona, kwenye kalenda yake,jinsi alivyojisikia wakati wa Komunyo takatifu:*Changamka na ufurahi, roho yenye woga, kwa sababu muumba wa vyote atachukua makao yake pamoja nawe; Mfalme wa kwaya ya mbinguni anakuja kwako;mwenye nguvu, Mungu mweza yote anakuja kwako…. jitumbukize katika bahari ya upendo wa Mungu.*[95]

Hii ni picha ya fumbo la kumshiriki Mungu kwa namna ya pekee. Jitumbukize katika bahari ya upendo wa Mungu.Ekaristi ni nafasi ya mwisho ya kushuka kwa Mwana wa Mungu na ya kupaa kwa watu kwa Mungu.Toka uzoefu wake mwenyewe, mwanzishi angekubali ukweli ambao Thomas wa Kempis aliandika: Neema hii wakati huu ni kubwa mno, kwamba wingi wa uchaji hauimarishi roho tu bali mwili dhaifu pia."[96] Katika mazungumzo kwenye mkutano, alisema: *Mngeacha mstari wa Komunyo…kama Simba atemaye moto.*[97] Tena inashangaza mno kwamba Padre Jordan angehisi kwa namna ya pekee sana uwepo wa Bwana wakati wa Ekaristi? Kwa Padre Jordan, kulikuwa na muungano halisi wa kweli kati ya Ekaristi na maisha yake. Kristo mwenyewe alimfundisha Padre Jordan kuishi na kufanya kazi kwa njia Yake, pamoja Naye na ndani Yake. Faraja aliyoipata wakati wa Ekaristi imechukua sehemu kubwa na muhimu katika uanzishaji wa Shirika.



95 D I / 149-150
96 Kumfuasa Kristo,VI, Chapt.I.,6
97 Chap.27.01.1899, DSS XXIII, 272

# 5. Kuwa mtu wa sala

Padre Jordan hakufikia hatua ya kutovurugwa katika sala ghafla. Kwake pia, ilikuwa inakua taratibu. Hata alipokuwa mvulana mdogo, aliendа kwenye msitu ili aweze kusali huko. Kama askari, alifunga mlango ili asali. Rafiki yake alipomuomba, wakati wa masomo yake ya juu,kwenda kwenye Misa pamoja naye, alijibu: *Sitaweza sababu nahitaji muda huu kusoma*.[98] Tunaweza kuelewa jibu hili vizuri,alipoendelea katika maisha ya sala kwa kweli alisoma kidogo ili aweze kupta muda wa kusali zaidi. Baadaye, alichukua tabia hiyo kama utaratibu wa maisha yake. *Kwanza Ibada halafu sayansi*.[99] Alielewa hili akiwa mwanafunzi wa Teolojia.

*Soma kwa wastani, hasa masomo yale ambayo siyo ya lazima sana:Itakufaidia nini,kama kwa sababu hiyo,ungempenda Mungu hata kwa kupunguza digrii moja katika umilele…Uwe mkubwa mbele ya Mungu na sio mbele ya ulimwengu*![100]



Hapa, anafikia hatua ya sadaka.Anaweka muda kwa Mungu na kwa sala. *Hata mkizidiwa na kazi nyingi,bado tumia muda wa saa moja kwa tafakari kama afya ikiruhusu.*[101] *Mara nyingi amejisikia kuwa saa moja kwa siku haitoshi.Wakati wetu unahitaji wanaume na wanawake wanaosali.Na kuna uzuri gani kwa kazi zetu zote na juhudi zote,mahubiri na maandishi yetu yote,kamaMungu hasaidii.Uwe na uhakika,muda unaotumika katika sala kamwe haupotei bure.Na muda tunaotumia katika sala hautoshi kwa vyovyote.*[102] *Sala zinahitajika zaidi wakati tunapokuwa na shida. Weka walao masaa matatu ya sala kwa*

[98] Barua ya Von Rupplin, 23.01.1925, APS I, 24
[99] Notizen, Archives II, 3
[100] D I / 30-31
[101] D I / 48
[102] Chap. 15.07.1898,DSS XXIII, 232

*siku.*[103] Kwenye Kalenda yak,e anaandika pia: *Muendelee na mazungumzo yenu ya kiroho na Mwokozi. Kaeni kwa upole na unyenyekevu kwenye miguu yake na kusikiliza maneno yake kwa makini.*[104]

*Sala za usiku –ni hazina!* [105] *Mara nyingi peke yako na Mungu; simama mara nyingi peke yako karibu na Tabernakulo,sahau mengine yote.*[106] *Jaribu kufikiri nguvu na faraja unayopata kwa njia ya sala!*[107]

Wakati mmoja anajisikia hali ya kuwa karibu na nguvu ya Mungu sala inakuwa muhimu na hitaji la siri. Tunaona mawazo yaliyorudiwa katika kalenda yake:

Sali –Sali- Sali
*Sali –Sali- Sali!* [108]
Sali –Sali- Sali
Bila kuacha, kwa matumaini makubwa.[109]
Jishindie Mbingu kwa sala!Usiruhusu chochote kikuzuie![110]
Sali –Sali- Sali
*Sali –Sali- Sali-Sali.*[111]



Wakati ule, Padre Jordan alijisikia hitaji kubwa la kujifunza lugha.Hivyo alilazimika kusali usiku.Tunaona wazi katika kalenda yake:*Kadiri utakavyoweza tumia muda wa kusali usiku.Kama afya yako inaruhusu,na muungamishi wako anakuruhusu umuige mpendwa Mwokozi mara nyingi katika*

[103] D I / 85
[104] D I / 65
[105] D I / 68
[106] D II / 92
[107] D II / 30
[108] D II / 28
[109] D IV / 6
[110] D II / 41
[111] D IV / 33

*hili,kwamba utumie muda walao nusu ya usiku peke yako kwa sala.*[112]

Na anafanya marejeo ya binafsi kwa Luka: "*Alikwenda mlimani kusali na alitumia usiku mzima katika sala kwa Mungu"*[113] Anawaonya wenzake: Mumwige Mungu mwalimu wetu ambaye alisali sana na ambaye Maandiko Matakatifu yanasema: "*Alitumia usiku katika sala.*"[114] Padre Jordan alituambia kidogo sana kuhusu sala yake ya usiku. Ameonyesha mara moja kama rejeo, alipowatia moyo wenzake kwenda kusali katika chumba cha maiti cha Mt Brigitta, Piazza Farnese 16,alipoanzisha Shirika: *Salini kwa Mt.Brigitta ambaye mara kadhaa tulienda katika chumba chake ambapo tulikuwa tumezama katika sala wakati wa usiku wa manane.*[115] Mtunza Sakristia, Padre Efrem Bonheim, alikuwa na wajibu wa kufunga mlango wa Kanisa usiku na kufungua tena asubuhi. Padre Jordan aliacha afungiwe na alitoka nje mtunza Sakristia alipokuja kufungua mlango asubuhi. Mwanzishi hapo aliwahi chumbani kwake, ili asionekane na mtu yeyoyte.[116] Alichokihisi Padre Jordan wakati wa sala zake za usiku kwa kweli kitabaki ukurasa usioandikwa katika historia yake fupi.

## 6. Sala inaunda nafasi

Padre Jordan alisali sana kabla sala haijawa sehemu yake ya pili ya maisha kwake. Sala kwanza inamhusu Mungu, lakini inahitaji jibu huru toka kwa mtu.Si mtu anayepanda kwa Mungu. Katika kila sala Mungu anainama kwa kiumbe chake, sababu anataka kukaa katika moyo, kama alivyofanya

[112] D I / 135
[113] Lk.6, 12- D I / 64
[114] Chap. 15.071898, DSS XXIII, 231
[115] Chap. 11.10.1901, DSS XXIII, 457
[116] Barua ya Fr.Engelbert Heilmann 15.12.1935, APS, N,3.1.2.14

na Maria, ili ajiunge na binadamu. Sala ni ufundi ambao tunalazimika kujifunza na kutekeleza.Tunajifunza kusali kwa kusali.Kwa kawaida, mmoja hapendi kusali:Anaweza kujisikia usumbufu fulani,kutovutwa au kutojisikia raha.Anafikiri kuwa anaweza kufanya kazi nyingine ambazo zinaonekana kama muhimu zaidi.Tunasema kwamba tunaipata mbingu kwa sala zetu,lakini sala ya kweli ni kujiweka chini ya mapenzi ya Mungu.Sala ya kweli toka ndani kabisa ya nafsi zetu hutokea mara chache sana!Padre Jordan alijua hilo vizuri sana: *Lakini tafuteni hili [mf.kuwa watakatifu] kwa njia sahihi:Si katika ugo wa kiroho ila kwa njia ya mateso,utii,ufukara,na kuzingatia taratibu za kitawa.Hata kama ungekuwa mbinguni na kuweza kupata miujiza kama huziishi fadhila uko hatarini hata kwa njia bora zaidi.*[117]

Tayari hata pamoja naye, sala imebaki kujitesa kwa daima. *Sali, hata kama ni mzigo au usumbufu kwako na kama zikionekana kuwa hazifai kabisa kwako.*[118] Kwa njia ya sala, zake alijiaminisha hivyo.*Sala zangu haziwezi kuwa bila matunda mradi kama ni sala bora;au nitapewa kile niombacho au nitapata bado neema nyingi.*[119]*Hata akinitupa bado nitamtumainia.*[120]

*Lazima usali zaidi, jishinde zaidi, unaweza kufanya mambo yote; mtumaini yeye kwa nguvu zote.*[121] Mungu anatoa sala kwa mtu anayesali. Anatuangalia sisi kabla sisi hatujamwangalia Yeye. Upendo wetu unaweza kuwa ni jibu la kibinadamu kwa upendo wake wa kwanza.Imani yake thabiti katika nguvu ya sala tu imemtunza mwanzishi katika hali ya uadilifu. *Salini kwa uaminifu,kwa uaminifu zaidi,kwa uaminifu zaidi kabisa na muwe na matumaini,sababu Bwana ni Mwenyezi, na yeyote anayemtumainiYeye kweli hatashindwa*

[117] Chap.20.04.1894, DSS XXIII,23
[118] D IV / 21
[119] D I / 170
[120] D I/ 122
[121] D III / 19

*kamwe!*[122] Kwa njia ya uvumilivu wa upendo, Padre Jordan amejifunza kusali.Nukuu inayofuata inaweza kufafanua sehemu ya juhudi zake za kuweza kusali:

Francis Sali kwa nia

Francis! Francis! Francis!

*O FRANCIS*

*Jitoe walao masaa saba kwa kusali!*
*Uwe makini na usiache! Francis usiyestahili!*
*Masaa saba kwa siku uyatoe kwa sala!*
*Francis usiyedumu katika sala!*
*Yatoe masaa saba kwa sala!*
*Francis uliye mvivu! Uweke masaa saba ya sala kwa siku,na kama hukutekeleza, jipe mwenyewe malipizi makali. Siku ya 25 ya Julai,1888.* [123]

Maneno hayo yalitokea ndani yake bila kuyatazamia.Yaliandikwa moyoni mwake. Anamaanisha nia hiyo kwa uaminifu kiasi kwamba anataka kujiadhibu vikali mwenyewe akifanya uzembe. Anajua vizuri kwamba sala inaweza kumaanisha aina ya mateso kwake. Mwanzishi alisali masaa saba kwa siku? Tunayo makala inayoonyesha alivyojaribu kuyapangia utaratibu masaa hayo saba katika ratiba yake ya kila siku. Lakini alitumia akili ya kawaida kuweka ratiba mbili za sala,kwa kuzingatia siku anazokuwa na kazi nyingi:



122 D III / 2
123 D I / 197-198

*Kwa Mungu* *Pamoja na msaada wa mungu*
*Jiwekee masaa saba ya sala kwa siku*

| **(Ratiba ya kwanza)** | | **(Ratiba ya pili)** |
|---|---|---|
| 6-9 | = 3 | 1 ½ |
| 10 ½ -11 ½ | = 1 | ½ |
| 2 ½ - 3 | = ½ | ½ |
| 5 – 7 | = 2 | 2 |
| 8 ¾ - 9 ½ | = ¾ | 1 |
| | 7 ¼ | 5 ½ [124] |

Kusali wakati wa masaa ya usiku inawezekana kwetu sisi binadamu tu kama Roho ya Mungu mwenyewe inapiga kite pamoja na wale wanaopiga kite.[125] Halafu roho inaweza kushiriki katika njia ya mafumbo ya kubadilishana upendo. Kama Mt. Paulo anavyosema: "Mungu amepeleka roho ya Mwanae kwenye mioyo yetu, tukiita: Abba Baba!"[126] Hivyo sala si hasa kazi ya nguvu zetu, bali ni zawadi ya Mungu. Kwa njia ya mwanga wa ndani na kwa njia ya nguvu ya upendo, mtu anateseka, kwa njia ya maumivu,kwamba yeye mwenyewe si mtakatifu,bali amevunjika na mdhambi. Anatambua kuwa hayupo na Mungu,na anajisikia kukimbia mbali na utakatifu wa Mungu.Wakati huohuo anatambua kuwa anahitaji roho ya Mungu katika hali zote za maisha yake; kwamba anaweza kuishi kwa msaada wa Mungu tu na kwamba hawezi kupata msaada wowote mahali pengine. Kwa njia hii, anavutiwa na utakatifu wa Mungu, licha ya hali yake ya dhambi, kutakaswa kama chuma kwenye moto.




Katika njia zake mwenyewe, Padre Jordan anaeleza uzoefu wake katika sala ifuatayo: "Ee ukubwa usiopimika na uwezo wote wa Mungu, unipe imani thabiti na matumaini

[124] DSS XV.I, 137
[125] Rom.8:26
[126] Gal.4:6

kwa Mungu kama mtu naweza kupata pamoja na kwa njia yako. Ah, natambua kuwa mimi si lolote,, bali kwa njia yako, Bwana, naweza kufanya mambo yote.Ah,naomba uishi ndani yangu, niruhusu nife, na wewe Uishi; chochote kinachozuia kazi yako ndani yangu kife ndani yangu,kama yalivyo mapenzi yako.[127] Tabia zote muhimu za sala zipo juu ya sala: imani, matumaini,upendo,upole, kujishusha na kujitesa.Shukrani kwa tabia hizi za msingi, kila kitu kinakuwa sala katika maisha ya Padre Jordan.Inaweza kusemwa kwake kama kwa Mt. Francis: "Hakuwa mtu wa sala tena,bali alikuwa sala kabisa."



[127] D I / 168



Nyumba mama Roma, Via della Conciliazione 51. 1895

# IV

# Kukua katika maisha ya sala

## 1. Mtu anakuwa kadiri ya sala zake

Sala ya mdomo ni kiingilio cha sala ya binafsi. Asiyesali kwa maneno mdomoni atafikia sala ya ndani kwa shida, hiyo ni taratibu ya wote. Katika jumuiya ya kikristo,sala ya sauti haiwezi kudharauliwa. Kwa uhakika sio sala ya Liturujia inayosaliwa kwa amri ya Kanisa. Kundi linaposali,Kristo anasali kama kichwa cha kanisa,na wanachama wanakusanyika mbele ya Kristo.

Padre Jordan kamwe hakudharau sala za binafsi.Ni wazi, hakuwa na shida pamoja na kusali kwa kuvuta pumzi.Alisali Breviari na sala za jumuiya,kamwe hakupenda kutumia kitabu kingine vya sala.[128] Alisali sala za kutunga mwenyewe kwani alijazwa neema na Mungu.Kitabu cha sala kingekuwa kizuizi kwake. Lakini alijifunza kwa namna ya pekee,

[128] Mapadre wazee niliowauliza kuhusu hili waliniambia kwamba daima alisali toka moyoni.Mawazo ya Breviari yake na nia zake kubwa za uchungaji zilitosha kwake.

kutumia vitabu vya Liturujia kama sala.Breviari ilikuwa sala yake ya moyo.Katika injili na katika aya Zaburi,alitafsiri kabisa hitaji lake masifu yake kwa Mungu.Alipenda kunakili na kuzitumia kama sala za mara kwa mara,hasa nukuu za rejea ya kuwa na matumaini kwa Mungu. Ndiyo maana aliwashauri tena na tena wafuasi wake kuzifanya sehemu hizo za Biblia kuwa mali yao binafsi. Padre Jordan alisema mara moja kwenye mkutano: *Yatupasa kujiingiza wenyewe katika roho ya Ofisio.Kwa hiyo, msisali tu,lakini muingie ndani kabisa ya fumbo kadiri inavyowezekana…*[129]

*Mara ngapi tunasoma kwenye Ofisio: "Katika wewe Ee Mungu, nimetumaini,usiniache niaibike kamwe!", au"Kwa sababu amenitumainia, nitamweka huru; kwa sababu amelijua jina langu,nitamlinda."…Si kila mmoja anaweza kuendelea katika hili kwa urahisi; lakini nyote mnalazimika kujaribu kusonga mbele kadiri inavyowezekana.(…)Ili msiende kwenye uzima wa milele halafu maana na umuhimu wa maneno haujawaingia moyoni.Mpendwa Mwokozi angesema nini? "Amesoma na kusali mara nyingi, lakini hakuwa makini."*[130]



Padre Jordan pia anatuonya: *Salini Rozari kwa makini na Ibada, kwa kweli ndivyo ambavyo kila sala nzuri ingetolewa. Na hivi pamoja na mtazamo wa maisha na mateso ya Mungu Mwokozi,ili kwa kumtafakari Mungu Mwokozi wetu tuwe kama yeye..*[131]

Watawa wote watoe baadhi ya muda wao kila siku kwa ajili ya tafakari, ili kupata ukomavu wa kiroho na uchungaji wenye kuleta matunda.Padre Jordan alionyesha umuhimu mkubwa wa tafakari: *Mdumu katika tafakari ya kila siku,mioyo yenu iwe na Yesu tangu mapema asubuhi,ili muangaziwe na*

[129] Chap. 19.05.1899, DSS XXIII, 312
[130] Chap. 10.12.1897, DSS XXIII, 158-159
[131] Chap. 10.02.1899, DSS XXIII, 276

*mifano mitakatifu ya maisha yake na kuangaziwa na upendo wake.*[132] *Mkiacha hiyo [yaani meditation] mara moja tu sio mbaya.Lakini ikitokea mara kwa mara, uwe na uhakika kwamba unaingia katika hatari kubwa na uharibifu mkubwa sana.Ni katika tafakari mtu lazima atafute mwanga na nguvu ili aweze kujilinda dhidi ya roho ya ulimwengu huu kama ilivyo silaha.*[133] Anachukulia tafakari kama chemchemi katika jangwa,ambapo mmoja anapata nguvu mpya na kufarijiwa. Mtu lazima apumzike pale na kujiweka sawa kwa kazi na mateso ya kichungaji. Mmoja lazima atafute mwanga pale na elimu ya kutojipoteza katika mawazo ya kidunia: *Kwa hiyo kamwe tusifikiri kwamba sababu tumeitwa kwa utume basi tusifanye juhudi kwa maisha ya kiroho au kwamba tungeacha kujitakatifuza wenyewe.*[134]

Padre Jordan hakuwapenda mapadre waliokuwa bora katika kazi ambao kamwe hawangekuja kupumzika kwenye tafakari. Kazi yoyote, kadiri yake,ingeleta matokeo ya umoja wa kweli na Mungu. *Msitumainie kazi zenu,akili zenu, au elimu zenu! Kama hazikufanywa zizae matunda na baraka za Mungu,angalieni!*[135] Aliamini kwamba, kuokoa roho ni kazi ya neema za Mungu. “Sababu bila mimi hamwezi kufanya lolote.”[136]



Alimwambia Padre Pancratius Pfeiffer: *Unaweza kupanga kadiri uwezavyo,kama wanachama hawana moyo, kila kitu ni bure.*[137] Tunaweza kupata neema tu kwa njia ya muungano wetu na Kristo. Kadiri mmoja anavyoishi kwa kuungana na Mungu, ndivyo atakavyofaulu kuwa mtume. *Kama tukitaka kuuongoa ulimwengu,lazima tuwe na roho ya Yesu. Hatuwezi*

[132] DSS X, no, 1112

[133] Chap. 08.10.1897, DSS XXIII, 129

[134] Chap. 02.12.1898, DSS XXIII, 246

[135] Chap. 12.06.1896, DSS XXIII, 64

[136] Jn 15:5

[137] Fr.Pancratius Pfeiffer, Gedankenaustausch, 312

*kuwaongoa watu,Kristo tu anaweza kufanya hivyo kwa njia yetu:ndio maana lazima tukubali kabisa kuongozwa na Kristo na kuunganishwa kwa upendo pamoja naye.*[138]

Muunganiko huu mara nyingi umeletwa na tafakari ya kudumu na fikara juu ya maisha ya Yesu.*Kadiri tunavyomsogelea Mwokozi aliyeteswa na kudharauliwa,mtu wa sala na tafakari, ndivyo utakavyokuwa utajiri wa matunda ambayo yatakua kutoka kazi zetu katika shamba la mizabibu la Bwana.Kwa vile sasa hatuwezi kusali usiku mzima,yatubidi kuweka walao masaa fulani kwa kutanabahi na Masifu au Ofisio.*[139]

Alichokihisi yeye mwenyewe kwa imani na alichowashauri wengine kinawekwa kwa ufupi hivi:*Kama mkiwa watu wa sala, basi hakuna maadui watakaotudhuru;Bwana atawaharibu.*[140] *Vinginevyo, kazi zikiwa muhimu zaidi kuliko tafakari Shirika litakuja kuharibiwa.*[141]



Padre Jordan kamwe hakutilia mkazo mtindo fulani wa sala. Mara nyingi anazungumzia juu ya masharti ya sala bora, lakini kamwe juu ya mtindo fulani. *Jitahidini kwa nguvu zenu zote kuwa watakatifu,halafu mtajisikia vizuri.Halafu kwa uhakika mtapata mawazo.Msipojitahidi kuwa watakatifu, hamtapata mawazo ya kutafakari. Nikijua mnafanya jitihada ya kuwa watakatifu, halafu ningesema: fanyeni lolote mnalotaka.*[142]

Sababu ya upole wake, moyo ulio kama wa mtoto, Padre Jordan kwa kawaida alikuwa akielekea kusali sala rahisi.Kwake, wazo moja tu lilitosha kujifungamanisha kabisa katika mduara wa upendo, kujiachia kwa furaha kwenye

---

[138] DSS X, no, 226

[139] Maelezo kwenye mkutano mkuu wa kwanza 06.10.1902, DSS XXIII, 471

[140] Chap.29.11.1895, DSS XXIII, 48

[141] Chap.09.05.1896, DSS XXIII, 56

[142] Chap.02.12.1898, DSS XXIII,

mapenzi ya Mungu.Alipokuwa mseminari,alijiandikia mwenyewe: Usifu na ushukuru daima, popote utakapokuwa, hasa unapoona kazi ya mikono Yake hata kama inafaa kidogo tu kwa matendo na maneno.[143]

Ukisoma mazungumzo Mwanzilishi, unaweza kutambua kwamba anarudia mara tano wazo lilelile fupi, kana kwamba ni msemo: “Muwe watu wa sala” au “Lazima niwe mtakatifu, kwa hiyo, kila kitu lazima kiwe kitakatifu.”

Kadiri tunavyosali, ndivyo sala zetu zinavyokuwa rahisi zaidi.Kwamba zaweza kuleta mtazamo ambao hatuwezi kuomba tena. Hatuwezi kutunga maneno mazuri na sentensi zaidi,lakini bado hatuwezi kuvurugwa. Daima, wazo lilelile, maneno yaleyale yanarudia.: “Yesu, jinsi gain u mwema, mimi ni wako.” Kwa upande mmoja, tunataka kusali, na kwa upande mwingine hakuna sababu ya kufafanua wazo hilo zaidi.Kweli, Padre Jordan alikuwa mtaalamu katika sala hiyo rahisi.Aliweza kuendelea kusali kwa masaa; bila kufikiri aliweza kutunga sala nyingi sana. Kwake yeye, ilitosha kuupata upendo wa karibu wa Bwana wake.Hakutaka mambo mengi kwa kufanya sala bora.Alijua kuwa Yesu yupo; alifungua moyo wake Kwake  na alijisikia furaha katika uwepo wake.Huko kweli ni kusali.Anaandika: *Muwe marafiki wa Bwana wetu katika Tabernakulo: umoja naye unaondoa uchungu wote,na uwepo Wake hautambui unyong’onyevu au uchovu.*[144]



Padre Jordan aliweza kufikia maamuzi makubwa kwa tafakari ndogo au fupi. Maisha yake ya ndani yalikuwa yanaongozwa na mawazo kadhaa,yaliyokuja si kutoka kwenye akili au hoja ila kutoka ndani ya uwepo wake. Ni ufafanuzi wa mapendo: Mshangao uliowekwa kwa ufupi:

[143] D I / 98
[144] DSS X, no, 1112,716

*Sali- Sali- Sali- Sali- Sali- Sali.*[145] Mara nane kwa mfululizo anaandika neno ‘confidence’ kumtumainia Mungu[146], na sehemu nyingine mara tano.[147] Inakuja kama lava kutoa kwenye volcano inayolipuka. *Wote, Ee Baba, wote,- wote, Ee Mungu, wote, Ee Yesu, wote, Ee Mwokozi wa dunia, natamani sana kuwaokoa wote!*[148] Sala hii rahisi polepole inakuwa sala ya kupumzika. Katika sala ya kupumzika, Mungu anagusa moja kwa moja utashi na kuamsha katika roho hekima yake na mwanga wake. Utashi hauhitaji tena picha ili kujisikia muungano na Mungu. Sala basi inakuwa ni kitu kinachoshinda kwa upendo wa Mungu.Kweli Padre Jordan alijua sala hii ya kupumzika. *Ni nini kinachofariji zaidi katika bonde hili la machozi kuliko kuruhusiwa kuingia katika uhusiano wa pekee na Mungu kwa njia ya tafakari na tanabahi. Ee binadamu, unapotafakari na kutanabahi mambo ya Mungu, unafanya kazi za malaika!*[149] Baadaye, hata anaeleweka vizuri zaidi anapoandika: *Endelezeni mazungumzo yenu ya kiroho na Mwokozi.Kaeni chini kwa unyenyekevu na upole kwenye miguu yake na kusikiliza kwa makini maneno yake.*[150] *Ingawa kazi zenu nzuri ni nyingi, muziache kila siku kwa masaa machache muwe pamoja na Mungu mpendwa katika mkusanyiko wa sala na tafakari, na ikiwezekana, katika kutanabahi, kujitunza na kujikusanya kwa kweli na kuipata amani tena.*[151] *Msiruhusu chochote kiwasumbue au kuvuruga amani yenu ya ndani;muwe macho wakati wote katika kusikiliza kwa makini sauti ya ndani*.[152]

Bruda Alipius Hansknecht, aliyesafisha chumba chake na ambaye aliruhusiwa kuingia chumbani bila kugonga mlango,



[145] D II / 28- D IV / 33
[146] D III / 7
[147] D IV / 33
[148] D II / 12
[149] D I / 61
[150] D I / 65
[151] D I / 65
[152] D I / 11

alisema kwamba mara nyingi alimkuta mbele ya msalaba, akiwa amezama kabisa katika sala. Hakutambua hata kinachotokea. Mwishoni alipomwona, alisema: “*Nilikuwa sijakuona*”, na: “*Nadhani, hakukuwa na mtu mwingine hapa?”*[153] Upendo waweza kuwa na nguvu hivi kwamba tunapoteza fahamu zetu. Wakati mwingine, uzoefu kama huo unaweza kumchukua mmoja kwa mshangao kabisa.Si shambulio la kushangaza,bali ni mawasiliano ya upendo. Harakati kama hii ya upendo inafahamika kama zawadi tusiyostahili.

## 2. Kipindi cha utakaso

Inaonekana kwamba Padre Jordan alianza kalenda yake 1875 sababu aliishi wakati mgumu sana: Kwa upande mmoja wakati wa muungano wa upendo na Mungu, na kwa upande mwingine ni wakati wa kukataliwa kwa kuachwa na giza. Sala inakuwa ngumu zaidi, kwa sababu kuna nafasi ndogo kwa kazi ya akili na fikra juu ya matokeo ya neema ya upendo. Kwa vile anayemtafuta Mungu hakuzoea kwa matokeo hai ya neema, anajisikia uchovu na ukame fulani. Hali hii ni ngumu kuielezea; ni mchanganyiko wa giza la mtu binafsi na mwanga wa Mungu, wa upendo halisi na ukavu unaoharibu. Kwa njia ya fikara na elimu, mtu anaweza kuja kutambua kutoweza kwake na mipaka, lakini kamwe hataweza kuuondoa ubinafsi na majivuno. Kama mionzi ya jua inavyoliumiza jicho lenye shida, kwa namna hiyohiyo kutiwa mwanga wa tanabahi kunasababisha maumivu na upweke. Mt.Yohane wa Msalaba anaita hali hii “Usiku wa giza”, wakati Mt. mkuu Theresa anazungumzia upofu uliosababishwa na mwanga angavu wa utakatifu wa Mungu Mwanzishi wetu pia alijua kipindi hicho cha utakaso.



[153] Brother Alipius Hansknecht, APS, n, 3.1.2.45

Baadhi ya maandishi mwanzoni mwa kalenda yake yanatupa mwanga fulani wa mawazo kama haya: *Nini kigumu katika hija ya duniani kuliko kumwacha Mungu na mtu kubaki peke yake. Pigo lake litakuwa kama mtu wa baharini aliyeachwa,ameachwa kwenye upweke wa bahari katika giza la usiku.Katika chombo chake kilicho hatarini na kuachwa na wote, anatupwa huku na kule kwa dhoruba na upepo mkali.Hata giza la kifo likinizunguka,ninatumaini Kwako na sitaaibika.Nyota zaniangaza hata kwenye giza la usiku; kweli huniahidi wokovu katika siku za mbele. Katika, wewe Ee Bwana, nimekutumainia, sitaaibika milele.*[154] *Usiwe na moyo wa hofu na kukata tamaa; kama ikitokea kuwa hakuna njia na matatizo yako au majaribuni ya kutisha,jua kwamba Mwojkozi wako, katika muda anaojuaYeye,atakuokoa na kukufariji.*[155]

Anaandika:*Ee roho yangu,jitupe mwenyewe kabisa kwenye mikono ya Mungu; usife moyo,hata kama mitego imewekwa kwako pande zote,simama kwa Mungu,hasa wakati huu mgumu na matatizo yasiyoelezeka. Jua kwamba Mungu mwema anakupenda,hata kama Anakupiga mno.Usikate tamaa bado, na wakati wa siku za amani zaidi,ujitayarishe kwa mateso makali.*[156] Kweli, alijua kabisa kwamba hali hii ni sehemu ya kukua kwa undani, kwani ni wakati huu tu alipoandika juu ya uzoefu wa kimafumbo: "*Kwa uvumilivu roho inaonesha kwamba imejiwekea pembeni upendo na imejivisha kwa moto wa mapendo ya kimungu."( Mt. Cath. Wa Siena ).*[157]

Na katika ukurasa huo huo: *Mt.Rosa wa Lima alipata dhoruba kwa miaka kumi na tano mfululizo pamoja na giza nene la ndani na matatizo,ambapo alijisikia kuachwa kabisa kila siku walao kwa saa moja au zaidi.*[158] *Na Mt.Magdalena wa Pazzi*



[154] D I / 6 – 7
[155] D I / 17-18
[156] D I / 37
[157] D I / 69
[158] D I / 69

*amejikuta yumo katika shimo lililofichika,linalofanana na ziwa lenye kina kirefu, ambapo samba wa kwanza waliomvamia walikuwa ni vishawishi vya kutokuwa mwaminifu,ambavyo vilikuwa na nguvu, kiasi kwamba vilimhimiza hata kumkana Mungu, n.k.... "Ah, sehemu za kuhofia zilikuwa ngapi,za mashaka,za kutotumaini,wakati jehena iliponijia,katika pambano la kutisha mno,kwa miaka mitano,kuniharibu mimi."*[159] Kutoka nukuu zifuatazo, tunaweza kupata ni mara ngapi

Padre Jordan mwenyewe alipiga vita kukataliwa. *Nipe tena furaha ya wokovu wako. Salini daima kwa matumaini makubwa kwa Mungu na kwa furaha isiyo na kizuizi. Kadiri iwezekanavyo epuka hali ya hofu sababu Bwana ni mwenye nguvu na anaweza kukuokoa.Jitahidi kumtumikia Mungu kwa furaha na upendo, na juu ya yote, weka kando aina yoyote ya hofu isiyo na msingi,ambayo haimpendezi Mungu, kwani Yeye siyo mkorofi.*[160] Hali hii ya hofu isiyo na msingi haikuwa woga wa kuadhibiwa na Mungu. Ilikuwa ni hofu ya kutengwa kutoka kwenye asili ya maisha.Kwetu sisi, upendo ni: uwepo na faraja, lakini katika ukweli, upendo ni: Kutokuwepo, tamaa, maumivu.



Mabadiliko haya ya muda wa uwepo wa kina na kutokuwepo na ukavu yanaweza kumbana mtu kwa nguvu. Kila mpenda anajua kwamba muungano huu wa uzoefu wenye mgongano, wakati fulani faraja ya ndani na baadaye upweke mkuu, waweza kuwa ni mateso yanayohitaji imani.Lakini huo ndio utakaso halisi. Kwa njia hii tutapata wema wa Mungu katika umaskini na utupu. Kwa kweli, uhusiano wa karibu na Mungu na kuachwa kabisa havipingani, bali huchanganyika katika upendo. Ni wazi kwamba tunaweza kuupata utukufu wa Mungu katika udhaifu wetu. "Mna vya kutosha pamoja na neema yangu.

[159] D I / 122-123
[160] D I / 62

Nguvu ya kuwa kamili katika udhaifu…sababu ninapokuwa dhaifu, ninakuwa na nguvu."[161]

Ingawa Mungu yupo tayari kumchukua mtu ndani katika upendo wake,atajua utupu na hofu,sababu fumbo linabaki limefunikwa.Mwanzishi pia alijua kwamba umaskini wa kiroho kama huu ni udongo wenye rutuba sana ambapo mbegu ya neema za Mungu inaweza kuweka mizizi.

Tunazungumza kuhusu mwanga wa imani, lakini lazima tuongeze bila kuchelewa kwamba imani kamwe haioneshi mambo yaonekanayo. Padre Jordan hakuachwa katika jaribio la imani, ambalo pia limeitwa usiku wa giza. Alivutwa kwa fumbo la upendo lililoonekana kwa hofu ya kutojua. Ndiyo maana alikuwa na hamu ya kuunganisha matendo na tanabahi katika Shirika lake. Kazi mbalimbali, shughuli na uchovu waweza kuvuruga umoja wa ndani. "Martha, Martha,… kitu kimoja tu ni cha lazima."[162]



Wakati wa ukimya na toba, yeyote kati ya waamini anaweza kujisikia utupu kabisa wa ndani, ambao hauwezi kujazwa na matendo ya nje,bali tu kwa kuachwa kwenye upendo wa Mungu.

Ili kujaribu kuelewa utakaso huu, Yohane wa Msalaba anatumia picha ya kipande cha mbao kilichotupwa kwenye moto. Kadiri kile kipande kilivyo na ubaridi, hakiwezi kushika moto. Mbao inapasuka na moto unakausha maji. Lakini kipande kile kikiwa kikavu, kinaunguzwa na moto. Upendo uliotiwa polepole unakula mizizi ya mtu wa kale kusudi tusijifukuze wenyewe. Lengo la utakaso sio kutaka kujua hali ya dhambi ya mtu binafsi,bali kutaka kumfanya mtu awe wazi na mpole kwa sauti inayosema toka kwenye mimea yenye miiba kama michongoma inayoungua. Moto

[161] II Cor. 12:9-10
[162] Lk.10:41-42

huu unawaka bila shaka unaweza kuleta mwanga kwenye hali yetu ya dhambi na umasikini lakini pia unaweza kufanya kutokaribiwa kwa Mungu kujulikane.

Mwishoni mwa maisha yake, August 1911, Mwanzilishi anaweka Konventi zote ambazo ziko kwa jina lake, katika jina la Padre Paulus Pabst.Wakati mmoja alipofanya uchunguzi juu ya hili alisema “Angalia Baba wewe ni milioneya”, aliangalia, kwa tabasamu,nje ya dirisha na aliangalia Hamberg akisema: “Mimi tu masikini mdhambi”[163] Mungu anapenda kuchagua rahisi ambapo kumeficha miito muhimu.Abrahamu alikuwa mtu mzee bila mtoto, lakini alichaguliwa kuwa baba wa mataifa. Musa alikuwa mchungaji mwenye kigugumizi Mungu alipomwaminisha kwa utume wa kuwaongoza watu wa Mungu nje ya utumwa. Mtumishi wa kawaida alichaguliwa kuwa Mama wa Mungu. Huku kutambua udogo wa mtu binafsi na udhaifu wake hauharibu wala kuzuia kama ambavyo angetegemea, bali humpa mtu mabadiliko yenye heshima ya ziada, kwa sababu amegundua msaada wa Mungu ambao unaziba nafasi ya udhaifu wake.

*Nakutumainia wewe, kwa sababu huruma yako ni kubwa kuliko udhaifu wangu, sina sauti nyingine ya kusikika zaidi ya masumbuko yangu ya ndani.*[164]

Padre Jordan anamhisi Mungu anayeishi kama msingi wa uwepo wake, kama asili ya amani. Mtu anayetanabahi anategemea kupoteza utashi wake.anataka kujitoa mwenyewe ili awe wazi kabisa kwa utashi wa Mungu.

[163] Fr. Paulus Pabst kwa mwandishi
[164] D I / 41

## 3 Sala ya Muungano kamili

Mmoja akijifunua mwenyewe wazi kwa Mungu, atafika baada ya muda mfupi, kwenye sala ya muungano kamili, ambapo sio utashi wake tu bali uwepo wake wote unainuliwa kwenye mazungumzo ya upendo na Mungu. Akili na kumbukumbu zinaweza kuwa na kazi nyingi kwa mambo ya kidunia; lakini utashi wake unaendelea kuunganika na Mungu.Kazi na tanabahi vinakwenda pamoja katika mtu mmoja.Tayari kuna mabaki ya mashaka kati ya nafsi ya ndani ya mtu inayofaidi uwepo wa Mungu na mtu wa nje anayetimiza utume wake. “Wakati Padre Jordan akiwa mahali Fulani katika nyumba, au peke yake kwenye kikanisa, angekuwa amezama kabisa katika uwepo wa Mungu. Kama mmoja angemuuliza kitu Fulani, ilikuwa kana kwamba anafanya juhudi ya kutoka nje ya muungano wa ndani.”[165]



Au kama Padre mwingine anavyoiweka: “ Tulipokuwa tunaongea naye chumbani kwake, ingetokea kwamba, katikati ya mazungumzo, angeangalia kwa ghafla sanamu ya Mama Bikira Maria na kusema sala.”[166]

Tukiwa watu wa siku-kwa-siku, tunafikiria kwenda juu kutoka chini na tunaona taabu katika kukaa juu kwa muda. Watakatifu wanafikiria chini kutoka juu na hawawezi kuwa na kazi nyingi kwa mambo ya kawaida kwa muda mrefu bila kurudi kwenye asili ya kila kitu. Mmoja kati ya Wasalvatoriani wa mwanzo kabisa alisema: Sikumbuki kwamba aliwahi kuongea nami kuhusu chochote kile zaidi kuliko juu ya Mungu au majitoleo yetu ya kitume.”[167]

[165] Fr.Johannes Scharfl, Summarium, &882, uk.193
[166] Fr.Sixtus Kraisser, Summarium, & 683, uk.151
[167] Fr.Tharcitius Wolff,APS, N, 3.2.2.51

Padre Jordan aliweza kusali bila kuchoka.Kwa watu wanaotafakari zaidi habari za Mungu si vigumu kwao kusali daima, upendo unawasaidia siyo tu kuwa na Mungu pamoja na mawazo yao, lakini husababisha umoja unaoendelea pamoja na Muubaji.

Kwa aina hii ya sala isiyovurugwa, hata vionjo vinaweza kuanguka kutoka muda hadi muda.Matendo ya binadamu hayacheleweshi uhusiano na Mungu; kinyume chake, tendo na tanabahi vinakwenda pamoja katika maana kwamba vinaunda umoja ndani ya duara. Hata kazi haionekani kama imesimama: "Tukae tukiwa tumeungana, ninyi na mimi."[168] Padre Konrad Hansknecht anashuhudia: " Kuna wakati alisema sala za kujitungia daima kwa uangalifu sijapata kuona kwa yeyote kabla. Nilipoeleza mshangao wangu juu ya namna hii ya kusali, aliniambia kile alichomwambia muungamishi wake: 'Kama ninasali kwa uangalifu na kusali sala nyingi za kujitungia kama ulivyofanya, ningalikuwa kwenye nyumba ya wendawazimu siku nyingi tayari.'"[169] Kwa Baba Jordan kusali ilikuwa asili yake ya pili. Kalenda yake inashuhudia namna alivyosali vizuri na kwa uangalifu alisali: *"Ee Maria!Ee Bikira! Ee Mama wa Mungu!Ee Malkia wa Mbingu! Ee Mtakatifu! Ee uliyekingiwa dhambi ya asili! Ee Mama yangu na Malikia! Sijui namna ya kukusifu,Ee msaidizi wangu. Ninajisikia zaidi kuliko ninavyoweza kujieleza!*[170] *Au Ee Bwana! Ee Mwenyezi! Katika wewe nimetumaini, kamwe sitaaibika milele! Naweza kufanya mambo yote katika Wewe unayenipa nguvu! Ee Baba! Nisaidie! Wewe ni nguvu yangu,ngao yangu! njoo, njoo, usikawie,mwangalie mtu huyu wa tamaa,amka,na unisaidie! Ee Baba yangu, Mwenyezi! Ee Yesu! Ee Mwokozi! Bwana atasikia tamaa ya maskini*![171] Mshangao "Ee" mara nyingi hutokea katika sala za kimafumbo. *Ni "Ee"*



[168] Yn 15:4
[169] Fr.Konrad Hansknecht, APS, N, 3.1.2.37
[170] D I / 196
[171] D II / 18

*ya mshangao mkubwa na tamaa ya upendo: Ee Bwana, Unajua,, siwezi kueleza!Naweza kufanya mambo yote katika wewe. Ee Mungu, Ee Mwenyezi, Ee yote! Ee Yesu, Ee Mwokozi wa ulimwengu! Nipo hapa, unitume- kwaajili yako, kwaajili ya roho, kwaajili ya Kanisa La Mungu.Yote Ee Baba,yote, yote, Ee Mungu, yote EeYesu,yote, Ee Mwokozi wa ulimwengu, natamani kwa hamu kubwa kuwaokoawote.Ee okoa roho!Ah okoa roho! Ninakuomba na kukusihi, okoa roho!kwa gharama yoyote, okoa roho!*[172]

Wingi wa upendo wa Mungu kwa Mwanzishi wetu ulikuwa na nguvu kiasi kwamba hakutaka kitu kingine zaidi ya kuumwaga upendo huo kwa wengine. Katika hatua hii ya sala, mmoja anatambua kuwa Mungu anafanya kazi katika yeye kutoka ndani.Padre Jordan alipata tendo hili la ukimya wa roho ya Mungu,vinginevyo asingeandika nukuu hizi katika kalenda yake: *Wakati Paulo, ambaye angeushinda ulimwengu, alikwenda Roma akibanwa na minyororo,Mungu alikwenda pamoja naye,akijificha moyoni mwake kama mmoja anavyokaa kwenye kibanda.*[173] *Au: " Angalia, nakwenda Yerusalemu, nikilazimishwa na Roho: Nakutafuta kwa uaminifu,nipo kwenye vifungo vya Bwana.* (Matendo 20:22).[174]



Ni kuamsha ukweli wa ndani wa uwepo wetu. Mt.Therese wa Lisieux anaonesha hili wazi: " Yesu ananilisha kila wakati kwa chakula kipya.Ninaona ndani yangu, bila kujua namna gani kimekuja pale, Kwa kifupi naamini kwamba Yesu Mwenyewe amejificha chini ya moyo wangu mdogo. Kwa njia ya mafumbo, anafanya kazi kati yangu na kuniambia nini cha kufanya kila wakati." Na zaidi, anaendelea: "Yesu anafundisha, bila kutumia maneno yoyote. Kwa muda mfupi, nimegundua ndani yangu ukweli ambao ulikuwa umefichika mbali."[175]

172 D II / 12
173 D I / 159
174 D I / 170 angalia pia D II / 72
175 H.Theresia wa Lisieux, Mijn roeping is de liefde, 1969, uk.172-173

Tendo hili la ndani ya Roho ya Mungu katika moyo wa mtu si lazima zionekane kwa ulimwengu wa nje. Hieronimus Jaegen, mkurugenzi wa benki huko Trier, alijaliwa vipaji vya hali ya juu vya mafumbo, lakini hakuna aliyetambua kati ya wenzake. Ua dogo halikuonesha kitu cha kumfanya awe tofauti.asingeandika "Hadithi ya Roho," kwa utii tusingelijua chochote juu yake sasa. Na bado asingekuwa na utakatifu kidogo.Nani alijua kwamba Dag Hammarskjold alikuwa mtu aliyemtafakari sana Mungu? (Mystic)

Kila 'mystic' alimfuata Yesu kwa njia zake mwenyewe; kwani Mt.Paulo wa Msalaba, ilikuwa ni mapendo ya mateso ya Bwana. Kwa Mt. Francis ilikuwa ni umaskini wa Yesu.Hata juhudi za kitume za Yesu zaweza kumpenya mtu kabisa; mifano mikubwa hapa ni Mt. Francis Xavery na Mt.Ignasius wa Loyola.

Ni wazi, Padre Jodan pia alikuwa na kipaji cha kuponya wagonjwa. Mmoja wa masista wa Tivoli alikuwa anaumwa sana. Aliombwa afunge nadhiri za daima, katika mikono ya Padre Jordan, Mwanzilishi. Lakini hakutegemewa Tivoli. Sauti ya ndani ilimtuma aende Tivoli siku ile.Kwa ujumla, kwanza alikwenda kwa mapadre.Safari hii, alikwenda kwanza kwa masista. Aliposikia hali na utashi wa sista,alipokea nadhiri zake.Sista Clara Rheinwald alifariki akiwepo bado. Hii ilitokea 26,Julai, 1892.[176] Bruda Alexius Berger aliumwa maumivu makali kwenye koo kiasi kwamba alikula chakula laini tu. Walimwambia: Kwanini usiende moja kwa moja kwa mwanzishi? Atakubariki. Alipofika kwa Padre Jordan alimwambia:"Lakini Bruda mbona hukuja mapema? Piga magoti!"[177] Mwanzilishi aliweka mikono yake yote miwili juu ya kichwa cha Bruda, alimbariki na asubuhi iliyofuata, maumivu yalitoka.



[176] Sista Liboria Hansknecht, APS N, 3.1.2.46
[177] Fr.Rudolf Fontaine, APS N, 3.1.2.44

Matokeo ya neema mbalimbali za Mungu ni tofauti na huendana na umoja na utume wa mtu. Lakini asili ni moja: Upendo wa Mungu kwa watu. Katika sikukuu kubwa ya Watakatifu wote 1891, Mwanzilishi alimaliza mkataba wake na Mungu ambapo alijitoa mwenyewe kabisa kwa Mwenyezi, akitumaini kuwa Muumbaji angemsaidia kwa mkono wa chuma.

Katika kalenda yake, tunasoma kwamba alirudia majitoleo yake Desemba 21,1894 anapoandika. *Jifungamanishe karibu na asiye na mwisho na umwombe Akusaidie.Tafuta kila kitu toka kwake ambaye anaweza na atakupatia!*[178] Hakuna neno ambalo linafunua muungano wake na Mungu zaidi kuliko neno analotumia hapa: '*Schmiege dich innig*' "Ingia jiunganishe mwenyewe karibu" na Mwenyezi. Kama moto mdogo aliyetishwa anavyokimbilia kwa mama yake. Maneno muhimu pamoja na undani wa fumbo…Baadaye, Padre Jordan anayaweka maneno haya katika fremu ya bluu. Ni wakati huu na mara moja tu alifanya katika kalenda yake, kwa uwazi atunze umakini wake kwa hicho tu.



"Jiunganishe karibu na Mwenyezi", Hilo ni jibu kwa sala ya Yesu: "Baba Mtakatifu, uwatunze, kwa nguvu ya jina lako ulilonipa katika jina lako, ili wawe kitu kimoja kama sisi." [179] Maneno haya ya Yesu yanachukua asili ya Habari Njema, mwisho wa lengo la binadamu. Hadewijch anaandika kuhusu maneno haya: "Haya ni maneno ya kirafiki mno ya Mungu ambayo hayajawahi kusemwa wazi na kwamba tunayasoma kwenye maandiko Matakatifu."[180] Maneno haya kwa kweli yanachukua wazo la mwisho na kukamilisha kazi zozote za kiroho. Kila kitu kimewekwa huru na wakati huohuo kila kitu hupatikana kwa kiasi kikubwa. "Jiunganishe mwenyewe karibu na asiye na mwisho" ili uweze kuinuliwa katika muungano kamili na Mungu.

[178] D II / 3

[179] Yn. 17:11

[180] Hadewijch, Paul Mommaers, 120

# V

# Maria katika maisha ya Mwanzilishi

## 1. Uchaji ulio kama wa mtoto kwa Maria

Nisingetenda haki kuandika juu ya maisha binafsi ya Baba Jordan bila kutaja nafasi ya Maria katika maisha yake.Kama tukiamini kwamba yote tuliyonayo ambayo yanahusu neema na wokovu, tunayamiliki kwa njia ya Maria,hayo yanaonesha kwa ufupi maisha ya Padre Jordan. Ibada yake kwa Mtakatifu Mama wa Mungu ina msingi wa tabia ya umoja wa ulinzi wa kimama na utegemezi wa kitoto.

Ibada hii kwa Mama yetu tayari alipewa katika ujana wake. Kwenye 'archive'ofisi ya kutunza kumbukumbu Roma bado tunayo picha ya Maria pamoja na mtoto aliyoichora alipokuwa fundi mchoraji.

Alipokuwa mseminari, aliona, katika ndoto, namna Maria alivyotabasamu kwake na kumpa ulinzi.[181] Anaandika katika kalenda yake: *Kamwe msidharau kufurahia na kuendeleza uchaji*

[181] D I / 121

*ulio kama wa mtoto kwa Maria wakati wote; mumruhusu awe wakili wenu katika mambo yote. Ee Maria unichukue na unipokee kama mtumishi wako nisiyestahili kwa milele.*[182] Alipokuwa Seminarini Freiburg alianzisha 'rozari ya wazi' "vivid rosary" na aligawa kadi za sala ambapo wanafunzi waliohusika walitambua alichokuwa anasali.[183] Mtihani wake wa mahubiri kama Shemasi ulihusu Litania ya Maria Bikira Mtakatifu.[184] Daima alimaliza sala zake za Breviari kwa antifona ya Maria.

Desemba 8, 1880, yeye na Joseph Hartmann aliyekaa naye nyumba moja na mwanafunzi mwenzake wa Teolojia, waliahidi, mbele ya sanamu ya Mama yetu wa msaada wa daima katika Kanisa la Redemptorists huko via Merulana, 'Roma' kuanza msingi wa jumuiya mpya ya kitawa.[185]



Uhusiano huu waulinzi wa kimama na utegemezi wa kimwana umefunuliwa kwa namna ya ajabu wakati wa kuanzishwa Shirika. Kwa vikubwa, uanzishaji wa Shirika ulitegemea sana msaada wa Maria.Mwanzilishi wetu amefanya hayo hayo, katika imani kubwa. Alipowapeleka wamisionari wa kwanza huko Assam (India) ushauri wake ulikuwa: *Mheshimuni Mbarikiwa Bikira Maria kwa namna ya pekee, Malkia wa Mitume na mama yetu kwa upendo wa kimwana na Ibada.Amesimama upande wa Shirika letu tangu mwanzo kabisa wa kuanzishwa pamoja na nguvu ya ulinzi wake na msaada mkubwa.*[186]

Alilitolea Shirika lake kwa Maria, wakati lilipokuwa linadumu kwa mawazo na mipango yake. Kabla ya kupata

---

182 D I / 120

183 Dean Josef Blattmann ( schoolmate), Barua ya 20.05 1928 kwa Fr.Bonaventura Schweizer

184 DSS XII, 117- 121

185 *Salvatoriaans Jubileumboek, 106*

186 Chap. 12.12.1890, DSS XXIII, 5

daraja la upadre, 20, Julai,1878,anaandika kwenye kalenda yake: *Kwa msaada wa Mungu na msaada wa Mbarikiwa Bikira Maria na kwa ulinzi wake,weka msingi kwa Shirika Katoliki mapema iwezekanavyo; usichelewe zaidi bila sababu!*[187]

March 13,1880 anaweka kielelezo chake cha kwanza kwenye kaburi la Mwokozi na anaandika kwenye kalenda yake: *Mwombe kila siku Bikira Mbarikiwa sana, ulinzi wa Shirika.*[188]

August 19, 1880, alipokuwa anasali kwenye kaburi la Mt.Canisius huko Friburg, ilikuwa kama sauti inamwambia: "Nenda Einsiedeln.Huko kila kitu kitakuwa wazi." Siku moja baadaye, aliadhimisha Ekaristi kwenye madhabahu na alibaki pale mahali patakatifu akisali mpaka sa kumi alasiriGiza lote la mawingu lilipotea na mara aliporudi chumbani kwake aliandika maneno machache kuonyesha umbo la Shirika lake. [189]



Mheshimiwa sana Padre alianzisha jumuiya mbili wakati wa sikukuu ya Mama yetu Mkingiwa dhambi ya asili. Padre Pancratius alimuuliza: " Kwa nini iwe siku hiyo hasa?" Alijibu: "*Kwa sababu Mungu ameamua Hivyo.*"[190] Lakini kwenye "Der Missionar", Padre Bonaventura Luthen anatoa jibu linaloeleweka zaidi: " Leo tumwombe Maria kwa Ibada kubwa,ili kwamba yeye aliyemponda nyoka aweze kutusaidia kupigana na mwovu ambaye siku hizi ana nguvu kubwa juu ya roho zisizokufa."[191] March 11,1883 alichagua jina la kitawa Francis Maria wa Msalaba.[192]

---

[187] D I / 141

[188] D I / 153

[189] Erinnerungen of Fr.Guerricus Burger, APS I, 93

[190] Chronik desRom. Scholastikates, maongezi ya Fr.Pancratius Pfeiffer 08.12.1936

[191] Der Missionar, 1881, I

[192] D I / 168

Juu ya meza yake, kulikuwa na sanamu ya Mama yetu wa Lourdes.Kwenye mikono yake,mara kadhaa aliweka vipande vya karatasi vyenye sala kwa nia maalum,kwa mfano: "*Mama,saidia" au "Mama, Narni, saidia" "lipa madeni"*.[193] Karatasi hizo tumezitunza 120.Wakati wa mchana alipokuwa anatembelea Basilika la Mt.Petro, mara nyingi alikuwa akitembea huku anasali kwa Mama yetu,na alipokuwa anakaa Freiburg, daima alikwenda kutembelea kikanisa cha Burgeln.[194]

Kutambua tumaini lake kwa msaada wa Mama yake wa Mbinguni, kwa ujumla kila alipoanza nyumba mpya alifungua katika moja ya sikukuu zake.Tivoli Julai 2, Bikira Maria kumtembelea Elizabeti; Lochau Septemba 15, Mama yetu wa huzuni; St. Nazianz August 15, kupalizwa mbinguni Mama yetu; Wealdstone Julai 9, miujiza ya Mama yetu; Hamont Septemba 21,Mama yetu Mkombozi wa Watumwa.



Kila jumuiya ilikuwa na jina "Collegium Marianum". Ilikuwa moja ya furaha zake kuu wakati Askofu alipokabidhi madhabahu ya Maria kwa Shirika, yaani Noto na Narni. Alitamani kumwacha huru Padre wa mwisho kwa lengo hilo. Alipokuwa bado hai, wakuu wa Provinsi walimshauri aache Noto na Narni, kwa sababu hazikuwa na matumaini tena baadaye, lakini daima alikataa kabisa.

## 2. Tabia za ibada zake kwa Maria

### a. Ugumu

Wakati litania zinakuwa ndefu zaidi na zaidi na majina ya Mama yetu yanakuwa mengi, Padre Jordan aliendelea kwa ugumu na msimamo mkali wa Ibada kwa Maria.

---

[193] DSS XXI, 7 – 17

[194] Fr. Paulus Pabst kwa mwandishi

Padre Paulus Pabst, mlezi wa wanovisi wakati ule, alitaka kulipa Shirika tabia ya Maria kwa ufupi. Aliwafundisha wanovisi kufanya kila kitu “kwa njia ya Maria, pamoja na Maria na katika Maria.”Mwaka wa 12 wa uwepo wa Shirika ulikuwa mwaka wa Maria na ulifungwa kwa sherehe kubwa na Mwanzilishi alijiweka wakfu kwa Maria.Mwisho wa mwaka wa jubilee 1893, walianzisha tabia ya kuvaa rozari juu ya singulumu. Mwanzoni Padre Jordan alikataza kwasababu ingekuwa kizuizi kwa uchungaji. Alipoachia, alitaka basi iwe rozari ndogo kama ile tunayoweza kuiona bado kwenye sehemu ya kumbukumbu Roma.[195]

Tukikusanya maandishi yote ya Mwanzilishi, tunaona kuwa alikuwa na maandishi kidogo sana juu ya Maria.Tayari Maria alikuwepo katika kila kitu alichofanya. Alipenda kuongea kwa kifupi juu ya Maria na aliandika mafundisho mafupi ya kuongeza Ibada kwa Maria.Lakini alibaki katika ugumu na busara katika yote haya.



## b. Ukunjufu

Ibada ya Padre Jordan kwa bikira Maria haikuwa matunda ya masomo au elimu; imekuja moja kwa moja toka moyoni mwake. Kwangu mimi, upendo wake kwa Maria ilikuwa ni zawadi toka kwa Mungu.Angekuwa na hali ya kutogeuka nyuma kamwe alipomkimbilia Mama Maria kwa matumaini makubwa.Kwa kujua kabisa alijiweka wakfu kwa Maria akitumaini kwamba angemuunganisha zaidi na zaidi na kazi ya ukombozi ya Yesu.

Alipenda sana kusali rozari kwa sababu, kwake, ilikuwa sala kutoka moyoni. Maisha yake ya sala yalibaki kuwa rahisi kwa njia ya uchaji wake wa kimwana kwa Maria.Wafuasi wake wa kwanza walishuhudia kwamba uchaji aliokuwa

[195] Fr. Dorotheus Brugger kwa mwandishi

nao Mwanzilishi kwa maria haukuwa wa kijuujuu tu na haukuelezewa kwa kutia chumvi, bali umekuwa wa asili na kweli**.** Kwenye kikanisa kidogo**,** kulikuwa na sanamu ya Mama yetu wa huzuni chini ya msalaba. Baba alimwona yeye pale katika sala, kwa mikono iliyonyooshwa, na kulalamika: "Bitte, Bitte!" (samahani!)[196] Kwake, Maria alikuwa picha ya kimama ya Mungu.Kadiri yake, kusingekuwa na msalvatoriani hata mmoja bila heshima, upendo na ibada kwa Maria.[197] Kwani Anaweza kutuonyesha njia ya kwenda kwa Yesu, kama Mwanzilishi anavyoandika katika sala ya kujiweka wakfu Desemba 8,1893:*Utufanye wafuasi waaminifu wa Yesu Mwanao na wa Watakatifu na Mitume, ili tuweze kufuata nyayo zao mpaka kifo.*[198]

## c. Unyofu



Ibada ya Mwanzilishi kwa Maria ilikuwa na muungano wa kushangaza.Ilikuja toka moyoni mwake, haikuhitaji mabishano ya kitaalamu,wala vitabu: Iliendeshwa kwa upendo wake wa kimwana.Ni vigumu kuelezea muungano huo, lakini, kwa mmoja anayependa kweli, si vigumu kuelewa.Kila mmoja anaweza kufuata ibada hii kwa Bikira Maria kwa namna yake, kwa sababu inakwenda mbali ya mipaka ya binadamu.Sharti ni kwamba ibada hii inatafuta chanzo na hutegemea msingi wa kiroho wa kuwa na matumaini na kufuata mfano.Uchaji wake ulikuwa na nguvu kama hamira katika maisha yake; ulikuwa kama muziki uliopigwa kwa kuvutia uliotungwa kwa namna mpya hivyo kuufanya ufurahishe.

[196] Fr. Paschalis Schmid, *Summarium* I, & 1047, p.233
[197] *Der Missionar, 1891, 6*
[198] DSS XII, 4-5

# 3. Picha ya Maria.

Mwanzishi wetu ana picha yake ya Maria, ana uso uliofanana na wa Kristo; ana kila kitu anachotuomba Kristo.Ndiye yule Kristo aliyempenda sana. Kwanza, kila mmoja ana picha yake ya Maria katika moyo wake. Kuna picha nyingi mno za Maria kama walivyo waamini. Tukitaka kuelezea picha ya Maria kwa mwanzishi wetu, tunaweza kufanya kwa namna au sehemu tatu. Katikati, picha ya Maria, Mama wa Mwokozi, pembeni picha ya mkingiwa dhambi ya asili na ya Malkia wa Mitume.

## a. Mama wa Mwokozi

Wakati wa ujana wake, Padre Jordan haikuwa rahisi kupata alama zozote za upendo toka kwa mama yake. Pamoja na kaka zake wawili, mara nyingi waliachwa wajitunze wenyewe kwa sababu mama yake alitakiwa kufanya kazi nyingi na ngumu kwenye mashamba.[199]



Kwa njia ya Ibada zake kwa Maria, moyo wake ungemwaga upendo wote ambao asingeweza kuuonyesha kwa njia ya kibinadamu. Katika mazungumzo yake, alipenda kumwita Maria kwa kiitaliano*: la nostra cara mamma celeste*.[200] Katika kalenda yake daima anamwita Maria: '*Mater Dei et Mater mea.*' Alitaka wafuasi wake wamheshimu Maria kwa upendo wa kimwana. *Katika Shirika, kusingekuwa na msalvatoriani hata mmoja bila heshima, upendo na ibada kwa Maria*.[201] Siku hizi, tunapozungumza juu ya Maria, maneno "heshima, juhudi, kwa moyo" yanaonekana kutiliwa mashaka. Tayari maneno ya Mwanzilishi hayako mbali sana na mafundisho ya Mababa wa Mtaguso ambao

[199] AS I, nos.129 na 176

[200] Br.Giuseppe Capparella kwa mwandishi

[201] *Der Missionar,* 1891, 6

hawakuogopa kutumia maneno kama hayohayo. Kanisa linatuomba tumkaribie Maria kwa “uchaji wa kimwana wa kujiunganisha”, kwa kumchukulia kama “Mama mwenye upendo mkuu”[202] “Ukarimu wa Mama wa Mungu Mwokozi”.[203] “Anawatunza kaka wa Mwanae kwa upendo wa kimama.”[204]

## b. Mkingiwa dhambi ya asili

Katika picha tatu za Maria ya katikati ikiwa ya Mama wa Mwokozi, upande mwingine tunayo picha ya mkingiwa dhambi ya asili. Mwanzilishi alifikiria juu ya picha iliyoandikwa kwenye kitabu cha ufunuo: “Mwanamke aliyevikwa jua na mwezi chini ya miguu yake,na taji la nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake.”[205] Ataponda kichwa cha nyoka wa Jehenam.Kwake, Maria alikuwa ni mwanamke atakayemsaidia katika mapambano dhidi ya nguvu za giza. [206]



Picha ya Shetani kupambana dhidi ya mwanamke ilitiliwa mkazo sana wakati wa Padre Jordan.Shetani alikuwepo. Mwanzishi alimwona katika kazi iliyokuwa kama vita ya wapinga Mungu huko Ujerumani na katika matendo ya kushika dini mno bila akili huko Italia. Alipokuwa akimtoa Shetani Bruda Felix, Padre Jordan alimhisi nguvu za kishetani kwa namna ya pekee.[207] Aliamini kwamba jehena ingebadilika dhidi ya Shirika ambalo lilikwishatangaza vita ya wazi (dhidi yake) na ambalo lilishapanga kushika roho za watu na kwamba liliona kuwa limeshashinda.[208]

[202] *Lumen Gentium, no.* 53
[203] *Lumen Gentium, no.*61
[204] *Lumen Gentium, no.*62
[205] AP. 12 : 1-6
[206] Angalia “Statutes za 1882” kwenye *Manna,* Desemba, 1881; Chap. 29.12.1895, DSS XXIII, 53
[207] Fr.Bonaventura Luthen, “Lucifers Erscheinung in Rom”, 29.12.1895
[208] Chap.15.02.1901, DSS XXIII, 400

Wakati wa jubilee ya miaka 25 ya Shirika, Mwanzilishi anawaandikia wanachama: *Angalieni namna mwovu anavyopigana kwa fujo.*[209]

Siku hizi, hatutumii maneno au misemo hiyo tena.Hatumwoni mwovu akifanya kazi tena.Tunaposikia juu ya kutoa pepo, tunafunga macho. Lakini kama tukitaka kukaa kwa utulivu na uaminifu, tunaweza kuona nguvu za uovu zikifanya kazi siku hizi. Na kwetu, Maria ni mwanga mwangavu wa matumaini, kama katiba ya kanisa inavyothibitisha katika maneno yake ya mwisho.

Kwa Padre Jordan, mkingiwa dhambi ya asili alikuwa ni alama ya imani na matumaini na kwamba nia njema hushinda uovu.

## c. Malkia wa mitume



Upande mwingine tunaona picha ya Malkia wa Mitume.Kadir ya Bruda aliyechora picha hii, Maria ni kiini cha utume wetu. Ni yeye anayewapeleka wamisionari sehemu zote za dunia.Ni yeye anayeangaza utume wa uchapishaji. Ni yeye anayewalinda masista katika kazi zao za kuwa tunza wagonjwa na watoto.Ni yeye anayeleta miito katika Shirika. Anawaangaza Wasalvatoriani kujitoa wenyewe kwa namna na njia zote ili Yesu ajulikane, kupendwa na kutukuzwa zaidi na zaidi. Ndiyo maana Shirika lina kazi ya kutangaza sifa za Maria mahali popote linapokaa.

Alipokuwa Friburg (Uswisi) sababu ya vita Mwanzilishi aliandika kwa Padre Fulgentius Moonen Roma: *Niletee, haraka iwezekanavyo, orodha ya majina yaliyoandikwa kwa mkono ya 1915; ipo juu ya meza yangu, chini ya miguu ya Madonna.Lakini uwe mwangalifu ili karatasi mikononi mwa Madonna*

[209] DSS X, no.854

*zisidondoke*[210] Ni ishara nzuri kama ya mtoto kujieleza namna Maria mwenyewe ambavyo angewalinda wanachama.

Miaka 12 ya Shirika ilikumbukwa Roma kwa sherehe kubwa kwa heshima ya Mama yetu pamoja na kujiweka wakfu alikoandika Mwanzilishi mwenyewe. Pale anauliza: *Utufanye wafuasi waaminifu wa Yesu Mwanao na wa Watakatifu na Mitume, ili tuweze kufuata nyayo zao mpaka kifo.*[211] Ndio maana, kama padre Jordan anavyoandika: *Shirika lazima litangaze utukufu wa Maria popote litakapokuwepo. Ingekuwa juhudi zetu nzuri kujitoa wenyewe ili kwamba Mama mtukufu na Malkia asifiwe na vizazi vyote.*[212]

Septemba 5, 1891, miaka 10 ya Shirika viongozi wa Kanisa walimpa mwanzishi nguvu ya kupanga kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi kama ni siku maalum ya Maria.



[210] DSS X, no. 1200
[211] DSS XII, 4-5
[212] DSS X, no. 1112

# VI

## Kumezwa na Matashi yasiyowezekana

Upendo wa Mungu unaweza kuwa moto uwakao ndani ya mtu. Yesu anasema:” Nimekuja kuleta moto duniani,na ningetamani uwe umeshaanza kuwaka.”[213] Upendo wa Kristo unavunja mipaka yote na nyakati zote. Mt. Therese wa Lisieux pia anasema: “Ningependa kuvuka dunia yote, kutangaza jina lako…Ningependa kutangaza Injili katika mabara matano kwa pamoja mpaka visiwa vya mbali kabisa.”[214] Haiwezekani lakini bado ni matashi ya kweli au nia njema.

Kwa namna hiyo hiyo, Padre Jordan alitamani kutangaza Injili ya Kristo kwa watu wote na kwa njia zote ambazo Kristo anaangazia. Moto huu usiozimika haujui muda wala mipaka ulimmeza tangu mwanzoni kabisa.Tabia ya kwanza ya kuanzisha Shirika ya Padre Jordan ni ile ya kuwa kumbakumba. Wakati wa Christmas usiku (1896) *wazo la*

[213] Lk. 12:49

[214] H.Theresia wa Lisieux, Mijn roepingis de liefde, p.162

*kikatili la kuokoa watu wote lilinijia.*[215] Wakati wa sikukuu yake ya kuzaliwa 1897, anaandika: *Karibu ningependa kusema, kwa kuhakikishiwa kitakatifu, kamba mapenzi ya Mungu yamejionesha kwangu hivi karibuni. Shirika lina utume mkubwa!*[216]

Tamaa hii isiyokatishwa daima ilikuwa utakaso mkubwa kwake. Alidhani kwamba Shirika lake halikufikia mtazamo wake. Zaidi ya hayo, juhudi yake isiyozuilika kwa ajili ya roho ilibanwa vikali na mkaguzi wa kitume. Hakuruhusiwa kuanza nyumba mpya za kitawa, kukopa au kuwa na deni, kupokea wakandidati ambao hawaezi kulipa kodi ya makazi. Kwa uchungu hakuweza, aliona namna kila nyumba, sababu ya ugumu wa mwanzoni, ilivyokuwa inajitegemea kwa nafasi ya kwanza na hakufikiri kwa ujumla wake. Karama ya kitume kwa wote na kila mahali ilikuwa hatarini kupotea.Pia aligundua jinsi kazi zilivyotishia kuchukua nafasi ya juu zaidi kuliko kutanabahi.Ilikuwa uzoefu wenye kutia uchungu ambao unasababisha kujisikia kukata tamaa.Alikwenda njia yake ya Gestemani.Padre Luthen anaandika: “Mchana na siku ya kuanzisha,Padre Jordan aliteswa na kishawishi kikubwa sana, alitaka kuacha kila kitu;alichukizwa na Shirika ambalo, kwa kweli, alilipenda mno.Ilikuwa hali ya kutisha.”[217] Padre Jordan anaandika kutoka Lochau kwa Padre Luthen Septemba 3, 1902: “ *Mwelekeo wa Shirika ni mgumu kwangu kuuchukua, unaniumiza…Bahati mbaya yote haya yana matokeo mabaya juu ya nia zangu na afya yangu. Mwaka huu nimebadilika kwa kiasi kikubwa, kwamba hii imenifanya niwe makini*.[218]



Huku kukatishwa tamaa, hasa wakati wa mkutano mkuu wa kwanza uliofunguliwa Octoba 6,1902, umehamasisha tamaaya kuunda Shirika jipya. Alijua zaidi kuliko kabla

[215] Notizen, Archives II / 3 angalia *Das Gebetsleben P. Jordans*, 106
[216] Chap. 04.10.1897, DSS XXIII, 127
[217] APS, G, 14
[218] DSS X, no. 617

kwamba utume ungeimarishwa na sala. Octoba 9, anaandika kwenye kalenda yake: Ee Bwana, kwako tu sifa itolewe mchana na usiku. Nitaweka mlinzi kwenye kuta zako, Ee Yerusalemu: mchana wote na usiku wote hawataacha kulisifu jina la Bwana.Kurasa mbili zaidi, Novemba 21,anaandika: kipindi kipya kinaanza sikukuu ya kutolewa Bikira Maria Mbarikiwa.[219] Anapoandika hivi, anafikiria juu ya Shirika jipya.

Shirika hili jipya lingekuwaje, imeandikwa kwa kifupi:*Ee Bwana, kwa utukufu wako na kwa wokovu wa roho,kulingana na nia.Nina lengo la kuanzisha Shirika la mabikira watakatifu na Shirika la wanaume watakaolisifu jina lako mchana na usiku na watakaojitoa katika sala kwako.Ee Bwana unisaidie,katika wewe nimetumaini, sitaachwa kamwe.(Wamonaki na Masista) Katika kundi watawa wa kike kuwe na kundi la Masista watawa na Masista walei.Kanzu ya kitawa inaweza kufanana. Licha ya sala, tafakari, sala masifu aou ofisio na mazoezi ya toba, ikiwezekana, yangejumlishwa na masomo, lakini mapumziko ya lazima yasikosekane.*[220] *Na zaidi: Ah, kwamba ningeanzisha kila mji walao kundi la mabikira watakatifu watumie mchana na usiku kuabudu mbele ya Sakramenti, Mwokozi wa dunia, aliyejificha ndani ya maumbo ya mkate(Ekaristi). Naweza kufanya yote katika Yeye anayeniimarisha.*[221]

*Mwezi mmoja baadaye anaandika:Ee Bwana mbona umeniacha?Ee Mungu mwenyezi, nisaidie! Simama unisaidie! Ee Bwana, Wewe waweza yote, kwa nini hunisaidii? Nakutumainia wewe tu, Wewe ni ngao yangu na kimbilio langu! (Januari 14,1903)*[222] Tamaa hii ya kuanzisha “Shirika” jipya ni ya pekee.Alishakumbana na matatizo makubwa sana ya



[219] D II / 40
[220] D II / 42-43
[221] D II / 44
[222] D II / 45

kutatua shida za mashirika yake mawili.Tayari alishakuwa na mkaguzi wa kitume sababu ya matatizo yake ya kifedha.Alikuwa na miaka 54, aliumwa shida ya mishipa ya fahamu na matatizo ya tumbo.Na lengo la hili Shirka jipya litakaloanzishwa halikuwa tofauti na lile ambalo tayari lipo.Hata alitaka kuwapokea wasaidizi wa kwanza wa Shirika jipya kutoka Shirika lake mwenyewe.Lakini walihitajika zaidi pale. Aliwaeleza hata mapadre wake vijana, ambao walishangaa na walihofu.[223] Waliomba ushauri wa mapadre Luthen na Pancratius. Lakini hayo hayakuvuruga mradi wa Mwanzilishi. Walishajua juu ya miradi isiyowezekana na mawazo ya Mwanzilishi yaliyosumbuliwa. Kama tusomavyo kataka kalenda yake, ufahamu huu unakuwa chanzo cha kudumu cha mateso na mahangaiko. Alitaka kufanya mambo mengi sana, kuyapanua, na kuyafanya kwa undani. Ilikuwa zaidi wakati wa jioni na usiku alipoteswa na mipango hii isiyowezekana. Alipata faraja katika sala: *Jitoe kwa sala hasa wakati wa jioni na usiku. Sala za usiku ni hazina!*[224] Matokeo yake ni kwamba wakati fulani asubuhi hakutulia na alikuwa na ukatili Fulani sababu ya uchovu. Baada ya chakula cha asubuhi, angeweza kumkemea mmoja kiasi kwamba wengine wangekimbia![225] Mahangaiko haya ya kudumu kati ya kutaka na kutoweza kwake yalikuwa chanzo cha maumivu ya ndani. *Katika Wewe, Ee Bwana, nimetumaini, sitaaibika milele. (Januari 23,1903)* [226]



Lakini hata marafiki wakubwa wa Mungu mara nyingi hawapati wanayohitaji. Ni wazi, Padre Jordan alijua hilo pia. Anaandika kwenye kalenda yake: *Kwa utukufu wa Mungu na kwa wokovu wa roho,anzisha kwa msaada wa Mungu Shirika kwa heshima ya Mbarikiwa Bikira Maria Mkingiwa*

[223] Mapadre Lukas Klose na Paschalis Schmid kwa mwandishi
[224] D II / 68
[225] Studi ya Fr.A.Scneble, no. 79 / 99
[226] D II / 45

*dhambi ya asili.Ee Bwana, unisaidie;niko tayari kwa lolote,nakutumainia.Ee Mwokozi,Wewe uliyekuwa mtu kwa ajili yetu,simama unisaidie kwa mkono wako wenye nguvu! Ee Mama wa Mungu, uwe mlinzi wangu na msaidizi mwenye nguvu! (March 24,1905,vijilia ya kutangazwa kwa Bikira Maria Mbarikiwa.)* [227] Na zaidi anaandika: *Licha ya mateso ya ndani na ya nje kuwa makubwa, na kukandamizwa kwa giza na woga, yaonekana kuwa haiwezekani kukwepa, mtumaini Mungu zaidi, jifungamanishe naye na utende bila woga kulingana na malengo uliyojiwekea.*

*Mungu hawezi kukujaribu zaidi ya nguvu zako na ataliweka jambo hilo katika mwisho wenye furaha. Daima nenda mbele za Bwana!*[228] Hii iliandikwa April 9,1905, na April 19, anaandika: *Pamoja na msaada wa Mungu, anzisha Shirika kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa roho! Ah, inaweza kuwa vizuri sana!*[229] Alibeba msalaba huu mzito kwa miaka saba.



Mara ya mwisho alipoamua kutekeleza yahusuyo mradi wake ilikuwa April 26 mpaka 28,1908,alipokwenda kuhiji kwa Mama yetu wa Loreto.*Kura imeshatupwa, jiunganishe na Mungu, kamilisha kwa njia ya Kristo Yesu msulubiwa. Watu wote, makabila yote, mataifa n.k,wote.*[230]

Padre Pancratius Pfeiffer aliyesoma kitabu, hasemi neno hata moja kuhusu hili katika historia yake fupi. Alikuwa kama mfanya biashara, aliyetaka kukwepa, katika historia yake fupi kwa Mwanzilishi, kila kitu ambacho kingeleta chuki isiyo ya lazima, lakini hiyo ndiyo sababu mpaka sasa sura yote ya maisha ya Mwanzilishi ilifichwa. Maandishi ya kwenye kalenda yanayozungumzia juu ya lengo la kuanzisha Shirika jipya yasomwe kwa mtazamo huo. Halafu

[227] D II / 87
[228] D II / 87-88
[229] D II / 88
[230] D II / 114

tunaweza kuona karibu kila wazo la kwenye kalenda linaonesha mahangaiko. Imekuwa ni tatizo la ndani na la kibinafsi kati ya muumbaji na kiumbe chake. Ilikuwa ni maumivu kama yatokayo kwenye moto uwakao katika roho ya Mwanzilishi. *Simama kama moto*![231] Si kwa bahati mbaya Padre Jordan anaunganisha tamaa hii kubwa kwenye "mkataba" wake.

Anaandika:*Ee Mungu mmoja mwenyezi,unionyeshe mapenzi yako! Mama wa Mungu, Mama yangu, uniombee,ili niweze kufuata na kutimiza mkataba wangu. (Januari 8,1909)* [232] Na zaidi: *Ee Mungu Mwenyezi ,unisaidie kadiri ya Mkataba.(Januari 22,1909*) [233] , *na .Februari 5,1909: Tunza mkataba uliouweka na Mungu!Lakini sio chini ya mateso na dhambi.*[234]

Sababu ya kuwa na matumaini makubwa kwa Mungu, Padre Jordan hakuridhika na ukweli tu. Anajiandikia: *Kama ukitaka kupata kitu fulani toka kwa Bwana, utapata chochote uombacho kwa njia ya sala.*[235]



Padre Jordan aliunda kiini cha sala zake toka "tamaa" zake.Kutoweza kwake kutambua wingi wa yale aliyoyatamani kumekuwa ni mahali pa kukutana na Mungu. Kwa njia ya sala, gogo limekuwa kavu hivyo kwamba limeweza kuliwa kabisa na moto wa upendo wa Mungu.

[231] D II / 44
[232] D II / 121
[233] D II / 121
[234] D III / 1
[235] D II / 72



Mwenye heri Mama Maria wa Mitume
1833-1907

Mkuu wa Shirika wa kwanza wa Masista wa Mungu Mwokozi



Padre Jordan mwaka 1900

# VII

# Matunda ya kumtafakari Mungu zaidi katika maisha yake

## 1. Unyenyekevu kama msingi.

Ungekutana na Padre Jordan kwa mara ya kwanza ungetambua utu wake. Hakuwa kama wengine, alikuwa tofauti.

Alikuwaje? Hiyo ni ngumu kueleza…Kamwe hakujaribu kuwafurahisha watu na hakufanya vitu kwa ajili ya maonyesho ya nje nje tu. Kila mmoja alimfurahia, hata mtu wa hali ya chini kabisa. Muungano wake na Mungu ulionekana kwa njia ya utu wake. Hiyo ilimfanya awe kama mtoto, kidogo, yaani hakusumbuka. Padre Paschalis anashuhudia: "Ninakumbuka kwamba Padre Jordan daima aliishi kwa kujua wazi kwamba Mungu alikuwa pamoja naye katika maisha yake. Hakuigiza; Mungu alitenda kazi pamoja naye na katika yeye."[236] Kwa hali ya kawaida,

[236] Fr.Paschalis Schmid, Summarium, & 1054, p.235

alikuwa ni rafiki, mwenye furaha na tabia ya kuwa wazi. Alikuwa daima tayari kwa vitendo. Hakujiachia kubanwa na mawazo yake. Angeshirikisha mawazo yake kwa vionjo vikubwa, lakini alisikitika sababu wengine hawakupokea kwa namna moja. Mara moja alilalamika: " *Ni kama vile mtoto mdogo alikuja mbio kutangaza habari njema na kupata ndoo ya maji baridi kichwani mwake.*"[237]

Wenzake wa kwanza walishuhudia: "Alikuwa na kiasi cha kushangaza. Alipenda migongano" "Alikuwa na moyo ulio wazi na bila ugumu; hakuna kilichofichwa katika mazungumzo yake au katika uwepo wake. Kujifanya na kudanganya hakukujulikana kwake, utu wake wote ulijaa ukweli"[238] Padre Cajetan Oswald anaandika: Mwanzilishi wetu alikuwa 'etwas Ganzes' (kitu kizima)"[239] au kama Padre Pancratius Pfeiffer alivyosema baadaye: "mwisraeli halisi ambaye hana hila ndani yake."[240]



Kwa Padre Jordan, unyenyekevu ulikuwa, ni tabia yake ya kumtumainia Mungu, kutambua kuwa uwepo wetu wote ni zawadi ya Mungu. Zaidi ya tabia yake ya uaminifu, alijua kuwa kila kitu alicho nacho na alichopata ilikuwa ni shukrani kwa Mungu.Akijiongoza mwenyewe kwa Mungu na kwa ufahamu, mwelekeo mwingine wowote ulianguka na yote aliyoyaweza yaliimarishwa. Hivyo Padre Jordan alijua kuwa alipendwa na Mungu bila mipaka, na alijiachia kuvutwa kwenye nafasi ya upendo wa Mungu, ambao hakuweza kujua sawasawa asili yake. Aliona njia kuelekea kwa Mungu kutokana na hisia za udhaifu wake mwenyewe. Alijifunza kukubali makosa yake na alijua kuwa alipendwa

[237] Fr.Pancratius Pfeiffer, Salvatorianer-Chronik, 1918, 180

[238] AS II, no. 138 ya mapadre Ogerius Bartsch, Heribert Winkler, Dunstan Wimmer na Simeon Heimann

[239] Barua toka C.Osswald ya Octoba 1962, APS, I, 110

[240] Yn. 1:47

na Mungu, licha ya udhaifu wake. Kwa kukubali makosa yake, aliweza kuyarekebisha.

Kwa kweli, mmoja anweza kurekebisha tu kile, ambacho amekipokea kwa undani. Asingeweza kujivuna juu ya wema anaotenda ambao ulifikiriwa kuwa ni zawadi toka kwa Mungu. Alijaribu kuona kila kitu kwa njia ya macho ya Mungu na kumfurahisha Mungu tu. Katika chaguo lake la uchungaji hakuruhusu kuongozwa na hisia za kibinadamu za msingi wa mafanikio kuwa utajiri.Kwa mfano Mkoa wa Assam haukutakiwa na Shirika jingine lolote, lakini kwa Padre Jordan haikuwapo sababu ya kuacha nafasi hiyo. Madhabahu ya Maria, Noto na Narni, kulikuwa na shida na hakukuwa na matumaini ya baadaye; alizipokea, hata hivyo, na hakutegemea kuziacha sehemu hizo. Upole wake ulikuwa aina ya unyofu bila maana mbili.Hivyo, ilikuwa vigumu kujadili mradi wowote pamoja naye.Daima ni vigumu kwa mmoja asiye Mtakatifu kuacha kila kitu na kufikiria mapenzi ya Mungu tu.



Padre Jordan alitegemea kwamba wafuasi wake wangetimiza wajibu wao katika dunia kwa upole kama wake. Aliuelezea kama "Unyenyekevu" Hakuwa na maelezo mengi au magumu juu ya unyenyekevu. Daima alirudia yale yale na aliongea kwa uhakika kiasi kwamba mmoja angeelewa kuwa alikuwa amezama kabisa katika mawazo yake. *Hatuwezi kufanya lolote bila unyenyekevu…Kwa hiyo, kweli kama tukitaka kufaulu katika mambo makubwa kwa ajili ya wokovu wetu na kwaajili ya ndugu zetu ni lazima tuweke msingi imara wa unyenyekevu. Kwa kweli, kadiri tunavyotaka kunyanyua juu zaidi jengo la wokovu wetu na wa wengine, ndivyo tunavyolazimika kuchimba msingi chini zaidi. Bila unyenyekevu kazi zetu zitakuwa ni bure; bila msingi yote tunayokamilisha yanaweza kuanguka kirahisi…Mnajua kwamba kama mabonde yanavyonyonya mvua, ndivyo mnyenyekevu anavyonyonya neema; lakini hakuna maji yanayojikusanya milimani.*[241] *Kadiri*

[241] Chap. 05.02.97, DSS XXIII, 110

*jengo letu la kujitakatifuza linavyokuwa kubwa, ndivyo kina kikubwa cha upole kinahitajika…Tunawezaje kujihesabu kwa Mungu kama hatuna unyenyekevu?*[242]

*Ukosefu wa unyenyekevu ni hatari kubwa kwa wito wenu mtakatifu! Hakuna anayepoteza wito wake sababu ya kukosa masomo au kukosa vipaji, lakini kwa kukosa unyenyekevu tu! Kama elimu haitawaliwi na unyenyekevu matatizo yatatokea…Kwanza, unyenyekevu. Kwanza, fadhila! Elimu inakuja yenyewe. Muwe na uhakika na hilo.*[243]

Mwanzilishi aliwapenda sana waseminari na wanovisi. Waliweza kuingia chumbani kwake bila hofu na mara nyingi walisubiri pamoja mlangoni kwake.[244] Padre Athanasius Krachan anatuambia:" Kama vijana waseminari, mara nyingi tulienda kumwona kumwomba ushauri na daima alijua namna ya kutusaidia kama baba na kwa utaalamu."[245] Mwanzilishi alichukulia ujio huo kwa namna ya pekee. Mwishoni mara nyingi alitualika kuja tena kwa maneno yaleyale: "*Kwa nini hamji mara nyingi zaidi*?"[246]



Mtu asiye na makuu anajua ameungana na Mungu. Amejiachia achukuliwe na mawimbi ya upendo wa Mungu kwa ajili ya watu. Padre Jordan alijifunza kumwangalia mtu kama Mungu anavyomwangalia, na kumpenda kama Mungu anavyompenda. Halafu anaweza kujitolea kabisa kwa Mungu ili ajiweke huru kwa furaha ya watu wenzake.

Katika uhusiano wake na Mungu, Padre Jordan alijua kuwa mtu, kwa asili, ni kiumbe maskini ambaye lazima amwombe Mungu kila kitu. Jibu letu la kwanza kwa fundisho

[242] Chap. 09.06.1899, DSS XXIII, 321
[243] Chap. 25.09.1896, DSS XXIII, 72
[244] Fr. Sixtus Kraisser, *Summarium*, & 692, p. 152
[245] Fr. Athanasius Krachan, *Summarium*, & 777 p. 170
[246] Fr. Apollinaris Thoma, *Summarium*, &692, p. 152

hilo lingekuwa:"Basi mtu ni maskini hivyo, mdogo na hawezi kujitegemea?"Lakini tukitaka kufikiri zaidi juu ya fundisho hili, linazungumzia pia juu ya ukubwa wa utu wa mtu. Tunaweza kuishi kwa njia ya Mungu.Tukiweza kuishi wazi kwa njia ya Mungu ni umaskini haswa, lakini pia ni uwezo wa hali ya juu. Huo ni uhuru wetu. Kinyume cha dhambi sio fadhila bali ni neema. Zaidi ya yote, nguvu ya Mungu inafikia mwisho katika udhaifu wa binadamu. Padre Jordan aliweza kupokea udhaifu wake kwa kujua kabisa: "*Mimi ni maskini mdhambi tu*",[247] akijua kwamba angeishi kwa neema za Mungu.

Unyenyekevu haumfanyi mtu awe mdogo, bali ni kutambua na kupokea udhaifu katika kutumaini kwamba Mungu anakutana nami katika kushindwa kwangu. Hivyo Padre Jordan alipata amani ya kweli na unyenyekevu. Alikubali kutoweza kwake na udhaifu katika ukweli kwamba Mungu alimpenda kiasi hiki na kwamba angeweza kushiriki katika nguvu zake



## 2 Kumtumainia Mungu kama Mwamba

Mmoja akizama katika upendo wa Mungu, upendo huo kwanza huleta umoja wa utashi. Huyo anasogezwa na Mungu kama peni katika mikono ya mwandishi. Uhakika wa binadamu unapoteza rangi kiasi kwamba tunaweza kushiriki uwezo wa Mungu.*Tukitaka kukamilisha mambo makubwa, basi ni lazima pia tuwe na imani kubwa. Udhaifu wa binadamu ni mkubwa hivyo kwamba hatuwezi lolote bila neema ya Mungu,tukitengwa na msaada wa Mungu,tukiwa na imani haba au bila imani,halafu tutakuwa viumbe maskini mno,sisi ambao hatuwezi hata kutamka jina la Yesu bila neema ya Mungu?*

[247] Fr. Paulus Pabst, AS II, no. 144

*Halafu ni kwa kiasi kidogo sana tutaweza kukamilisha mambo makubwa kwa utukufu wake*![248] Ndiyo maana Padre Jordan kamwe hakupenda kutengwa kutoka kwenye mapenzi ya Mungu.Mapenzi ya Mungu yalikuwa na maana zaidi kuliko maisha yake. Ndiyo maana daima alikuwa anasali: "*Bwana unioneshe mapenzi yako", au:" Sema Bwana mtumishi wako anasikia; Bwana, unataka nifanye nini?"* Alipotaka kufanya uamuzi wa muhimu, alikuwa akisema*: "Kama ningejua mapenzi yaMungu tu."* Kimsingi, kumtumainia Mungu ina maana ya kuishi katika muungano na Mungu kwa undani zaidi. Mara nyingi sana tunashangazwa na haya katika kalenda yake: *Ee Bwana, unisaidie, unionyeshe njia!Bila Wewe siwezi kufanya lolote.Ninatumaini mambo yote kutoka kwako. Katika Wewe Ee Bwana, nimetumaini, sitaaibika milele.*[249]



*Bwana Yesu Kristo,mimi nipo,nitume kufanya kazi yako! Mapenzi yako yatimizwe! Sema mtumishi wako anasikiliza! Nifanyie unavyopenda mimi ambaye umenijaribu kupita kiasi! Bwana,ifanyike kadiri ya mapenzi yako. Sema, Bwana,Ee Bwana sema!*[250] Kadiri alivyopata ugumu au masumbuko, ndivyo alivyozidi kuomba msaada wa Mungu: *Fanya kazi, teseka, vumilia, Sali, tumaini katika Mungu, fanya yote-yote- yote kwaajili Yake! Jinsi alivyo mwema kwako. Kama ungeelewa hili zaidi!*[251] *Ishi tumaini hili kwamba Shirika lenyewe litakuwa na nguvu zote, na hakuna nguvu za jehena, hakuna nguvu za kidunia zitakazoweza kulishinda…Kama ukitumaini akili zako mwenyewe tu, wakati ujao utakufundisha tofauti…Msaada wetu watoka juu!*[252] *Mtu anayeongoza hatua zake kulingana na mahesabu ya busara ya kibinadamu tu hataweza kamwe kujenga kwa msaada usio wa kawaida wa mbinguni, hataweza kamwe kukamilisha*

[248] Chap.15.06.1894, DSS XXIII, 32
[249] D II / 2
[250] D I / 146
[251] D II / 59
[252] Chap.27.04.1894, DSS XXIII, 25-26

*mambo makubwa.*[253] *Kwa kuwa amenitumainia, nitamweka huru. Nitamlinda kwa kuwa amelijua jina langu.* (zab.90)[254]

Padre Jordan daima alimtumainia Mungu, na matumaini hayo kamwe hayakumwaibisha. Padre Dominicus Daunderer anasema: "Matumaini ya Padre Jordan yalikuwa makubwa hivyo, kwamba, kuyafikiria kwa karibu, tungeyafikiria kama ni ya kishupavu bila hadhari na ya kijinga. Mimi mwenyewe nimeshuhudia namna matumaini haya katika Mungu yalivyozawadiwa mara nyingi kwa namna isiyo ya kawaida. Siku moja, alipata 30.000 marks kutoka mfadhili mmoja wa Ujerumani, mara nyingine 15.000 marks, na mara nyingi zaidi hata kiasi kikubwa zaidi, kinafika wakati Shirika lilipokuwa na matatizo makubwa zaidi."[255]

Siku ya kuanzisha Shirika Padre Jordan hakuwa na fedha**.** Lakini PadreVon Leonhardi, mmoja kati ya wawili ambao walipenda kuanzisha Shirika pamoja naye, aliahidi kumpa kiasi kikubwa cha dhahabu kwa ajili ya kuanza uchapishaji. Lakini, akiwa njiani kwenda Roma, huko Florence, dhahabu yake iliibiwa.[256] Hivyo uanzishaji wa Shirika ulilala katika matumaini yake kwa Mungu tu.Licha ya upinzani, aliweza kuanzisha nyumba ya Watawa 24 katika nchi 12 tofauti. Kwa miaka, kwa shida aliweza kuwatunza waseminari 200 katika nyumba Mama. Ilikuwepo sababu zaidiya kuiita Nyumba Mama "Collegium de Divina Providentia." Kwa miaka, alikuwa anaishi, akitishiwa na ukata. Mawazo ya kibiashara hayakumwingia, sababu kitu muhimu zaidi kilikosekana: Aliamini Msaada wa Mungu! Wakati Padre wa kwanza alipopelekwa Hamont Ubelgiji kuanzisha nyumba



[253] D I / 200
[254] D I / 162
[255] Fr.Dominicus Daunderer, Summarium,& 585, P.131 na pia Barua ya Fr. Jordan kwa Bruda Amilian Rempel ya 21.09.1913, DSS X, no.1144
[256] *Die Salvatorianer*, Vienna, 1931,10

ya Watawa, alimuuliza Mwanzilishi wapi angepata fedha. Jibu la mwanzishi lilikuwa: "*Mungu ni mwema na tajiri, atatusaidia ikiwa tunatimiza wajibu wetu.*"[257]

Jibu hili la Mwanzilishi halikuwa kama namna ya dawa ya kutuliza. Alimaanisha: Ni lazima ufanye kama hivi. *Ndiyo, kila kitu linategemea Mungu, lakini fanya kama kila kitu kinakutegemea wewe!*[258] Alipokuwa mseminari Padre Bonaventura Schweizer alimsikia akisema: "*Ukiwa na matumaini makubwa, unaweza ukaonja uwepo wa Mungu kwa karibu na kwa njia hii, unapata uhusiano unaoonekana na Mungu. Angalia uzuri na nguvu ya Bwana Mungu ilivyo. Nimenunuaje nyumba Mama na chuo kule Tivoli? Sikumbuki kama tulikuwa na hata marks 100 mkononi. Kwa sasa, tumeshalipa kabisa kwa Tivoli, na kuhusu nyumba Mama, bado kuna kiasi kikubwa ambapo tunaweza kulipa deni lote bila shida…Muwe na matumaini makubwa kwa Mungu.*"[259]



Katika maisha ya Padre Jordan, Mungu alionyesha kuwa yupo na kwamba ni bora zaidi kumtumainia Mungu kuliko mwanadamu. Mwaka 1883 alikwenda Ujerumani kumwona rafiki bila raha, sababu alimdai marks 4500 na kwamba alitakiwa kulipa bila kuchelewa. Akiongozwa na matumaini, alikwenda Wurzburg bila lengo. Mara moja pale, aliadhimisha Ekaristi asubuhi na alimwomba Maria: "*Maria lazima unisaidie*." Baada ya Misa alipatwa na wazo la kumtembelea Padre aliyejulikana sana. Aliongea wazi kabisa na mtu huyu kuhusu matatizo yake ya kifedha. Alishangaa kusikia Padre akimwambia kwamba mtu fulani alikuja kumwona siku chache kabla na alimpatia marks 4500 "kwa jambo jema". Mchana alisoma katika kitabu chake cha sala: "Angalia, Maria ni tumaini letu. Tunamkimbilia yeye

257 Fr. Fulgentius Moonen kwa mwandishi
258 Chap.03.12.1897, DSS XXIII, 153
259 AS II, no. 30

tunapokuwa na shida, ili kwamba atuweke huru. Amekuja kutusaidia."[260]

Katika maelezo yake, tunasoma:

1894: *Watu wawili waliniletea 2000 marks, za kutosha kulipa madeni yetu.*

1896,Desemba 25:*Bwana mwema alisaidia Assam kwa namna ya pekee kabisa.*

1897,August 14*: Katika kuishiwa fedha kusiko kwa kawaida, Mama yetu ametusaidia* 4000 *marks*.[261]

Wakati wa mkutano wa Julai 3,1896, alisema: *Mungu ana vyanzo vya kutosha na daima anaonyesha hii! Mfano mmoja: hatukuwa na fedha kwa safari hii ya Marekani na leo marks elfu tatu zimefika kutoka Ujerumani toka kwa mtu ambaye hakutajwa, "Kwa ajili ya safari"!*[262]



Padre Jordan anaandika kwa Bruda Emilian Rempel, ndugu mmendikanti,(Mtawa) kumtia moyo: *Mwezi uliopita, nilimwomba mtu mmoja anitengenezee "Deo Gratias"rozari yenye vifungo 33, kwa kumbukumbu ya maka 33 ya Yesu; baadaye kidogo, Bwana mwema aliniletea 33.000 marks.*[263]

Mwaka 1897, wakati Mwanzilishi alipoumwa sana, watoaji walikimbia kudai fedha zisizowadia kwenye akaunti. Bruda mlinda mlango alimtoa muuzaji wa nyama akisema: "Kumtumainia Mungu". Mchinjaji alijibu: "Matumaini, matumaini, siwezi kununua Maksai kwa matumaini". [264]

---

[260] *Apostelkalender*, 1920; Fr. Otto Hopfenmuller, DSS IV, 146-147

[261] *Annales Soc.Cath.Instructivae,* 1894

[262] Chap.03.06.1896, DSS XXIII, 69

[263] DSS X, no.1144

[264] Br.Giuseppe Capparella kwa mwandishi

Mara moja mambo yaliyohitajika yalikuwa mengi na kwamba ukata ulikuwa haukwepeki. Kama alivyofanya mara nyingi katika hali hizo, Padre Jordan alikwenda kwenye sanamu ya Mama wa huzuni na alibaki pale akisali kwa masaa kadhaa. Ghafla, alisimama na alipita kwenye veranda kana kwamba anamngojea mtu fulani.

Kengele ziligongwa na alifungua mlango bila kuchelewa, kitu ambacho alikuwa hafanyi mara nyingi. Mbele yake alisimama mwakilishi wa Shirika la Trinitarian, amemkabidhi Padre Jordan bahasha. Alifungua bahasha na akakuta 33.000 marks, kiasi hicho hicho alichokihitaji. Alipotaka kumshukuru yule wa Shirika la Trinitarian akageuka na kuona kuwa alishaondoka. Maombi yamekuja bila matazamio.[265] Katika kile kilichoitwa wosia wake, anaandika maneno haya kama ushahidi tosha: *Ni katika Mungu tu muweke Imani na matumaini yenu. Atawalinda kwa nguvu za ushindi wake. Ole wenu kama mkiweka matumaini yenu kwa watu au mali za duniani.* Na: *Mfikirie matumaini katika mapaji ya Mungu urithi wa daima. Itawawezesha kama Mama mpendwa,"*[266] Charles Peguy anasema: "Imani ninayopenda zaidi, Mungu anasema, ni kumtumainia."



## *3.* Juhudi ya pekee kwa ajili ya Roho.

Alama kubwa ya ki-karama ya utu wa Mwanzilishi ni juhudi yake kwa ajili ya roho. Moja kati ya sala zake, anajiita "mtu wa tamaa".[267] Alikuwa akifikiria kitakatifu daima; alikusanya kila kitu katika upendo wake wa utume. Hakuna nchi, Taifa, wala namna iliyoachwa. Alitaka kutumia namna zote ambazo Mungu alimwangazia, ili asifikie mwisho wa mipango yake.

[265] Fr.Bonaventura Schweizer, AS II, 38; Fr.Joseph Klimke, Summarium, & 1478, P.337; Fr.Ogenius Bartsch, AS II, no. 153

[266] APS, B 105

[267] D II / 18

Padre Konrad Hansknecht anasema: “Mwanzilishi alikuwa mtu mkatili. Alipokuja Drognens, nilikuwa nimekata tamaa kila mara na sikujua nilichokuwa nafanya, nilitawaliwa na tabia yake ya kudai kwa nguvu. Tulikuwa tukifikiri juu ya mambo mengi pamoja naye, alipendekeza miradi na pia kulikuwa na matatizo mengi. Alikuwa mkali lakini bila kulazimisha.”[268]

Roho Mtakatifu akianzisha makao yake katika moyo wa mtu, hatuwezi kutofautisha kati ya upendo wa Mungu na upendo wa mwenzake. “Upendo wa Mungu unamiminwa mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu.”[269] Upendo huo huo unatudai sisi na Mungu na ndugu zetu. Padre Jordan hakuzungumza na Mungu bila kuzungumzia wokovu wa watu, kama alivyoongea na watu hakuongea nao bila kuzungumza juu ya upendo wa Mungu.

Kutokana na muungano wake na Mwokozi, aliona ulimwengu na watu kwa namna tofauti. Kwa Mwanzilishi, wito wa kichungaji ulikuwa ni kushiriki katika umwilisho wa Yesu, Mwokozi wa dunia. Alikuwa tayari kutoa maisha yake kwa watu wote, sababu Kristo pia alimwaga damu yake kwa ajili ya watu wote. Katika mtu, aliona mwanga wa utukufu wa Mungu, picha ya Kristo mteseka. Katika moja ya mazungumzo yake, alirudia kwa kusema maneno ya Mt.Catherine wa Siena “ *Kama yeyote angeona uzuri wa roho moja, angependa kufa mara mia moja kila siku kuiokoa.”*[270]

Katika sheria zake za mwanzo aliandika: *Roho inayowahamasisha ni upendo wa Mungu na wa jirani… upendo kama huo hufanana na moto uwakao,ni sadaka kubwa ya kitume kwamba wanatoa kila kitu kwa ajili ya wokovu wa watu*.[271]



---

[268] Barua ya Fr.Donatus Blonde kwa mwandishi, 05.12.1956

[269] Rm.5:5

[270] D I / 169, angalia pia mikutano ya 11.05.1894, 08.04.1899, 29.04.18948, 06.05.1898,27.01.1899- DSS XXIII.

[271] DSS I, 21

Mwanzishi anapenda kuongea kuhusu moto, kwani moto pia unajumlisha kila kitu na hauondoi chochote. Anasali: *Ee Bwana, kwamba daima niweze kuwaka kwa bidii kwa ajili ya upendo wako na kuwaangazia wote. Naomba niwe moto unaowaka, Ee Mungu, na tochi inayomulika!*[272] Alitaka wafuasi wake watawaliwe na moto kama huo. *Ee Mungu Mwenyezi, peleka mafuriko ya moto mtakatifu juu ya watu, hasa kwa wafuasi wangu, uendelee kuwaka katika mioyo yao wakati wote waishipo mpaka mwisho wa nyakati, kwa utukufu wa Mungu na furaha ya watu. Uwaongeze kama nyota za angani.*[273]

Juhudi ya kuokoa roho daima ni tunda la sala. Sio sisi tunaompenda Mungu; Alitupenda kwanza. Juhudi hii ya kuwaleta watu wote kwa Mungu pia ni chanzo cha wito wake kama Mwanzilishi. *Ee Bwana, Ee Baba, Ee Mungu na muumbaji, kwanini hao wanaoishi chini ya giza kuu la upagani wasijue uzuri na huruma yako…Yesu Kristo, unipokee kama chombo chako na unifunue kama upendavyo. Angalia, kwa msaada wa neema Yako, niko tayari kufa kwa ajili yako.*[274] Alijisikia sio upendo wa Kristo tu, lakini kwa kila mtu ambaye Kristo alikufa kwaajili yake. Anaandika katika kalenda yake: *Ikiwa kuna mtu mmoja duniani ambaye hamjui Mungu na hampendiYeye zaidi ya vitu vyote, usithubutu kujipa muda wa mapumziko. Ikiwa Mungu hatukuzwi kila mahali, usithubutu kujipa muda wa mapumziko. Ikiwa Malkia wa mbingu na dunia hasifiwi kila mahali, usithubutu kujipa muda wa mapumziko. Hakuna sadaka, wala msalaba, wala ukiwa, wala majaribu, wala vishawishi,oh! Hakika hakuna kitakachokuwa kigumu kwako kwa msaada wa neema ya Mungu.Naweza kufanya mambo yote katika Yeye anayenipa nguvu. Msiruhusu usaliti, wala ukosefu wa uaminifu, wala ubaridi na matumizi mabaya vipunguze juhudi*



[272] D III / 20
[273] APS G, 7.5 (vitini vya Fr. Jordan); DSS XXI, 5
[274] D I / 12

*yenu! Lakini kila kitu kwa njia Yake, pamoja Naye, na kwa ajili Yake*.[275]

Alitaka kuwashirikisha wafuasi wake juhudi hizi za kitume. Alitaka wanachama wote wa Shirika kushiriki katika wazo lake la kokoa roho. Kwenye meza yake, kulikuwa na tufe dogo, na wanafunzi walipokuja kumwona, aliwaonesha nchi ambazo zinasubiri kupata ujumbe wa Injili.Kwenye veranda mbele ya chumba chake, ambapo mabruda walikuwa wakisubiri daima, kulikuwa na ramani pamoja na habari za dini zinazoonyeshwa kwa hesabu. Aliposoma barua kutoka kwa wamisionari, uso wa Mwanzilishi ulijawa na uchangamfu kiasi kwamba kila mmoja angeona furaha ya ndani inayoangaza uso wake.[276] Kuwapeleka wamisionari wapya ilikuwa sehemu ya juu ya maisha yake, kwake ilikuwa ni furaha kubwa kabisa. Mwanzilishi alifurahi kwamba wengi kati ya waseminari walikuja kumwona kila wiki ya pili au ya tatu.



Daima alizungumzia juu ya shughuli zake za kitume.Alisema kwa Padre kijana Bonaventura Schweizer: *Ulimwengu una njaa ya mapadre. Tungeweza kutumia bila kuchelewa mapadre elfu moja.*[277] Kwa Padre Athanasius Krachan, analalamika: *Kama ningekuwa na mbinu tu na watu wa kusaidia kila mahali.*[278] Fr. Elisaus Gabelseder anashuhudia: “Daima nilikuwa nafikiri kwamba mheshimiwa Mwanzilishi wetu asingeweza kusali kwa njia yoyote kuliko njia ya kitume alijiingiza ndani kabisa katika kazi yake. Maneno yake yote yalionekana kupumua juhudi kwa ajili ya roho.”[279]

---

[275] D II / I

[276] Fr.Timotheus Moser, AS II, no.16

[277] AS II, no.16

[278] AS II, no.16

[279] AS II, no.9

Wajibu wa kimisionari katika mkoa wa Assam ulikuwa mzigo mkubwa mabegani mwake. Kuhusu hili, alisema, wakati wa mkutano: *Hata hivyo tufikirie mahitaji ya ulimwengu. Katika eneo la Assam, ambalo lilikabidhiwa kwetu yenye idadi ya watu zaidi ya 7,000,000 kila saa watu 30-40 wanakufa bila ubatizo…*[280]

Akifungua mkutano mkuu wa Shirika 1902, alisema: *Mwisho, watoto wenye thamani kubwa, kumbukeni kwamba roho ya Kristo ni roho kumbakumba, siyo ya sehemu moja tu. Kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili ya wote, Shirika letu pia lina tabia kumbakumba.*[281] *Katika sura nyingine anasema: Ninaamini- moyo wangu daima unaniambia- kwamba Shirika letu, kama mkikubaliana na mapenzi ya Mungu litafaulu kupeleka roho nyingi mbinguni.*[282]



Inashangaza kwamba Mwanzilishi wetu, aliyeshughulika sana juu ya wokovu wa roho, mara nyingi hakufanya kazi muhimu za wongofu na kutunza roho..[283] Kutoka 1880-1882, wakati mwingine aliadhimisha Ekaristi katika Kanisa la Mt.Brigitta, na Maria, wakati mwingine mpaka wakati wa sala ya jioni. Hakufanya kazi za Parokia kamwe, wala kwa vijana, hakutembelea nyumbani kwa watu; tunavyojua hakusikiliza kitubio lakini yote sawa alikuwa mtume kwa njia ya juhudi yake ya kuokoa roho, aliyopewa kutoka ndani na kweli ilimmeza. Juu ya kitanda alichofia, alisema: “Oh kama tu ningeongoa ulimwengu wote.”[284]

Mwanzilishi alijisikia kuwa mtumishi ambaye huwaita watu wote kwa mapambano matakatifu. Daima anajisikia

---

[280] Chap.11.03.1898, DSS XXIII, 198

[281] Mafundisho ya.06.10.1902, DSS XXIII, 471

[282] Chap.08.04.1898, DSS XXIII, 207

[283] Fr.Augustinus Borchet, *Summarium* &262; Fr.Guerricus Burger, *Summarium II* & 286

[284] DSS XXI, 19

nabii wa Armagddon; anafikiri kwamba ufunuo wa nyakati za mwisho umekaribia. Anaandika: *Pigeni kelele kwa nguvu kama tarumbeta kwenye miji yote ya dunia, ili kila kiumbe kisikie! Rukeni kama mwewe na kama malaika na kwa sauti kubwa viiteni viumbe vyote kwenye mapambano matakatifu kupigana kwaajili ya kamanda mkuu pamoja na askari waliopangwa katika mapigano.*

*Waamsheni na kuwaita waliolala! Wasukumeni wazembe! Pigenikelele, pigeni kelele kama malaika ambao, pamoja na tarumbeta, huwaita wanaoishi na waliokufa kwenye hukumu ya mwisho! Msiogope, kwani Mimi, Bwana mwenyezi, nipo pamoja nanyi na nitakuwa msaidizi wenu mwenye nguvu.*[285]

## 4. Upendo wake kwa Msalaba.

Wakati, wa Jumapili ya Mateso 1883, Padre Jordan alichagua jina “Francis Maria wa Msalaba” kama jina lake la kitawa, ilikuwa ni kutokana na mwanga wake kiimani, kwa kujua kwamba angetimiza utume wake tu kama Mwanzilishi katika maana kwamba ameingia kwenye utume wa Yesu ambaye msalaba ni maelezo ya juu ya upendo wake na zawadi yake. Kulingana na alivyoamini, aliandika kwenye kalenda: *Iwe mbali nami kwa utukufu isipokuwa katika msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo.*[286]



Utukufu katika msalaba wa Bwana Yesu ulikuwa, kwake, kutaka kujiweka mbali kutoka shughuli zake mwenyewe, kwa utashi wake kusudi aingie “katika hali ya akili ilikuwa katika Kristo Yesu.”[287] Akiendeshwa na upendo wa Kristo uliomwagwa katika moyo wake, Roho ya Mungu ilichukua utawala wa utu wake kiasi kwamba Yesu mwenyewe aliishi nia zake za wokovu katika yeye. Katika sheria yake ya kwanza

[285] D I / 190
[286] D I / 71
[287] Wafil.2:5

anaandika: *Roho inayohamasisha wanachama ni upendo wa Mungu na wa jirani; upendo huo ni kama moto ambao juhudi kubwa za kitume kama hizi hutokea kwamba hutoa kila kitu, hata wenyewe hata kumwaga damu yao kama Mungu akipenda.*[288]

Padre Jordan alipenda msalaba kwa sababu ni asili ya wokovu. Ni kwa njia ya msalaba wokovu umekuja ulimwenguni. Anayetaka kuleta wokovu kwa watu lazima aupende msalaba. Kama fikara ya jina lake la kitawa, anaandika kwenye kalenda yake:

Yohane Maria Francis wa msalaba, kwa hiyo:

*Msalaba ni maisha yako,*
*Msalaba ni wokovu wako,*
*Msalaba ni taji lako,*
*Msalaba ni utukufu wako,*
*Msalaba ni matumaini yako,*
*Msalaba ni ngao yako,*
*Msalaba ni ulinzi wako,*
*Msalaba ni sehemu yako,*
*Msalaba ni furaha yako,*
Kwani inakuwa kwangu kutukuza si chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo![289]



Katika ukurasa mwingine anaandika:

*Salamu Ewe msalaba!*
*Salamu Ewe msalaba tumaini letu tu.*
*Tunayo fahari kutukuza msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao una wokovu, maisha na ufufuko.Ishara ya msalaba itakuwa mbinguni, wakati Bwana atakapokuja kuhukumu. Tazama msalaba wa Bwana, rukeni, maadui wa ushindani, simba wa kabila la Yuda anashinda.*

[288] DSS I, 21
[289] D I / 179

Maneno haya ya kibiblia yanakuja moja kwa moja toka moyoni mwake. Maneno ambayo upendo wa Kristo na mateso ya watu hutokea. Kwake, msalaba ni tukio la ufufuko; furaha hutokea kwenye huzuni, maisha yanakuja kuwapo nje ya kifo, udhaifu ni marekebisho katika nguvu.

Anaandika kwa Padre Bonaventura Luthen: *Tuwe macho katika ukweli kwamba ni utume wetu kumfuata Yesu maskini, aliyedharauliwa, aliyeteswa. Oh, hiyo ingeandikwa wazi ndani ya mioyo yetu. Halafu baraka za Mungu zitashuka chini.*[290]

Alisema kwa Masista: *Kila kitu tunachofanya kwa ajili ya wokovu wa roho zisizokufa lazima kiwe na msingi katika Kristo msulubiwa…Msalaba pekee hutupa wokovu na amani. Kadiri unavyopata mateso na dharau, ndivyo utakavyoweza kukamilisha zaidi…Yeyote anayeogopa mateso hawezi kuwa mtume.*[291] *Asiyependa Kalvari hafai.*[292]



Kwa njia ya upendo, aliungana sana na msalaba, na kwamba aliandika kwenye kalenda yake: *Ee Msalaba, Ee Msalaba mtamu! Ee Msalaba ambao nataka kuupenda na kwa gharama kubwa na juhudi kwa ajili ya Yesu! Ee Msalaba wenye kupendeza! Ee Msalaba, nguvu kubwa! Hivyo kwamba ningeweza kweli kujua namna ya kuteseka pamoja na Mpendwa wangu, Yesu, Mungu wangu! Ee mtamaniwa na Manna tamu kwa hao wanaojua! Ah, kuteseka kwa ajili ya Kristo na pamoja na Kristo*![293]

*Zaidi ananukuu: "kati ya zawadi zote za ndani ambazo Roho Mtakatifu anazimimina katika roho zetu iliyo kubwa zaidi ni zawadi ya kujishinda na kuteseka kwa furaha kwa ajili ya upendo kwa Mungu." (Mt.Francis wa Assisi).*[294]

290 DSS X, no.185
291 Hotuba kwa Masista, 08.02.1904, DSS XXIII, 479
292 Chap.24.02.1899, DSS XXIII, 282
293 D I / 208
294 D IV / 10

Katika ofisi kuu ya kutunza kumbukumbu, kuna mpango wa mkutano maalum ambao Mwanzilishi alitaka kuuingiza katika katiba, lakini hilo lilikataliwa na ofisi inayoshughulika na maisha ya kitawa Roma kwa sababu ilikuwa na maandishi mengi toka Maandiko Matakatifu.

Nini wanachama wanalazimika kujua kuhusu mateso ya Kristo!

Wanachama ni lazima wajue kwamba wanachangia sana wokovu wa roho kwa mateso mengi zaidi kuliko shughuli za nje nje tu.Ndiyo maana lazima wajue kwamba wameitwa kuteseka zaidi kwa ajili ya Kristo kuliko kufanya matendo ya nje.

Watajitahidi kuweza kusema pamoja na Paulo, mtume wa watu: Kwani inakuwa kwangu kutukuza si chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa njia yake tumeokolewa na kukombolewa.



Kwamba mateso ya Kristo yawe ngao, isiyopenyeka na inayotisha kwa adui.

*Kwamba wanachama waelewe namna wanavyowezeshwa kama wakijiunganisha na Bwana wetu Yesu Kristo, msulubiwa!*[295]

Maneno haya ni kama agano. Ilikuwa hamu ya Mwanzilishi kwamba tuingie kwa kuongezeka kwenye fumbo lisilo na mipaka la mateso ya Yesu juu ya msalaba. Katika kalenda yake anaandika: *Kwa nini mnaogopa kuchukua msalaba unaoongoza kwenye ufalme? Katika msalaba kuna wokovu; katika msalaba kuna maisha…Katika msalaba kuna utamu wa mbingu. Katika msalaba kuna ukamilifu wa utakatifu. Chukua Msalaba wako, halafu, umfuate Yesu, na utaingia kwenye*

[295] Skizzen fur das Schuldkapittel, APS G

*maisha yasiyo na mwisho. Maisha yote ya Kristo yalikuwa msalaba, ushuhuda.*[296]

*Kazi za Mungu zinasitawi tu katika kivuli cha msalaba*[297]

Padre Jordan, mwenyewe, aliita upendo wa msalaba kuwa dhamira yake aliyoipenda kwenye mahubiri. Kwa kweli, ni alama ya upendo wa Mungu kwetu. Katika mikutano ya kila wiki, alizungumza kwa kurudiarudia na kwa vionjo: *Hata mkiona kuwa mnakamilisha kabisa, kazi hadi kazi, msipoteseka kwa vikubwa, halafu msihesabu, msitegemee chochote!…Kwa njia ya mateso, kwa njia ya uvumilivu wa mateso, mtaziita chini baraka kutoka juu!Mnajua mpendwa Mwokozi aliukomboa ulimwengu kwa njia ya mateso!Tunataka kuchagua njia nyingine? Ni sheria inayojulikana mno: mtume wa kitawa daima anafaulu kulingana na mateso yake!*[298] *Mnajua kwamba mfanyakazi wa kitume anakamilisha zaidi kwa njia ya mateso kuliko nguvu au juhudi. Ndiyo maana Mungu Mwokozi amesema: "Nitamwonyesha namna gani ni lazima ateseke", siyo namna gani ni lazima ahubiri, kiasi gani lazima afanye, au wangapi ni lazima awaongoe, Asiyependa Kalvari hafai.*[299]



## 5. Maisha yake yaliyojaa mateso

Katika maisha yake yote, mwanzishi ameingia zaidi na zaidi katika fumbo la mateso. Yeyote anayesoma maisha ya Mwanzilishi kwa undani atafikia hitimisho hili: mtu huyu atakuwa ameteseka sana. Kukua kwa maisha yake ya ndani hakika yanatokana na afya yake. Padre Pancratius Pfeiffer anaandika: "Kwa ujumla, alifurahia mema, ingawa hakuwa na nguvu sana kiafya."[300]

[296] D I / 189;Kumfuasa Kristo II, 12
[297] D I / 163
[298] Chap.04.10.1898, DSS XXIII, 234-235
[299] Chap.24.02.1899, DSS XXIII, 282
[300] Fr. Pancratius Pfeiffer, P.Jordan, 400

Nafikiri Padre Pancratius alitaka kuficha, kiasi fulani, hali ya kuumwa ya Mwanzilishi. Ushuhuda wa kaka yake, Padre Justinianus Pfeiffer, pengine ni sahihi zaidi: anabainisha kuwa Mwanzilishi alikuwa na afya njema tangu upadrisho wake.[301] Mwanzilishi hazungumzii juu ya kutofurahi kwake kiafya. Daima alipata maumivu ya tumbo. Si mengi yaliyoandikwa juu ya mishipa yake ya fahamu, pengine ili isipunguzwe hadhi ya utu wake. Mishipa yake ya fahamu ilikuwa ni chanzo kikubwa cha kukosa kwake raha. Katibu wake, Padre Magnus Wambacher, aliandika tena barua wakati mwingine mara mbili au mara tatu. Uvumilivu ulipomshinda, Mwanzilishi alimwonya: *Uwe mvumilivu, chochote kwa ajili ya upendo wa Mungu*.[302] Kwa sababu ya nervu zake dhaifu, kila kitu kilimshtua moja kwa moja na kwa nguvu, hivyo Padre Bonaventura Luthen angesema: “Hatuwezi kudhani maumivu aliyolazimika kuyapata.”[303]



Haijulikani vizuri Padre Jordan alikufa kwa ugonjwa gani; pengine ni kansa ya tumbo? Kilichomsumbua zaidi siku zake za mwisho kinaonesha kufanana na ugonjwa wa ‘Parkinson’. Kupumua kwa shida, kutetemeka mikono, na ugumu wa kukunja vidole ni baadhi ya dalili ya ugonjwa huo. Mara alipopita miaka 50, mara chache aliadhimisha Misa katika jumuiya, kwasababu wakati wa Komunyo, mikono yake ilikuwa mizito, na vidole vyake vilikuwa vinaganda kiasi kwamba hangeweza kugawa hostia.[304] Ndiyo maana alisali Misa kwenye kikanisa kidogo. Kwake, mahubiri ya sehemu ya Misa na Breviari ilikuwa ni mateso sababu ya alikuwa na mashaka. Hakupenda kusali Breviari peke yake. Ndiyo maana daima alisaidiwa na wenzake.[305] Padre Jozef Bergmiller anasema: “Siku moja, wakati

[301] Fr.Justinianus Pfeiffer, Summarium, & 1131, 256

[302] Fr.Magnus Wambacher, Summarium, I,& 1230-31, 278

[303] Fr.Pancratius Pfeiffer, P.Jordan, 401

[304] Mabruda Giuseppe Capparella na Gabriele Manni kwa mwandishi

[305] Bruda Giuseppe Capparella na Fr.Lucas Klose kwa mwandishi

Mwanzilishi hana na raha sababu ya matatizo ya kifedha, nilimwambia Fr. Damian:Leo utasali Breviari na Mwanzilishi, wewe ni mkimya zaidi.Baadaye Fr.Damian aliniambia kwamba kwanza hakuweza kusali.Mwanzishi alihangaika mpaka kutetemeka na kukosa utulivu.Yeye mwenyewe alimwonea huruma mpaka kutokwa na machozi machoni mwake."[306]

Fr.Ambrosius Suter anaeleza muda aliotumikia chakula cha jioni huko Drognens(CH), wakati Mwanzilishi alipotembelea. Mwanzilishi alishtuka ghafla kwamba alidondosha sinia pamoja na nyama.[307] Mwanzishi hakuweza kuvumilia radi. Hakuweza kukaa chumbani, angetembea kwenye veranda; nywele zake zilisimama na kumetameta.[308]

Jioni alichangamka sana na alifikiri na kupanga kwa juhudi kiasi kwamba hangeweza kusinzia.Asubuhi, hakuchelewa kuamka, ingawa hakuchangamka mpaka baada ya chakula cha asubuhi. Mvutano kaati ya "utashi" na " kutoweza" ilikuwa ni chanzo cha kudumu cha mateso ya ndani kwake.Hivyo tunaweza kusoma kwenye kalenda yake: *Ee Yesu, nateseka kwa majaribu makubwa.Ee Bwana,nionyeshe njia nitakiwayo kutembea.*[309] *Ee Bwana, Mungu Mwenyezi, nimebanwa mno! Angalia, nipo hapa. Angalia damu ya mwanao.*[310] *Au: Mateso makubwa nataabu ambayo yamepungua jioni hii. Mateso ya nje na ya ndani.*[311]



Mmoja aliposema kitu, Mwanzilishi angekasirika na kugoma kwa nguvu hata kabla hajasikia sentensi nzima.

---

[306] AS II, 86
[307] Fr Ambrosius Suter kwa mwandishi
[308] Bruda Giuseppe Capparella kwa mwandishi
[309] D II / 70
[310] D II / 94
[311] D II / 55

Alifikiri kwamba aliwasumbua na kuwatisha alipogoma kwa ghafla mwanzoni. Wakati wa mkutano mkuu wa pili wa Shirika alitoka kwenye chumba cha mkutano katika hali mbaya, akilalamika: “Gemein”yaani sikubali.[312] Mwanzishi angejifunza kukubali udhaifu huu bila kukata tamaa au kufanya upinzani dhidi yao. Pengine inashangaza kidogo, lakini wanachama wengi hawakujali juu ya udhaifu huu wa kibinadamu.

Kwenye mkutano, Padre Jordan alisema juu ya kalisi nne ambazo kila mtume alitakiwa anywe. Ni utume wetu kunywa kalisi aliyokunywa Bwana wetu. Na tutakunywaje?

Kwanza tutapokea toka jehenam, toka kwa wapinzani wa wokovu, toka kwa adui anayetisha…anayetuchukia na kutufuata tunapofanya kazi kuharibu himaya yake na kueneza ufalme wa Yesu Kristo…Lakini kikombe hiki ni moja ya vikombe rahisi kuvumilia.



Kikombe kichungu zaidi hutoka kwa watu wabaya. Hiyo ni sehemu ya pili: kufuatwa na watu wabaya wanaotushambulia kwa sababu tunakumbana na vishawishi vyao.

Kikombe cha tatu mtume anacholazimika kunywa na ambacho ni kichungu zaidi ni kile kilichoandaliwa kwake na watu wema wakati wanaposhindwa kumuelewa, mipango yake na nia zake; wakati, matokeo ya hii, watu huamini kwamba wanafanya kitu kizuri wanapoyapinga hayo. Hicho ni kikombe cha tatu, lakini bado kile kichungu zaidi.

*Cha mwisho, kama Mungu akikupa, ni pale ambapo hata wale waliochaguliwa na Mungu kukusaidia na kukulinda, hata*

[312] DSS XIV II, 819

*wakubwa wa Kanisa, wanapoweka vizuizi katika njia yako. Hiki ni cha nne na kichungu zaidi!*[313]

Kila mmoja alielewa kwamba Padre Jordan alisema katika mkutano huu juu ya uzoefu pamoja na msalaba aliochukua mwenyewe. Alijua uvamizi wa Shetani.Huo ni msalaba wake wa kwanza. Kwenye kalenda yake, anaandika: *Shetani anapenda kuvuruga sala na analeta vizuizi vya kishetani dhidi ya sala ya ndani ya hali ya juu, dhidi ya kazi kubwa kwa ajili ya wokovu wa roho, dhidi ya mawazo, tamaa na jitihada za kuwa mtakatifu, dhidi ya kazi nzuri za toba na kujinyima kwa kila aina*.[314] Katika nafasi ya miaka 25 ya Shirika, anaandika: *Mnajua namna adui alivyoendelea!*[315]

Msalaba wake wa pili ni hofu zake, na hasa kuogopa dhambi. *Sitaki kutenda dhambi* yalikuwa maneno yake aliyotumia daima.Hata alijaribu kuogopa kivuli cha dhambi. mpaka kwenye kitanda chake cha kifo alirudia '*nolo peccare*': Sitaki kutenda dhambi.[316]



Muungamishi wake alimshauri asiende kwenye kitubio bila kumjua muungamishi, sababu ya hofu zake.[317]

Hofu hii ilimwumiza sana sababu ilifanya iwe vigumu kwake kutekeleza wajibu wake wa mwisho kama mkuu wa Shirika. Ndiyo maana Fr.Bonaventura Luthen ilikuwa zawadi ya Mungu kwake. Mwanzishi angeenda chumbani kwake mara nyingi kila siku kuuliza: *Naweza kuwa kimya?* Padre Pancratius Pfeiffer anaandika: "Mmoja lazima awe na nguvu katika fahamu na uvumilivu kumsikiliza kwa ukimya ili kuweza kuondoa mashaka yake" Inaonekana

[313] Chap. 05.05.1899, DSS XXIII, 306-307
[314] D I / 91
[315] DSS X, no.854
[316] DSS XXI, 30
[317] Fr. Conrad Hansknecht, AS II, no. 43

ilikuwa kazi ya kupoteza muda. Lakini Mwanzilishi angesema: *Muwe wavumilivu, Mungu ameruhusu hii.* Padre Bonaventura Luthen alifafanua: Mwanzishi angekwenda mbali zaidi pamoja na tabia yake ya kuwaka na vionjo visivyozuilika katika jambo kubwa”[318]

Kikombe cha tatu kilikuwa wafuasi wake.Waseminari vijana walilaumu juu yake kwa mgeni; wenzake walijadili juu yake na walijaribu kumtoa wakati wa uchaguzi. Wakati wa mkutano mkuu walikuwa na msemo: “Achana na mwanzishi!” Kwenye mkutano mkuu wa 1902 na 1908, wakati wa uchaguzi wa mkuu wa Shirika, alipata kura za lazima tu waliporudia mara ya tatu. Alikuwa anaangalia mapadre vijana wangapi, waliosoma kwa gharama za Shirika walitafuta Askofu wawe mapadre wa jimbo mara tu baada ya kupadirishwa. Aliandika jinsi maumivu yalivyokuwa makali kwake.[319]



Kalisi ya nne iliyomuumiza ni mateso aliyopata chini ya Kanisa. Inaeleweka kabisa! Mateso chini ya Kanisa hayakwepeki, kwa sababu haikuwa na haitakuwa vizuri Kanisa liongozwe na watu kwa ubinadamu. Kanisa ni Kanisa la binadamu, ni Kanisa la wadhambi. Hata watakatifu waliteseka chini ya Kanisa, kama Mt.Francis, Mt.Catherine wa Siena, Mt. Peter Canisius, Newman na Blaise Pascal. Mwanzilishi aliteseka, sababu mtazamo wake kumbakumba haukukubaliana na utaratibu wa kirumi. Alionja ugumu wa viongozi wa Kanisa kwamba ulinyamazisha na kupunguza mtazamo wake wa kiroho. Kuteswa chini ya Kanisa maana yake: Kuteswa chini ya taratibu za Kanisa zenye kutu. Kwa kujaribu na kushindwa alilazimika ajifunze namna ya kutulia katika magomvi na mamlaka ya Kanisa. Juhudi zake za kitume zilifungwa na taratibu za Kanisa.

318 Fr.Pancratius Pfeiffer, P.Jordan, 400-406
319 DSS X, no. 627

Naibu Kardinali wa Jimbo la Roma alimwambia mwaka 1885: "Baba Mtakatifu ameambiwa kuona masingizio juu yako"[320] Sheria ambayo, kulingana na yeye, iliandikwa chini ya mwanga wa Mungu kwa muda imewekwa badala ya sheria ya mtu wa nje. Alipata mkaguzi wa papa aliyeweza kukata mabawa yote ya miradi yake mikubwa kwa miaka ishirini. Ilikatazwa kupokea wanafunzi maskini, kuanzisha nyumba mpya, kujadili mikopo bila ruhusa yake.Hicho kilikuwa kikombe kichungu zaidi kabisa.

Padre Jordan alikunywa kikombe cha mateso bila woga, bila kulaumu,bila kukasirika, kwa sababu alikuwa anaamini kuwa *kazi ya Mungu inasitawi tu katika kivuli cha msalaba.*[321]

Kulingana na mafundisho ya Kanisa, aliidhinisha kwa uhakika, na kwa ukamilifu. 1901, anaandika juu kwenye ukurasa wa kwanza wa kalenda yake: *Nakikubali kinachokubaliwa na Kanisa na ninakataa chochote kinachokataliwa na Kanisa.* Kuhusu sheria zinazohusiana na kufunga, alijaribu kupata ruhusa kwa wanafunzi wake. Kamwe hakuonyesha malipizi makali zaidi kama kuvaa shati la nywele na kulinda usiku, ambavyo ilikuwa ni kawaida kwa siku hizo. Alijua kwamba Kanisa limejengwa juu ya upendo wa Kristo na upendo wa kindugu wa wakristo. Kwenye kalenda yake, ananukuu maneno ya Pius X "*Hatuwezi kujenga Kanisa juu ya mabaki ya upendo*."[322] Alitamani kutoa kila alichonacho kwa ajili ya umoja na upendo.



Mwisho wa maisha yake, aliandika kwenye ukurasa maalum wa kalenda yake aina ya marudio ya imani yake kamili, akifikiri: *Ninaamini kabisa yote ambayo Kanisa Takatifu Katoliki la Roma linaamini na kufundisha kwa imani. Ninataka kuishi na kufa katika imani hii takatifu Katoliki ya Roma.Kama*

[320] DSS XIV, 496

[321] D I / 163

[322] D III / 4

*nimefanya, kusema au kufikiri chochote katika maisha yangu dhidi ya imani, takatifu, Katoliki ya Roma au kama ingetokea kwa njia yoyote ile dhidi yake kwanjia ya hao walio chini yangu, hapa nakirudisha nyuma na kukikataa. Friburg, Uswisi-Januari 5,1916.Padre Francis Maria wa Msalaba Jordan.*[323] Haya ni maneno ya mtu aliyejipatanisha mwenyewe kabisa kwa maisha.

## 6. Alipenda Maandiko Matakatifu

Maisha yetu ya kiroho yanasitawishwa si kwa mkate wa Mungu tu, ila pia kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Mwamini anayesoma Biblia hufanya matayarisho mazuri kwa sala ya ndani. Mt.Yohane anasema: Miujiza mnayoiona hapa iliandikwa ili mpate kuamini kwamba Yesu ni Masiah, Mwana wa Mungu na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake.[324]



Mwamini anayesoma Maandiko Matakatifu ana nguvu ya kutupa mwanga uleule wa ndani waliopewa mitume wa kwanza. Neno la Mungu tunalochukua wakati wa mahubiri na sala litapenya zaidi na zaidi maisha yetu ya kila siku "atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo."[325]

Alipokuwa katika Sinagogi huko Konstanz (1870-1874) Padre Jordan alichagua mapema lugha ya Kiebrania na mwisho wa masomo yake kwenye sinagogi aliweza kusoma Biblia ya Kiebrania vizuri kabisa. Katika Chuo Kikuu cha Freiburg (1874-1877) alisoma maandishi ya asili ya Kiebrania na Kigiriki na alipata tathmini: " Vizuri sana na juhudi isiyo ya kawaida."[326] Askofu angalipenda kwamba Padre Jordan

[323] D IV / 15
[324] Yn. 20:31
[325] 2Kor 4:6
[326] DSS XII, 61

apate digrii ya udaktari katika lugha za mashariki ili achukue kiti kwenye Chuo Kikuu cha Freiburg

Akiwa mseminari, Padre Jordan tayari alijua nguvu ya pekee ya neno la Mungu: *Hatimaye, nitasoma Maandiko Matakatifu kwa heshima kubwa na ibada, siyo kupitia harakaharaka, lakini kusoma kwa moyo na kwa uangalifu hasa kwa mambo yanayofaa kunifanya niwe mnyenyekevu.*[327] *Daima soma Maandiko Matakatifu kwa heshima kubwa, na kwa magoti yako, angalao wakati ukiwa peke yako.*[328] *Mahali pengine ameandika: Weka nguvu kubwa zaidi katika kutafakari Maandiko Matakatifu, mjifunze, kutanabahi, mkitumia komentari kama Maldonati, Cornelius wa Lapide.*[329] *Soma Maandiko Matakatifu kwa undani! Mtumikieni Mungu peke yake; msitawishe na kuimarisha roho kwa mambo haya matatu: Mkate wa Uzima-tafakari-masomo ya kiroho. Roma, Nov.27, 1878.*[330]

Alitaka Maandiko Matakatifu yaongoze roho yake ya kitume na kwamba hiyo iwe ndio tabia ya shirika lake. Alitafuta mwanga ili ajue mapenzi ya Mungu.Alieleza msingi wa Shirika kutoka sehemu nne za Maandiko Matakatifu. Ndiyo vichwa vya habari katika toleo lake la kwanza.



Huu ni uzima wa milele; watu wakujue wewe, Mungu wa kweli wa pekee, na kumjua Yesu Kristo ambaye ulimtuma"[331] Wenye hekima watang'aa kama nyota za angani; na hao watakaowaongoza watu kwenye haki kama nyota kwa milele na milele."[332]

[327] D I / 68
[328] D I / 68
[329] D I / 139
[330] D I / 150
[331] Yn. 17:3
[332] Dan.12:3

"Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi: mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu;na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi."[333] "Angalia, tumeacha kila kitu na kukufuata wewe. Tutapata nini?[334]

Ingawa Mwanzilishi aliweza kusoma Maandiko Matakatifu katika lugha ya asili, Maandiko Matakatifu, kamwe hayakuwa somo lake haswa.Alitaka kujifunza kumjua Yesu kwa njia ya Maandiko Matakatifu.Moja ya maelezo yake ya kwanza kwa wafuasi wake yalikuwa: *Watasoma sura moja ya Maandiko Matakatifu kila siku.*[335]

## 7. Mkataba na Mungu



Katika kalenda ya Padre Jordan, tunaona kurasa tatu za kukumbukwa, yaani, sehemu ya I kutoka ukurasa 202 hadi 204A.Zilichakaa na shikamana. Anaandika kurasa hizi kuhusu Watakatifu Wote 1891; ni kama aina ya "mkataba" na Mwenyezi.Pembeni upande wa juu kulia, alionesha siku tano baadaye, pengine sababu ya siku hizi,alirudia mkataba ule kwa kujua kabisa:30.10.1892-21.12.1894-16.11.1897 na 08.01.1909.Mwishoni,April 20,1903, anarudufu mara moja zaidi maandishi yote kwenye kalenda yake.

Leo sikukuu ya Watakatifu wote, mkataba huu ulifanyika kati ya Mwenyezi na kiumbe Chake kidogo sana.

1 ) Kinachosemwa kiumbe kinajitoa chenyewe kikamilifu na kwa milele kwa Mwenyezi Muumbaji wake.

2 ) Kiumbe kinatoa na kitatoa kwa Muumba wake, chochote Muumbaji alichompa, kumpa, na atakachompa.

---

333 Mt 28:19
334 Mt 19;27
335 Sheria 1882 / DSS I, 24

3 ) Kiumbe, kinatumaini kwa nguvu zake zote, katika msaada wa Mwenyezi, sio katika ule wa mtu, anajikabidhi kwa utawala wa ulimwengu wote, kama, watu wote ambao wanaishi sasa au baadaye, kusudi wamjue,wampende na kumtumikia Yeye, na wenyewe wapate wokovu.

4 ) Kiumbe pia kitaongoza viumbe visivyo na akili kwenye huduma ya Mwenyezi.

II Kiumbe kinategemea kwa matumaini neema hizi kutoka kwa Mwenyezi, Kwa huruma ya Bwana wetu Yesu Kristo na kwa maombezi ya Bikira Maria Mbarikiwa:

1 ) Muumbaji atakivika kiumbe chake kwa utakatifu mkubwa, zaidi ya yote, kwa unyenyekevu ili kwamba, kadiri hii inavyowezekana, angekuwa chombo kifaacho kwa matumaini ya maongozi ya Mungu na kwa uaminifu kutimiza ahadi zake, na baada ya maisha haya Atampokea yeye katika uzima wa milele.



2 ) *Muumbaji, katika uwezo wake wote, atasaidia kiumbe Chake kwa mkono wake wa nguvu kukamilisha kile alichoahidi.* [336]

Namna alivyojizatiti katika "Mkataba" huu inaonekana katika rejea mbalimbali anazofanya katika miaka 18, kwa mfano: *Hata yakija mateso juu yako, daima songa mbele katika Bwana kulingana na lengo, ukurasa 52, kumtumainia Bwana kwa imani kubwa. (18.09.1904)*[337] Mwaka mmoja baadaye anaandika: *Amrisha kiasi kwamba mmoja atii kwa furaha. Ee Mungu unisaidie kulingana na Mkataba! (01.07.1905)*[338] Anasema juu ya "mkataba wetu" kati ya kiumbe na

[336] D I / 202-204
[337] D II / 79
[338] D II / 91

Muumbaji, Na baadaye: *Songa mbele na tenda kwa ujasiri kulingana na mkataba, ukimtumainia Mwenyezi, ataakayekuokoa na maadui wako wote n.k. (30.12.1906)*[339]*Au: Ee Mungu, Mwenyezi, mmoja, nionyeshe mapenzi yako! Mama wa Mungu, Mama yangu uniombee, ili niweze kuendelea na kutimiza mkataba. (08.01.1909)*[340] *Ee Mungu Mwenyezi, unisaidie kulingana na Mkataba; nimekutumaini wewe, sitaaibika milele! (22.01.1909)*[341]*Tunza mkataba ulioweka na Mungu! Lakini sio chini ya maumivu ya dhambi (05.02.1909)*[342]

Mkataba una kila kitu cha kufanya na wazo lake lisilozuilika la kuanzisha Shirika jipya. *Ee Mama wa Mungu, Mama yangu uniombee. Ee Bwana, nakutumainia. Neema zako zinisaidie; Naweza kufanya kila kitu katika wewe unayenipa nguvu. Onyesha nguvu zako na uinue kikundi (kitakatifu) kipya. (20.02.1909)*[343] Baadaye, hafanyi rejea katika mkataba, tena sababu hafanyi rejea zaidi kwenye uanzishaji wa Shirika jipya.



Mara nyingi sana, Mungu amefanya maagano na viumbe Vyake.Adam kwa njia ya mti wa mema na mabaya kama ishara wazi. Daima kuna watu waliofanya maagano na muumba wao, zaidi katika mtindo wa kujiweka wakfu. Mfano, Mt.Theresa wa Lisieux na Mt.Elizabet wa utatu, ambaye, kwa njia hiyo hiyo alitoa jibu kwa uzoefu wa ndani wa upendo wa Mungu. Hivyo hivyo, mkataba wa mwanzishi umeandikwa ndani ya uwepo wake; katika wingi wa upendo unaotafuta chanzo chake katika Mungu mwenyewe, kama anavyoandika: *Mungu aliyetoa utashi, pia akamilishe!*[344] Ni upendo wa Mungu wenyewe unaoendelea

[339] D II / 104
[340] D II / 121
[341] D II / 121
[342] D III / 1
[343] D III / 1
[344] D I / 203

kumiminika katika kwake, unaomsukuma kukamilisha mkataba ili aweze kuishi kikamilifu kwa njia ya upendo wa Mungu wenye utajiri na kumwagika katika moyo wake.

Inashangaza kwamba wanachama mbalimbali, walioandika maisha ya kiroho ya Mwanzilishi, na kusoma kalenda yake ya kiroho hawakutaja mkataba huu. Katika mwanga wa yote tujuayo juu ya Mwanzilishi, hii kwa kweli inashangaza. Kama tukitaka kuufikiria kwa upole na kwa namna inayokubalika, kwa kweli inaonyesha wazi, hata kama inasababisha maswali ambayo ni vigumu kujibu.

Ni katika uzoefu wa kimafumbo tu wa Mwanzilishi unaweza ukajibiwa. Kwake, uumbaji wote umetokana na upendo wa Mungu. Yesu, Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho wa viumbe vyote. Mwanzilishi anaonyesha ufalme fulani pamoja na elimuroho ya Mt. Francis ambaye aliona mwanga wa utukufu wa upendo wa Mungu katika viumbe vyote.



Tayari 1877, tunaona sala kwenye kalenda yake ambapo anaungama mbele ya baraza la mbinguni na viumbe vyote kwamba hakuna kitu kizuri kwake na ndio maana anathibitisha kwamba vizuri vyote alivyo navyo vimetoka kwa Mungu: *Bwana Yesu Kristo, Mwokozi na Mkombozi wangu, Mungu pekee, Mmoja na Utatu, usiyeelezeka na usiyefahamika milele! Ah, mimi mdhaifu mdhambi zaidi mbele Yako; Mungu wangu, kwa magoti yangu naungama mbele yako na mbele ya baraza lote la mbinguni, mbele ya viumbe vyote, kwamba mimi ni mdhambi kabisa; wala siwezi kufanya chochote kizuri bila wewe, Bwana wangu na Mungu wangu; ambapo, mbele yako na mbele ya viumbe vyote, natamka kwamba chochote kizuri ndani yangu ni kutoka kwako, na chochote kizuri nilichofanya au nitakachofanya, ni kwa msaada wako kwamba nimekifanya, nafanya au nitakifanya.*

*Kwako peke yako heshima, nguvu,na utukufu kutoka viumbe vyote kwa milele na milele.Amina.*[345]

Hotuba hiyo juu ya Muumbaji na viumbe pia inashangaza, inaongea toka mbali, ndogo na tegemezi lakini pia inasema kwamba ameungana na Mungu kwa njia ya umoja wa fumbo, pamoja na viumbe vyote, kwamba anafikiria mwanga wa utukufu wa Mungu.

Ukisoma maandishi yote, ni muungano na Mungu unaomgusa mtu zaidi. Ni umoja huu tu na Mungu unaoweza kutoa ufunguo kwa maandishi ya kimafumbo. Kwenye mkataba tunaona maneno yake aliyoyapenda yaliyojazwa na mabadiliko ya ndani kiasi kwamba hatuyaoni sehemu nyingine. “Kabisa”, “kwa nguvu zake zote”, “daima na siku zote”, “watu wote”, “wamjue Yeye”, “wampende kumtumikia na kupata wokovu kwa njia hii”. Anaweza kufanya mkataba huu kwasababu tu anaamini kwamba Mungu anayetoa utashi pia atatoa uwezo wa kufaulu. Hii siyo juu ya watu wawili walio sawa; mkataba unatoka kwa mdhaifu, lakini ni jibu kwa hisia ya upendo wa Mungu na uaminifu. Muumbaji na kiumbe vina uhusiano kati ya mmoja na mwingine. Anajua kuwa Mungu ni kichwa na bega: mwenye nguvu zaidi. Akiwa sehemu ya viumbe, anataka, kwa niaba ya watu wote na vitu vyote, kutoa jibu kwa upendo wa Mungu ili kwamba kuwe na uwezekano wa kurudi katika uwingi wa uwepo wa daima.Mungu pekee anaweza kuuleta mkataba huo kwenye ukamilifu. Kwa kweli, ni katika upendo wa kweli tu kwamba Mungu anaweza kufanya agano na watu. Mmoja anaweza kupata hisia fulani kutoka umbali usioweza kuunganishwa kati ya Muumbaji na kiumbe. Kwa kawaida, Mungu anafanya agano; hapa, ni kiumbe kinachojibana chenyewe ili kumfanya Mungu ajulikane, apendwe na kutumikiwa na



[345] D I / 101

watu wote na viumbe vyote. Kiumbe hakitajitwalia chochote ambacho kimepokea au kitapokea. Kila kitu kitainuliwa juu katika upendo wa asili usio na mipaka. Ndiyo maana anatumaini kwamba Muumbaji atamtajirisha kwa utakatifu mkubwa kuwa safi katika unyenyekevu mkuu, kurudisha utukufu wote kwa Mungu.

Upendeleo alioupata Padre Jordan kwa njia ya sala kutoka Muumbaji umempa hamu ya kukamilisha muungano na Mungu: *Kinachosemwa kiumbe kinajitoa chenyewe kikamilifu na kwa milele kwa Mwenyezi Muumbaji wake, na baada ya maisha haya Atampokea katika furaha ya milele.*[346]

Inaeleweka kwamba Mwanzilishi anaweka msisitizo kwa anayetoa na anayepokea mtazamo kinyume kati yao. Anaandika: Kiumbe…1) kinajitoa chenyewe kabisa; 2) kinatoa na kitatoa kwa Muumba wake, chochote Muumbaji alichompa, kumpa, na atakachompa; 3) Kiumbe kinategemea msaada wa Mungu; 4) Kiumbe pia kitaongoza viumbe visivyo na akili kwenye huduma ya Mungu..



Kwa upande mwingine anasisitiza zaidi kwa mpango wa upokeaji katika mkataba: 1) kiumbe kinategemea kwamba Muumbaji atakivika kwa utakatifu mkubwa; 2) Muumbaji atakipokea kiumbe chake kwenye furaha ya milele; 3) Atakisaidia kiumbe chake kukamilisha kile alichokipendekeza. Kwa nguvu ya Mwenyezi anchagua njia ya Shirika kama hatua ya utakaso. Anajitoa nje kusudi ajue kwamba anabebwa kwa nguvu za uumbaji za Mungu.

Padre Jordan anajua upendo wa Mungu usio na kina. Kwa kina gani naweza kushuka katika upendo wa Mungu, sitafika chini kwa sababu hakuna mwisho. Upendo wa Mungu hauna kina. Padre Jordan alifika chini kusiko na kina katika sala zake.Kwa hiyo, mishangao yote hii, maelezo, hali

[346] D I / 202-203

ya kujisikia kutoweza kujieleza mwenyewe.Daima alijisikia zaidi kuliko alivyoweza kujieleza.

Inabaki kuwa kitendawili namna Mwanzishi alivyofikia mkataba huu uliogusa maisha yake kwa nguvu. Hatujui alikopata mwanga, na chanzo chake ni nini.

## 8. Nia ya shirika 'Intentio Societatis'

Mara tu Mwanzilishi aliporudi safari yake toka Nchi Takatifu, aliandika mambo ya msingi kwenye kalenda yake ambayo aliyaita "Intentio Societatis", yaani nia na mwelekeo wa Shirika.[347] Kabla ya yote, anaandika utangulizi kama alivyokuwa akifanya daima, ambapo anaelezea mtazamo wake kuhusu Shirika:

### Mwelekeo wa Shirika



Kwamba lisitawi zaidi na kuenea kila mahali na kutimiza zaidi kwa heshima ya Mungu Mwenyezi na kwa wokovu wa roho, na kwamba lisiwe na mawaa au shida, kumpendeza Mungu na kumtumikia Yeye peke yake. Oh, namna upendeleo mkubwa ulivyo kwa watawa wote mwanzoni mwa mashirika yao matakatifu! Namna Ibada zao zilivyokuwa kubwa katika sala! Namna juhudi zao zilivyokuwa kubwa kwa fadhila! Namna taratibu zilivyofuatwa vizuri (Kumfuasa Kristo I, 18)

Baadaye, kulikuwa na nukuu nane za Maandiko Matakatifu ambayo lazima yaweke msingi wa maisha ya kitume na kutoa sura kwa kumfuasa Kristo. Mwanga wake kama Mwanzilishi unapatikana kwenye Maandiko Matakatifu.Yeye ni mfano unaoishi wa baadhi ya maandiko aliyoyapenda yatakayokuwa kama mwongozo wa maisha yake yote.

[347] D I / 157

Kwa sala, alitambua maandiko haya: *Nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu; na wakaziacha nyavu zao mara moja na Kumfuata*[348]

Anajenga utume katika wito huu wa Bwana.Mungu daima anaanza. Sisi tunaweza tu kutoa jibu la wito wake.

*Kila mmoja aliyeacha nyumba au kaka au dada au baba au mama au mke au watoto au nchi kwa ajili ya jina langu atapokea mara mia na kupata uzima wa milele.*[349] Sharti ambalo linadai kuwa mtume wa Bwana ni kuacha kila kitu kwa ajili ya utume. Anayependa mtu au kitu zaidi kuliko Bwana hamstahili.Hiyo ilikuwa imani yake haswa. Mwanzilishi alitaka kuacha kabisa kila kitu, kwa ujumla na kikamilifu.Huko kulikuwa kujitayarisha Kiinjili.

*Nenda, simama ndani ya kanisa na kutangaza kwa watu wote maneno ya uzima huu.*[350] Mwanzilishi pengine aliyajua sana maneno hayo, kwa sababu anayarudia baadaye katika sheria za kitume.

*Wenye hekima watang'aa kama nyota za angani; na hao watakaowaongoza watu kwenye fadhila watang'aa kama nyota kwa milele.*[351] Hiyo ilikuwa daima moja ya maandiko yake aliyoyapenda: "Kung'aa kama nyota za angani". Tunalazimika kutoa ushuhuda wa maisha ya matumaini ndani yetu.

*Hakuna atakayepata taji bila kishi kikamilifu kulingana na sheria.*[352]

[348] Mt 4:19-20-D I / 157
[349] Mt 19:29-D I / 157
[350] Mtd 5:20-D I / 158
[351] Dan. 12:3-D I / 158
[352] 2Tim2: 5-D I / 158

*Hakuna anayepigana kwa ajili ya Mungu na kujiingiza katika mambo ya kidunia.* [353] Wazo la kujitahidi, kupigania imani, kuwa askari wa Kristo kilikuwa kitu cha msingi kwa Mwanzilishi.Baadaye, anaruhusu kuangaziwa mara nyingi zaidi kwa mawazo ya kupigana ya Mt.Ignatius:Kupambana chini ya mwanga wa Kristo dhidi ya mwovu.

*Utii ni bora kuliko sadaka.*[354] Na anaongeza maneno ya Mt.Jerome*: Utii ni uhuru wa hali ya juu; anayeupata hawezi kutenda dhambi mara nyingi. Kristo alikuwa mtii mpaka kufa, hata kufa msalabani.*[355]

Ukitafakari hizo sehemu nane, tunaweza kiasi fulani kutofautisha namna Padre Jordan alivyofikiri juu ya Shirika lake. Kumfuasa Bwana kwa ukamilifu kabisa, kwa uhakika na kwa njia ya maisha ya kitume, kuacha kabisa mambo ya kidunia, kujitoa kabisa kwa ufalme wa Mungu. Mwanzishi lazima alipiga mahali pagumu, wakati 1902; viongozi wa Kanisa walipotoa tangazo la kuzuia kuingiza Maandiko Matakatifu katika Katiba.



## 9. Sheria za kitume.

Zinazoitwa Sheria za kitume[356], zilizama kabisa kwenye nukuu za Maandiko Matakatifu, ilikuwa tabia ya upendo na elimu yake kwa Maandiko Matakatifu.

Tukisoma, tutashangazwa na sehemu nyingi za Maandiko Matakatifu:

*Wapendwa, (Pe 2:11)*
*Wafundisheni watu wote, (Mt. 28;19)*

---

353 2Tim24-D I / 158
354 1Waf 15:22-D I / 158
355 Wafil 2:8-D I / 159
356 DSS I, uk.33 / Sheria ya 1884

*hasa watoto wote, wamjue Mungu wa kweli,*
*na yule aliyemtuma,Yesu Kristo. (Yn 17:3)*
*Ninawatafuta mbele ya uso wa Mungu*
*Na ninampata Yesu atakayewahukumu wazima na wafu?*
*Na tokeo lake ni ufalme,(Tim 4:1)*
*Tangazeni neno la Mungu( Waebr.6:5)*
*Sisitizeni wakati unaofaa au wakati usiofaa;*
*Onyeni na kufundisha kwa uvumilivu mkubwa.*
*Nendeni na kuwaambia watu kwa uvumilivu*
*maneno yote ya uzima wa milele.(2Tim 4:2)*
*Tangazeni na kuandika mafundisho makuu yote ya*
*mbinguni kwa wote,bila kuacha.(2Tim 4:17)*
*Hayo ni mapenzi ya Mungu,(1Wates.4:3)*
*Wapendwa, kwamba wote wajue ukweli wa daima( Yn17:3)*
*Natafuta sio kuacha kutangaza nia za Mungu,(Mtd 20:27)*
*Ili muweze kusema na Mt.Paulo:*
*"Sina hatia na damu ya mtu yeyote"(Mtd 20:26)*
*Msiache kumuonya kila mmoja mchana na usiku,*
*Hata kwa machozi yao.*
*Msiruhusu muda wowote upotee*
*Kutangaza na kufundisha mafudisho makuu yamhusuyo*
*Mungu*
*Kwa wote, waziwazi na toka nyumba hadi nyumba.*
*(Mtd 20:20)*



Padre Jordan anatumia mlolongo wa sehemu za Biblia akitaka kuandika mawazo yake muhimu. Amejificha kabisa nyuma ya maneno ya Mungu.Hivyo Sheria ina nguvu maalum kwetu, kwa sababu imeegemea katika neno la Bwana na katika desturi za Kanisa la mwanzo. Mwanzilishi anafikiri kuwa yeye ni nabii ambaye atatangaza ujumbe katika jina la Mungu: Anatumia maneno ya Mt.Paulo: "Ninawatafuta mbele ya uso wa Mungu na wa Yesu."[357] Hiyo ndiyo inayofanya sheria hiyo istahili mbele yetu.

[357] 2Tim 4:1

Sheria ya kitume siyo matokeo ya tafakari ya kiakili au vipimo vya uwezo. Mwanzilishi aliandika hayo maandishi ya kikarama nje ya uzoefu wa ndani. Mei 31,1901 alisema kwenye mkutano: *Naweza kuwaambia kwamba hakuna sheria niliyoandika iliyonipa faraja ya mbinguni zaidi kama ile niliyoandika mbele ya Mtakatifu zaidi. Machozi ya furaha yalinitoka kana kwamba kuidhinisha kuwa haya ni mapenzi ya Mungu*.[358]

Idhinisho la mbinguni daima ni tofauti kutoka lile la Kanisa. Mwanzilishi aliandika sheria hii 1884 alipoomba idhinisho la katiba katika mwaka 1886, sheria hii inayohusu utume iliondolewa na Msgr.Jacquemin, mkaguzi wa kanisa, kwasababu ilikuwa na nukuu nyingi kutoka Maandiko Matakatifu.Alikuwa mkarismatic mno. Katiba lazima iandikwe kwa uwazi na kisheria kwa maneno machache. Katika toleo la Katiba ya 1888 sheria hii ilirudishwa kwa msukumo toka shirikani.1896, inapotea kabisa toka kwenye katiba.[359] Baada ya Mtaguso katiba na sheria za kitume zilirudiwa, wakati wa mkutano mkuu wa 1981, ziliongezwa kama utangulizi na ziliidhinishwa na uongozi wa Kanisa mwaka 1983. Siku hizi sheria hizi zinapamba katiba kama matangulizi, kwa sababu sio kazi ambayo inatakiwa kufanyika kikamilifu kama tabia ya kiroho kwamba ituhamasishe popote na kwa kila kitu.




Wapendwa ni neno la kuanzia lililotumika na Padre Jordan katika sheria zake za kitume, na anarudia maneno hayo mara mbili katikati ya habari kama maelezo ya ziada ya hisia zake za kibaba. Hatoi mwongozo wowote kwa wafuasi wake, lakini anafanya rufaa kwa wanawe kwa utume wa ndani ya moyo wake wa kitume. Ni wazi, kuwa ni wakati huo tu anazungumza hivyo kwa moyo katika

[358] Chap. 31.05.1901, DSS XXIII, 431-432
[359] Fr.Paulus Pabst kwa mwandishi



Picha ya Padre B.Luthen, mkono wa kuume wa Padre Jordan
1846-1911



Picha ya Fr.Pancratius Pfeiffer, aliyemfuata Fr. Jordan
na kama Mkuu wa Shirika.
1915-1945

katiba kwa wanachama wa Shirika. Wakati sehemu ya maandishi ya Lebanoni yanaelekeza kwenye ukumbakumba wa kitu chenyewe, " kwamba wote wakujue wewe", agano hili linaelekeza kwenye ukumbakumba wa wokovu. Neno "wote" linajitokeza mara tisa katika hatua mbalimbali.

Sheria hii ya kitume ni kama ilikuwa jibu kwa uzoefu wa Lebanoni. Hapa pia, maneno "uzima wa milele" na " kumjua Mungu wa kweli" yanatajwa wazi kwenye utangulizi kama ilivyo katika katiba za 1882 na 1884.

## 10. Wosia wake wa kiroho.

Unaoitwa wosia wa kiroho[360] ni moja ya maandishi ya kikarismatiki ya Mwanzilishi, pamoja na sheria za kitume.Ni maandishi yaliyo katika kilatini, katika karatasi ya akiba. Hakuna tarehe, ni kichwa cha habari tu: "Rom, Borgo Vecchio, 165* Generaldirection der Katholischen…"na kupigia mstari "Wosia" katika mistari ya mwanzo ya habari hii, Padre Jordan ameiita " wosia wake wa mwisho".



Taarifa za uhakika zinaonyesha kuwa habari hii haikuandikwa mwishoni mwa maisha yake.Kuna maoni tofauti kuhusu tarehe na mvuto, vikilalia zaidi kwenye kudhani kuliko ukweli.Hakuna wazo la kuhitimisha lililounganisha wosia pamoja na utengano na masista wa kwanza (1885) au na kuugua sana kwa Mwanzilishi (1897).

Kinachofanya wosia uguse zaidi ni ukweli kwamba tunaweza kuuona karibu wote kwenye wosia maarufu wa Mt.Francis wa Siena.

Miezi 6 kabla ya kifo chake, alikuwa na miaka 45, April 1226, Hugolinus alimleta Francis wa Siena kumwona mtaalamu maarufu. Usiku mmoja alikuwa karibu na kifo

[360] AGS B,105

na waliogopa kwamba angekufa. Bruda Benedictus aliitwa toka Prato na Francis alisema maneno na Benedict ayaandike kama wosia kwa Mabruda wake. Wosia huu unahesabika kwa mistari mitano tu, na kwa hiyo haiwezi kuchanganywa na wosia alioandika Francis miezi mitano baadaye huko Portiuncula, wenye idadi ya aya 45

Wosia wa Siena ulikuwa katika roho ya Padre Jordan, kwa sababu baadhi ya sentensi zimechukuliwa moja kwa moja toka maandishi ya Mwanzilishi.

Tutatoa hapa maandishi ya Padre Jordan yaliyoitwa wosia na tunaongeza kila pointi rejea kwa wosia wa Mt.Francis.

Salamu na matashi mema kwa mabradha wote

Wosia wa Padre Francis Maria wa Msalaba kwa wanawe wa kiroho, waliopo na watakaokuwepo wakati wowote ujao katika Shirika:



“Angalia ninavyowabariki wenzangu, waliopo Shirikani sasa au watakaoingia mpaka mwisho wa dunia” (Aya ya kwanza ya wosia wa Mt.Francis wa Siena)

1. Matumaini ya maongozi ya Mungu yawe urithi wenu wa daima. Yatawaongoza kwa uangalifu kama mama mwenye upendo. (rej. Zab 54:23-zab 77, Mt 6:25, 1Pt 5:7)

2. Ninaweka mikononi mwenu lulu na hazina yenye thamani isiyopimika ndiyo Ufukara wa daima ambao Mungu atawadai arudishiwe siku ya hukumu (Mt 13:44, Mt 2:36)  “ Daima wampende na kumdumisha mama yetu Ufukara mtakatifu?” (Aya ya nne ya wosia wa Siena)

3. Mtumaini Mungu tu na imani yenu yote iwe Naye tu. Yeye kama mshindaji hodari atapiga vita badala yenu. (Jer.20:11, Eccl 4:33)

4. Ole wenu ikiwa matumaini yenu mtajenga juu ya watu na juu ya mali za dunia.(Jer.17:5-7)

   Muwe siku zote waana waaminifu wa Mama kanisa Katoliki. Mfundishe –linachofundisha; msadiki-linachoamini; mkatae-linachokataa.

   “Wawe daima waaminifu na watiifu kwa maprilate na viongozi wa Mama Kanisa Takatifu” (aya ya tano ya wosia wa Siena)

6 Mpendane katika Roho Mtakatifu na mapendo yenu yaonekane mbele ya watu. (2Kor 6:6, Wafil.4:5 )

   Mfahamu kwamba nimewapenda kwa moyo wote. Ningependa hata ninyi kwa ninyi mpendane. (1Yn 3:23, Yn 13:1.)

   “Ili …daima wapendane.”? (Aya ya tatu ya wosia wa Siena)

8. Mjitakatifuze na muongezeke mahali pote duniani, mpaka mwisho wa nyakati (Mw.1:28, Mt 18:20).

Kwa jina la Bwana. Amina.

Mwanzishi anafanya pointi nne kuwa msingi wa fadhila anazotaka kuziacha kama wosia wa daima kwa Shirika lake:

1) Matumaini ya maongozi ya Mungu

2) Umaskini wa kienjili wa daima

3) Uaminifu kwa Kanisa Katoliki la Roma

4) Upendo wa kindugu.



Padre Jordan akiwa na miaka 70 ya kuzaliwa.
*1918*

# VIII .

## Je Padre Jordan alimtafakari Mungu zaidi na habari zake?

Chochote tunachojua kuhusu Padre Jordan kinaonyesha wazi kwamba aliishi katika uhusiano wa karibu na Mungu, ambapo sio matokeo ya mazoezi ya kujitesa au nguvu za kibinadamu, bali ni zawadi toka kwa Mungu tu. Pamoja naye, tunapata maneno na mawazo yaleyale tunayoyapata toka kwa wanaomtafakari Mungu zaidi na habari zake. Kwa kurudiarudia, alijua wakati mwafaka wa kiroho, kumezwa na upendo wa Mungu.Tukimpenda Mungu kama alivyofanya mwanzilishi, bila kuuona uso Wake; kama tunamfuata Mungu bila kusikia sauti yake; tukiweza kumfuata kwa uaminifu na kwa kujitoa mpaka kifo, halafu tunaweza kusema juu ya hali ya kumtafakari Mungu zaidi (Mystic). Kama furaha ya ndani ikitutawala tunapokandamizwa na msalaba, kama tunatunza amani wakati wa kukata tamaa kibinadamu, halafu tunaweza kutegemea kuwa Roho ya Mungu inafanya kazi ndani yetu. Hiyo ndiyo sababu haikuwa vigumu kwa wafuasi wa Padre Jordan kumwita “Mheshimiwa Baba” kama Padre

Bonaventura Luthen alivyofanya, na kumwona yeye kama "mtu wa Mungu"

Kwa Padre Jordan utakatifu haukuwa sawa na ukamilifu. Pia alijua vizuri udhaifu wake mwenyewe na mara nyingi alikumbana na madhaifu ya wengine. Pia alijua kwamba hali ya fadhila, kwa yenyewe, haifanyi utakatifu wa mtu. Mtakatifu ni yule anayemshiriki Mungu kwa karibu zaidi kwa namna isiyo ya kawaida; mmoja ambaye, daima bila kujua, anamleta Mungu karibu kwa wenzake na kumfanya Yeye aweze kukaribiwa bila shida.

Hali ya utakatifu imefichika toka kwa watu sababu inakuwepo chini ya mahangaiko ya hofu za kila siku na udhaifu. Musa pia alidharau ukweli kwamba uso wake uling'aa kwa utakatifu baada ya kuongea na Mungu.Mwanga huu mara chache unatambulika kwa watu walio wazi; wengine hawana hisia yoyote kwa mwanga huo.



Mwanzilishi alijifikiria kuwa mtu masikini ambaye alikuwa akimwomba Mungu kwa kila kitu.; lakini kwa wengine daima alikuwa mwanga wa uwepo wa Mungu.

Utashi wa kweli wa kuwa mtakatifu kwake ulikuwa msingi wa utakatifu binafsi. Mungu anataka utakatifu wetu. Wakati wa mkutano, alisema juu ya uzoefu wake binafsi: *Lakini tafuteni [ kuwa watakatifu ] kwa njia zilizo sahihi: si katika kujifungia kiroho, bali kwa njia ya mateso,kwa njia ya utii, ufukara, kufuata taratibu za kitawa kikamilifu…wenye uvuguvugu kamwe hawawezi kuwa watakatifu…Acha gharika zitoke ndani au nje. Hata kama jehena zote na ulimwengu wote vingetoa hukumu dhidi yako, jiambie, "Lazima niwe mtakatifu kwa gharama zozote." Vitu vingine vitakuwa na maana gani [mateso makubwa, kazi, ndoto za kuongoa mataifa yote n.k.] kama tusipofanya jitihada kwa ajili ya utakatifu? Mtu mmoja mtakatifu atafanya mengi zaidi kuliko maelfu na maelfu ya wengine.*[361]

[361] Chap.20.04.1894, DSS XXIII, 22-24

Padre Jordan alijua kuwa Mungu ndiye peke yake Mtakatifu.Yeye ni Mtakatifu wa Israeli.[362] Kwa mwanzilishi kuwa mtakatifu kulimaanisha: “kuishi katika ile hali ya mawazo yaliyo ndani ya Yesu Kristo”[363] na kumezwa kwa moto wa Roho wake Mtakatifu. Hasa katika pongezi fupi alizozoea kupeleka kwa wanachama wake, angeeleza hii kwa namna tofauti na kwa maneno yanayojitosheleza. Kwa mfano, kwa Fr.Robert Waltz aliandika: *Kristo aishi ndani yako*[364] Kwa masista aliandika: *Roho ya Yesu Kristo iwaangaze nyote na iwape nguvu ya kufanya kazi zaidi kwa heshima ya Mungu na kwa faida ya watu maskini.*[365] Na kwa wenzake: *Bwana mwema awajalie neema zaidi, akae na kufanya kazi ndani yenu, na awe furaha yenu, wokovu wenu na yote kwenu.*[366]

## Utakatifu wake ulikuwa ni utakatifu wa kitume

Kwa Padre Jordan jitihada za utakatifu zilikuwa hasa za kitume.Hakupenda, kwanza katika ukamilifu wake mwenyewe au zawadi yoyote. Alitaka kuwa mtakatifu kama alivyoamini kwamba ni katika njia hii tu angeweza kuokoa roho. Amekuwa Padre kwa sababu alijisikia kuwajibika kwa ajili ya wokovu wa watu. Sala zote, kazi zote, juhudi zote na hofu, na pia uzoefu wake wa kumshiriki Mungu kwa karibu yote hayo yalielekezwa kwenye lengo hili tu: kuokoa roho, kuwafanya watu washiriki maisha ya kimungu yaliyotolewa kwetu na Kristo. Kwake, kujitakatifuza binafsi kulikuwa ni kwa faida ya wokovu wa watu wenzake.



[362] Hos 11:9
[363] Phil. 1:21 na 2:5
[364] DSS X, no.991, 11.06. 1909
[365] DSS X, no. 1150, 01.01.1914 (kwa sista Ambrosia Vetter)
[366] DSS X, no. 997, 05.01.1909

Maisha ya jumuiya, pia,yalitolewa maana ya kichungaji. Alitamani kwamba maisha ya sala na kutanabahi yaangaze na kuhamasisha shughuli za kitume. Mtu anayemtafakari Mungu zaidi ni yule anayefungua macho yake na moyo kwa mateso ya watu na kilio dhidi ya maovu ya jamii. Wakati wa mwanzilishi 'mysticism' lilikuwa neno lenye kutiliwa mashaka ni ufunguo kwa chochote ambacho kilikuwa hakieleweki, cha kushangaza au kisicho cha kawaida.

Katika wakati wetu, neno hilo 'mysticism' linapata maana ya kitume. Ni maisha ya kuishi kwa njia ya imani. Kumweneza Mungu kwenye giza na kwenye jumuiya zisizoelewa. Watu hawaulizi tena juu ya uhakika wa uwepo wa Mungu; wanauliza juu ya uzoefu au hisia za kuwa na Mungu.

Tamaa ya kuwafanya watu washiriki katika maisha ya kimungu ilikuwa ni kishawishi cha maisha ya Padre Jordan. Moto ulioletwa na Yesu duniani ulimmeza.



Kwenye kalenda yake tunasoma: *Mimi nipo hapa, nipeleke-kwa ajili yako, kwa ajili ya roho, kwa ajili ya Kanisa la Mungu. Wote, Ee Baba, wote, wote, Ee Mungu, wote Ee Yesu, wote, Ee Mwokozi wa dunia, natamani kwa hamu kubwa kuwaokoa wote! Ah, okoa roho! Ah, okoa roho! Ninakuomba na kukusihi, okoa roho! Kwa gharama zozote okoa roho!*[367]

Mmoja anaweza kuita maneno hayo ni pumzi tulivu ya Roho, anayetamani kumwaga upendo wake kwa watu wote. Huruma kwa watu inakua kama mmoja ameungana zaidi na Mungu katika upendo. Juhudi za kitume ni upendo wa Mungu unaomwagwa kwenye mioyo yetu na kutaka kuwamwagia wengine. Matendo na sala hutoka kwenye chanzo kimoja. Kadiri ya mwanzilishi wetu, kwa upande

[367] D II / 12

mmoja, sala lazima iangaze maisha ya kitume na kwa upande mwingine, shughuli za kitume lazima zitokane na wingi wa sala au tanabahi. Tamaa ya mwanzishi ya kuokoa watu wote ina uhusiano na undani wa muungano wake na Mungu. Upendo wake kwa Mungu ni, katika hali halisi, hufanana na tamaa yake kuu ya kuwafanya watu wote washiriki katika upendo huu. *Wote, Ee Mwokozi wa dunia, natamani kwa hamu kubwa kuwaokoa wote!*

Kutoka kwenye kalenda yake inaonyesha wazi kwamba upendo wake kwa watu ni kivutio cha kumwomba Mungu amwangazie na amsaidie katika kukamilisha mipango yake ya kitume. Kuamini katika Mungu na matendo ya kidunia, kwa Padre Jordan, ni nyuso mbili zenye ukweli uleule. Alikuwa mtu wa sala kiasi hicho kwamba wajibu wake wa kila siku haukumzuia kuendelea na sala zake. Wasaidizi wake wa karibu, mapadre waliozunguka pamoja naye kila siku, walishangaa kuona kwamba ingawa aliendelea kuzama katika sala, hata hivyo alihusika sawasawa na mahitaji binafsi ya wote. Shughuli za kawaida za kila siku hazikuogofya uhusiano wake wa ndani na Mungu.[368]



Mwanzilishi hakupata mgongano wowote kati ya sala na utume. Huduma kwa watu pia ni huduma kwa Mungu: ni dini; ambapo sala zisizojumlisha na huduma kwa jirani ni kujidanganya. Mmoja anaweza kushangaa kipimo kilicho sawa kati ya sala na kazi katika maisha ya Padre Jordan, lakini kumuiga ni vigumu. Anatufundisha kuwa tunaweza kupata maisha ya sala za kweli kwa njia ya watu wenzetu. Huruma yake kwa watu ilimfundisha kusali na mashaka yao yalimhimiza kuanzisha Shirika. *Shirika letu ni yote mawili: Kutanabahi haswa au sala na kazi. Kutanabahi kutawasaidia muangaziwe na Roho Mtakatifu. Ningependa kusema, kutanabahi*

[368] *Summarium*, Fr.Pancratius Pfeiffer, pp.16-17,& 9; Fr. Paschalis Schmid, p.233, & 1047

*au kusali ni kama kutia mafuta kwenye taa ili iwake na kuangaza. Bila hivyo taa itazimika…*[369] *Wokovu wa kweli ni nini? Mambo mawili hasa ni lazima: roho ya kitume na roho ya kitawa.*[370]

Mungu amempa mwanzilishi wetu juhudi kubwa kwa ajili ya roho, alifikiri juu ya wote watakaokuja baada yake, ili kwamba bado wawe sehemu ya moto huu wa kitume.

Padre Jordan alitambua kuwa lazima awe tochi ya moto wa kitume ambao alitaka kuwasha katika mioyo ya wafuasi wake. Tayari, mwanzoni mwa Shirika aliandika sala hii: *Ee Mungu Mwenyezi, peleka moto mtakatifu kwa watu, hasa kwa wanangu wa sasa na wa baadaye ili uweze kuendelea kuwaka katika mioyo yao – wakati wa maisha yao, kadiri wanavyoishi – mpaka mwisho wa nyakati, kwa heshima ya Mungu na kwa wokovu wa roho; uwaongeze kama nyota za angani.*[371]



Padre Cajetan Oswald anaandika: "Daima tumemheshimu Mwanzilishi wetu kama mtakatifu; kwa kweli, hatukufikiria kama mkubwa wetu. Wengine walitawala. Kamwe hatukuwa na sababu ya kupinga chochote katika yeye. Sababu ya ugonjwa wake wa mishipa ya fahamu, hakuweza kuchangamsha kwa uhuru au kirahisi, lakini wema wake na kiasi vilirekebisha sura yake. Uso wake haukung'aa kwa tabasamu ya ndani, usio wa kawaida, bila chochote cha kijuujuu."[372] Mmoja anaweza kumlinganisha mwanzilishi na mlima ambao kilele chake hukaa katika mwanga wote wa jua, wakati mteremko na mabonde bado yamefunikwa na giza la mawingu na ukungu. Ndani mwake kabisa, aliunganishwa na Mungu kwa mwanga wa tanabahi katika njia ya pekee sana, wakati uwezo wake wa kawaida ulikosa mwanga kwa udhaifu wa

369 Chap. 23.06.1899,DSS XXIII, 330
370 Chap. 17.05.1901,DSS XXIII, 426
371 DSS XXI, 5
372 Fr.Cajetan Oswald (APS I, 110)

kibinadamu au ugonjwa kiasi kwamba alikuwa kimya na kusikitika, kufa-moyo na mdhambi wakati huohuo. Kama mwanga na ukungu juu ya mlima vinavyoweza kuchanganyika, hivyo ugonjwa, shida ya nervu na upweke vinaweza kwenda pamoja na utakatifu. Udhaifu wa kibinadamu na nguvu ya Mungu vinakutana katika moyo wa mtu aliye mpweke. Mungu hahitaji ukamilifu wa kibinadamu, bali kuacha utashi wa mmoja tu kushiriki upendo wake wenye mateso, kusudi watu wote waweze kushiriki katika wokovu wa Kristo.



Fr.Otto Hopfenmuller,
Mkubwa wa kwanza wa Misioni ya assam, 1890

# IX

# Mwanzilishi na wafuasi wake.

Padre Jordan bado anaishi katika Shirika lake.Alisema katika hotuba yake kwenye mkutano: *Ni mtazamo wa Kanisa baada ya kifo cha Mwanzilishi, linadai kuwa macho kwa roho ya mwanzilishi.*[373] Kama mwanzishi, alijua kwamba anahusika au kuwajibika kwa Shirika lake: *Mara nyingi na kwa daima, hata kama siishi!*[374] Mwanzilishi hafi,kwa vile tunataka kujistawisha wenyewe na maisha yake ya kiroho,lakini *kama msipotilia maanani roho ya mwanzishi mtakuwa na Babiloni, na Babiloni iliyoanguka.*[375]

Mwanzilishi anaonyesha nguzo ya alama kwa Shirika lake. Wasalvatoriani wanamheshimu Mwanzilishi wao kiasi kwamba wanapenda kubaki katika mazungumzo ya kudumu naye.Kwa namna Fulani mmoja anaweza kuingia katika mazungumzo naye kila siku, mmoja anaweza

---

[373] Chap. 13.01.1899, DSS XXIII, 266
[374] Chap. 22.10.1897, DSS XXIII, 137
[375] Chap. 13.01.1899, DSS XXIII, 267

kumuuliza maswali na kupata majibu yake. Muungano huu wa kiroho unasababisha umoja ndani ya jumuiya za Shirika.

Hakuna sababu ya kumsifu mno Mwanzilishi kama mtu. Alikuwa na matatizo yake, udhaifu na mambo ya pekee kama yeyote kati yetu. Kwa hiyo, tumfikirie Mwanzilishi kama alivyokuwa mtu. Tofauti kubwa kati ya mwanzilishi na sisi ni kwamba Mwanzilishi alijua kupokea udhaifu wake na kujaribu kuurekebisha katika maisha yake yote. Alikubali udhaifu wake kama msalaba kwa sababu ya upendo wake kwa Kristo.

Sisi, Wasalvatoriani tunamheshimu mwanzilishi wetu kama mtakatifu kwasababu alipata kwa njia isiyo ya kawaida, kuwa karibu zaidi na Mungu katika mambo ya kawaida ya maisha ya kila siku, kwa sababu maisha yake yalikuwa mfano wazi wa Injili.Hata sasa, Mungu bado anaandika historia ya wokovu katika maisha ya watakatifu.



Kweli, Mwanzilishi alikuwa mtoto wa wakati wake. Teolojia, Maisha ya kiroho, Teolojia ya kichungaji ya wakati ule ilielezea maana ya mawazo na maneno yake yote. Asingeweza kutupatia elimu roho nyingine yeyote zaidi ya mafundisho ya Injili, pamoja na msisitizo wa wakati wake. Na tayari… hiyo ni tabia ya manabii: Alikimbia mbele ya wakati wake. Alielewa umuhimu wa uchungaji wa walei, ukumbakumba wa wokovu, umuhimu wa uchungaji wa uchapishaji. Mageuzi ya kweli ndani ya Kanisa daima yamefanywa na watakatifu: Watu walioishi na kutangaza imani yao katika njia ya asili.

Padre Jordan alihakikisha, kwa njia ya maisha yake, kwamba si hao wanaofanya kazi kwa nje zaidi ndio mitume wakubwa zaidi, bali hao wanaojiachia wenyewe kugeuzwa kuwa Kristo mwingine, katika upendo na katika sala. Mwanzoni mwa Vita Kuu ya I ya Dunia, aliandika: *Mungu Mwokozi aliimarishe Shirika lake kwa upole, unyenyekevu,*

*wanachama waliojazwa na ari ya kujitesa na kuhamasishwa kwa roho wake dhidi ya roho ya dunia hii. Mwenyezi awaunde ili muwe wafuasi wa kweli wa Mwokozi msulubiwa!*[376]

Anatuonesha njia rahisi ya utakatifu: *Tafuteni kuwa watakatifu kwa njia sahihi: Si katika ndoto zenu za kiroho lakini kwa njia ya mateso, kwa njia ya utii, ufukara na kuzifuata vizuri taratibu za kitawa…mkitaka kuwa watakatifu ni lazima muwe kama mfano wa kimungu…watu wa masikitiko,watu wanaojitesa, watu wenye kudharauliwa, watu wa kudhihakiwa, watu wa mateso.*[377] Anaandika kwenye kalenda yake: *Nawe, uwe nani, utamani neema kuu za ndani kama Mungu anazowajalia watakatifu wakuu kwa sababu hii: kuweza kumpenda Mungu kama wanavyoweza. Ndiyo, kwa sababu hii, hata tamaa ya kuwa na hamu kama watakatifu- kwa njia ambayo Mt. Theresa anaionyesha, wameendelea sana katika upendo wa Mungu- isingeweza kueleweka.*[378]




Maisha ya Padre Jordan yalikuwa ushuhuda wenye mwanga kwa yeyote anayetaka kuyaunda maisha yake toka kwenye vyanzo vya wokovu. Katika maisha yake ya kitume, Mwanzilishi alitaka, kwa njia ya upole kabisa, kuleta wazo kuu, tanabahi na matendo. Msingi wa utume wake ulikuwa ni kutumainia maongozi ya Mungu kama mwamba. Kwa namna hiyo, utume wake ulitekelezwa kwa undani zaidi na aliweza kuwa na matumaini wazi, yanayozidi hali yoyote ya chini.

Sasa ni wajibu wetu kutunza ndoto za Mwanzilishi wetu ziwe hai na kuchangia katika utekelezaji wake. Kwa kweli, "Mtazamo ukikosekana, hapo watu watakuwa wakorofi; wakati mtazamo huu ukiungana na mafundisho makuu, halafu mtazamo wa Mwanzilishi wetu na ndoto zake vitakuwa katika ukweli."

[376] DSS X, no.1169, 03.09.1914

[377] Chap. 20.04.1894, DSS XXIII, 23

[378] D I / 81-82



*Papa Yohane Paulo wa II akisali kwenye kaburi la Padre Jordan*

## Books published under *"Salvatorian Spirituality & Charism Series"*

## Vitabu vilivyotolewa na "*Maisha ya Kiroho ya Kisalvatoriani & Karama*"

1. **Fr. Winfrid Herbst, SDS,**
   *Father.Francis Jordan and His Practice of virtue(2001*)
   *Padre Francis Jordan na mazoezi yake ya Fadhila(2001)*

2. **Fr. Joseph Lammers, SDS,**
   *Drinking from our Source. (2001)*
   *Tunywe kutoka asili yetu (2001)*

3. **International charism Commission 'Kamati ya Kimataifa ya Karama'**
   *Salvatorian Key elements (Charism, Mission, Spirituality, Identity), Part I. (2002)*
   *Mambo muhimu ya Kisalvatoriani ( Karama, Utume, Maisha ya Kiroho, Utambulisho) Sehemu ya I (2002)*

4. **Fr.Gabriel Stapleton, SDS**
   *God's Foolish General- The Life of Father Francis Jordan Founder of the Salvatorians (2002)*
   *Kinachoonekana kuwa ni upumbavu kwa Mungu kina busara kuliko hekima ya binadamu: Maisha ya Fr. Francis Jordan Mwanzilishi wa Wasalvatoriani (2002)*

5. **Fr. Bernward Meisterjahn SDS**
   *…Lest any flesh should pride itself (2002)*
   *...Hakuna mtu awezaye kujivunia chochote mbele ya Mungu (2002)*

6. **Spiritual Diary of Fr.Jordan in Tamil (2002)** *Translated by Mrs. Mary Xavier*
   *'Kalenda ya Kiroho ya Fr. Jordan kwa Tamil' (2002*)

7. **Fr. Joseph Lammers,SDS**
   *The Spirituality of Fr. Jordan (2005)*

8. **Fr.  Pancaratius Pfeiffer, SDS**
   *Fr. Jordan and his foundations (2005)*

9. **Fr. Joseph Lammers,SDS**
   *Maisha ya Kiroho ya Fr. Jordan (2006)*
   Tafsiri ya Kiswahili na:
   Fr. Lazarus Msimbe, SDS